

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Thelathini na Nane - Tarehe 2 Agosti, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha kwa Mwaka 2002/2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Arusha International Conference Centre for the Year, 2002/2003*).

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

**MHE. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 355

### **Benki ya Dunia Kufadhili Utengenezaji wa Barabara za Manispaa**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa Manispaa karibu zote nchini zinafadhiliwa na Benki ya Dunia katika utengenezaji wa barabara za lami na mitaro katika barabara za Manispaa hizo lakini Manispaa ya Shinyanga haimo katika miradi hiyo tangu ianze mwaka 2000 hadi sasa. Je, ni lini sasa Manispaa hiyo ya Shinyanga itawekwa katika miradi hiyo ili barabara zake ziweze kutengenzwa na kuboreshwa na kuifanya Manispaa hiyo iwe kwenye hadhi inayofanana na Manispaa nyingine nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Huduma Mijini (*Urban Sector Rehabilitation Project*), pamoja na shughuli nyingine, ulihusika kutengeneza barabara na mifereji ya maji ya mvua kwa baadhi ya Manispaa. Mradi huu ulianza mwaka 1997 na ulitekelezwa katika Manispaa za Arusha, Moshi, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma na Majiji ya Mwanza na Dar es Salaam. Wakati huo Mji wa Shinyanga ulikuwa bado haujapewa hadhi ya Manispaa. Mradi huu umeghamiwa kwa kiasi kikubwa na mkopo toka Benki ya Dunia na unatarajiwa kufungwa rasmi ifikapo Desemba, 2004. Kwa hiyo, fedha zote zimekwishatumiwa. Chini ya Mradi huo, jumla ya Kilometra 104 za barabara za lami kati ya Kilometra 210 za barabara za lami zilizomo katika Manispaa hizo ndizo zimeweza kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya Mpango wa Kuzisaidia Serikali za Mitaa uitwao *Local Government Support Programme*, utakaowezesha kupatikana kwa fedha zaidi kwa ajili ya Bajeti za Maendeleo za Halmashauri katika maeneo ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, ujenzi wa miundombinu katika maeneo yenye makazi duni ya Manispaa za Jiji la Dar es Salaam na kujenga uwezo wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri, wa kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huu unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani milioni 121.7 na utaanza rasmi mwezi Januari, 2005 baada ya Serikali kuingia Mkataba na Benki ya Dunia mwezi Desemba, 2004. Ni matarajio ya Serikali kuwa, Halmashauri zitatumia vizuri fedha zitakazopatikana chini ya mpango huu ili kuleta maendeleo ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu zikiwemo barabara na mifereji

ya maji machafu ya Manispaa ya Shinyanga. Napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira na kuihamasisha Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kuboresha utendaji wake ili ifikie viwango vitakavyo iwezesha kushirikishwa katika Mpango huu.

Na. 356

### **Orodha ya Wafanyabiashara**

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY (k.n.y. MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi zote duniani hutegemea kuongeza Pato la Taifa kuitia walipa kodi na hasa wafanyabiashara wakubwa:-

- (a) Je, Serikali imenorodhesha wafanyabiashara wangapi katika taratibu hizo za ukusanyaji mapato?
- (b) Je, ni wafanyabiashara wangapi wanaolipa sahihi katika taratibu hizo?
- (c) Je, ni wafanyabiashara wangapi sugu wanaokwepa taratibu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi kodi haiongezi Pato la Taifa bali ni namna ya kukusanya rasilimali zilizopo kwa lengo la kuzitumia kwa njia inayotoa manufaa makubwa zaidi kwa jamii nzima. Pato la Taifa hutokana na ongezeko katika uzalishaji bidhaa na huduma na si vinginevyo. Kwa upande mwengine, ukusanyaji mzuri wa kodi huiongezea Serikali uwezo wa kutoa huduma za kiuchumi na kijamii. Matumizi ya aina hiyo yanaweza kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kwa kadri yanavyoboresha mazingira ya uzalishaji wa bidhaa na huduma katika uchumi husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2004, jumla ya walipakodi 236,392 walikuwa wameorodheshwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hii ni kwa mujibu wa Namba za Utambulisho za Walipakodi (*TIN*). Aidha, waajiriwa wasiopungua 795,809 wanalipa kodi chini ya utaratibu wa *Pay As You Earn*.

(b) Mheshimiwa Spika, sio rahisi kusema ni walipa kodi wangapi wanalipa kodi zao kwa usahihi kwa kuwa ni mlipakodi mwenyewe anajua kwa uhakika usahihi wa kodi anayolipa. Hata hivyo, kumbukumbu za Mamlaka ya Mapato Tanzania zinaonyesha ongezeko katika uwajibikaji, yaani *compliance* kwa walipa kodi. Kati ya mwaka 1998/99

na 2002/2003, idadi ya walipa kodi ya mapato iliongezeka kutoka asilimia 80 hadi asilimia 82 na walipa kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) kutoka asilimia 80 hadi asilimia 94 katika mwaka 1998/99 na 2000/2001.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na uchunguzi uliofanywa na Kitengo cha Upelelezi wa Kodi (*Tax Investigation*), cha Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa kipindi cha miaka mitatu 2000/2001 hadi 2002/2003, takwimu zinaonyesha kwamba, idadi ya makosa imekuwa ikipingua, toka makosa 474 mwaka 2000/2001 hadi makosa 247 mwaka 2002/2003, japo thamani ya makosa hayo imeongezeka kwa karibu mara mbili katika kipindi hicho.

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ametujibu kwamba hana hakika ya takwimu sahihi kwa wale ambao hawalipi kodi. Je, kutokuwa na takwimu hizo hahisi kwamba fedha za Serikali za Wananchi zinapotea?

Pili, je, hawa wanaokataa kulipa, yaani wakwepaji kodi sugu, je, Serikali ina mkakati gani ili kuwezeshwa kukusanya fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mlipa kodi mwenyewe ndio anajua kama analipa kodi sahihi ama halipi kodi sahihi. Lakini kwa wale wanaogundulika kwamba wamekwepa kodi, sheria zipo ambazo ni aidha kufilisiwa ama mali kukamatwa au kupelekwa Mahakamani. Tunasema kwamba, kama ikigundulika umekwepa kodi, inabidi ulipe asilimia 30 ya kodi ambayo unadaiwa halafu kama unakwenda Mahakamani au unakwenda kudai haki yako, basi umelipa hiyo asilimia. Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Wizara ya Fedha, imejitahidi sana kuelimisha walipa kodi na ninapenda nitumie nafasi hii kuwapongeza walipa kodi wanaolipa kodi kwa uaminifu, wamelisaidia sana Taifa hili kuongeza malipo ya kodi kutoka shilingi milioni 25 mpaka shilingi milioni 130 hivi sasa. Nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakwepaji kodi sugu, Serikali inapambana nao na Mamlaka ya Mapato imefanya mabadiliko makubwa katika vitengo mbalimbali na kuwa na *One Stop Centre* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, inatoa huduma nzuri na zenye ufanisi zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Kuna baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa yakifahamika kwamba, yana wakwepaji kodi sugu. Maeneo hayo ni pamoja na Idara ya Mafuta ya Petroli, ambayo juzi Serikali imechukua hatua na toka imechukua hatua toka Bajeti iliyopita, makusanyo kwenye Sekta ya Petroli yameongezeka sana. Juzi tumefunga *flow metre* na hatua nyininge za kiutendaji.

Pili, eneo lingine ambalo lilikuwa na matatizo ni Kodi ya Mapato. Sheria ya Kodi ya Mapato iliyopitishwa imeziba mianya mingi sana ambayo wakwepaji kodi walikuwa wanaitumia kutokana na Sheria hii ya Kodi ya Mapato kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe taarifa kwamba, Serikali imejizatiti vilivyo katika kuongeza mapato ya Serikali na napenda niwaombe wafanyabiashara wasiwe

wanakwepa kodi kwa sababu fedha zinazokusanywa na Serikali maendeleo yake yanaonekana.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Wananchi wengi katika nchi hii hawalipi kodi kwa sababu hawajawezeshwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima wadogo wadogo, wavuvi, wafanyabiashara wadogo wadogo ili wawe na uwezo wa kuchangia mapato ya Serikali yao kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali? (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe, labda unajua namna ya kuwawezesha. Hebu jibu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, hakuna Serikali yoyote duniani inayowezesha raia wake kulipa kodi. Hakuna! Raia wanajiwezesha wenyewe. Sisi tunamfuata yule ambaye amekwisha jiwezesha, ana ziada na anatakiwa alipe kodi, ndio huyo tunayemtoza. Lakini hiyo ni kwa kodi ya mapato. Lakini kwa kodi ya thamani, *VAT* ni mtu wa kawaida anapokwenda kununua mali dukani ndio anayelipa kodi hiyo. Kwa sababu kila mtu kila wakati ananunua kitu, basi hakuna wala sababu ya kuzungumza tutamwezeshaje mtu huyo kwa sababu anapokwenda kununua bila shaka ameshajiona ana uwezo wa kununua. Isipokuwa niseme kwamba, kama Mheshimiwa Mbunge, anataka kuuliza swali jipya la uwezeshaji, anaweza akafanya hivyo na atajibiwa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, eneo hili la *VAT* bado lina utata, watu wengi bado wanakwepa kodi ya *VAT* na mimi nataka kuanza kutoa taarifa kwamba, mwaka huu wa fedha tukimaliza tu Bunge hapa, nataka binafsi nisimamie watu walipe kodi za *VAT*. Ule mchezo wa kupewa risiti bila *VAT*, tumaini langu ni kwamba, utakwisha mwaka huu na kuendelea. (*Makofî*)

Na. 357

### **Kilimo cha Minazi Tanzania**

**MHE. RAMADHANI H. KHALFAN** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania inaaminika kuwa na zaidi ya minazi milioni ishirini na tano inayolimwa katika sehemu mbalimbali za nchi hii, yaani Tanzania Bara na Tanzania Visiwani; na kwa kuwa zao hilo linalimwa na wakulima wadogo wadogo wapatao milioni moja wanaomiliki viunga vya ekari moja hadi tatu na imeoteshwa kwenye eneo lenye ukubwa usiopungua hekta 300,000; na kwa kuwa Minazi ni zao la chakula na la kibiashara na lenye matumizi mengi sana hasa kwa wakulima wa maeneo ya Pwani; na kwa kuwa mwaka 1979 Serikali ilianzisha na kuendesha mpango wa miaka 25 wa *NCDP* wa kuendeleza zao hilo ambao unaishia mwaka huu 2004:-

(a) Je, baada ya mpango huo kufikia mwisho wake ni kitu gani kitakachofuata baada ya hapo?

(b) Katika nchi hii tunazo Mamlaka/Bodi za Mazao mbalimbali kama vile Pamba, Chai, Korosho, Kahawa, Tumbaku na kadhalika, je, ni kasoro gani zinazolifanya zao la Minazi likose kuwa na Bodi/Mamlaka kama ilivyo kwa mazao mengine?

(c) Je, Serikali inakubali kuwa inalipuuza zao hilo muhimu kimakosa na kwamba hatua yake hiyo inazinufaisha sana nchi za Mashariki ya mbali na kumuumiza mwananchi?

#### **WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Ramadhan Hashim Khalfan, Mbunge wa Bagamoyo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa Taifa wa Kuendeleza Minazi unaojulikana kama *NCDP* ulianza kutekelezwa na Serikali mwaka 1979 kwa gharama ya Sh.8,951,526,289/= ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Shirikisho la Ujeruman, mkopo kutoka Benki ya Dunia na michango ya Serikali zote mbili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano.

Kwa kuwa utafiti wa mazao ya miti kama vile minazi huchukua muda mrefu, mpango huo ulipangwa kuchukua miaka 26 na unatarajiwa kumalizika tarehe 30 Novemba, 2004. Chini ya mpango huo, inakadiriwa kwamba, uzalishaji wa nazi umeongezeka kutoka nazi milioni 555 katika mwaka wa 1979 hadi nazi milioni 850 zinazozalishwa kwa sasa, yaani nyongeza ya nazi milioni 295. Ili kuendeleza mafanikio hayo, mpango utakapofika mwisho, Serikali itaendeleza shughuli za utafiti na ugani wa zao hilo kwa kutumia fedha zake yenewe wakati ikizungumza na Wahisani kuona uwezekano wa kuongeza muda wa mradi.

(b) Zao la minazi lilikuwa likishughulikiwa na *GAPEx*, baada ya Shirika hilo kuvunjwa mwaka wa 1986, Serikali iliona ni bora kuendelea kutafuta ufumbuzi wa matatizo yaliyokuwa yanalinkabili zao hilo na kusababisha uzalishaji wake ushuke. Kwa kuwa sasa uzalishaji wa zao hilo umeongezeka, Serikali itaangalia uwezekano wa kuanzisha Bodi ya zao hilo na kwa kuanzia litashughulikiwa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo tunatarajia itaanishwa wakati wowote.

(c) Serikali haikubali kwamba inalipuuza zao la minazi. Serikali ndiyo ilianzisha Mpango huu wa Minazi tunaouzungumzia na inaendelea kutenga fedha katika Bajeti yake kwa mfano, katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, Serikali ilitenga Shilingi bilioni 70 na katika Bajeti ya mwaka huu imetenga Shilingi milioni 100. Kutokana na maelezo ya sehemu (a) na (b) ya swal hili, ni dhahiri kwamba, Serikali inafanya kila linalowezekana kuhakikisha zao hili linakuwa na maendeleo mazuri.

**MHE. RAMADHAN H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambayo nakubaliana nayo na ninashukuru kwamba yanatia moyo, labda angetuambia itachukua muda gani kufikia hatua ya kuanzisha hiyo Bodi ya Mazao Mchanganyiko tuweze kuwa na uhakika kwamba, hili zao linaendelea kupata huduma? (*Makofi*)

Pili, kuna tatizo la mdudu chonga ambaye anamaliza minazi hii. Ukiangalia maeneo yote ya minazi utakuta vilele vya minazi vinakatika inabakia miti tu imesimama haina makuti au tuseme haina kilele pale na haya matatizo yapo karibu nchi nzima. Mkuranga ukienda utaona, ukiingia Tanga Mjini eneo lote linaonekana, hali mbaya, vilevile Mafia, kila mahali. Je, Serikali ina mpango gani wa kumdhiliti mdudu huyu chonga ili tuwe na uhakika kwamba minazi inaendelea kuishi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tunatarajia Bodi ya Mazao Mchanganyiko itaanzishwa mwaka huu kwa sababu maandalizi karibu yote ya kuanzisha yameshakamilika. Kwa hiyo, tunatarajia baadaye mwaka huu hii Bodi itaanzishwa na kwa kuwa itahitaji kuwa na Sheria, tutarudi Bungeni hapa kuomba idhini ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa sana la huyu mdudu ambaye anaharibu minazi na ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Ramadhan Khalfan kwamba, Kituo chetu cha Utafiti wa Minazi kinafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba, tunapata ufumbuzi wa tatizo hili mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali mwaka huu inasema imetenga Shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuliendeleza zao la minazi, labda kwa kutumia pesa hizi Serikali haioni kwamba kuvisaidia viwanda kwa mfano kuna Kiwanda kinachoitwa *Mafia Coconut Limited* au *Mikumi Milling* kilichokuwa kule Mafia, ambacho kina mashamba makubwa na pia kina uwezo wa kuweza kukusanya nazi za Wananchi na kutengeneza mafuta ambayo mafuta haya kwa nchi nyininge...

**SPIKA:** Sawa, uliza swali.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Ndio hilo, kwamba tatizo kuvipa uwezo viwanda kama hivi na Wananchi ili zao hili liweze kupata mnunuzi kuliko sasa hivi mazao haya yanapokuja Kariakoo wafanyabiashara wa sokoni hujipangia bei wanazotaka wao na kuwdhalilisha wakulima wa minazi kama wa Mafia?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *Mafia Coconut Limited* ni Kampuni ya watu binafsi, ningeshauri Kampuni hii itafutie mitaji ya kuwekeza katika zao hili kutoka kwenye vyombo vya fedha na nina hakika kutokana na mkazo ambao sasa hivi Serikali inatilia kilimo, Waziri wa Fedha ataipa *guarantee* ili waweze kupata mkopo. (*Makofi*)

### **Mkanganyiko wa Utendaji**

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma za ugani kwa kilimo na ufugaji katika miaka ya huko nyuma zilitolewa kitaalamu ambapo Maafisa Ugani walifunzwa kwa kuzingatia mazao kama vile Tumbaku, Pamba na kadhalika, lakini sasa wataalam hao wamechanganywa tu bila kujali mazao wahudumiayo, yaani wale wa Kilimo wamechanganywa na wale wa Mifugo, Ndonobo, Kuku na kadhalika; na kwa kuwa Maafisa hao wanatoka kwenye Wizara mbili tofauti, yaani Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Kilimo na Chakula; na kwa kuwa mafunzo mahsusini ya taaluma hizo hayatolewi tena:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ufanisi wa huduma za ugani umezorota vibaya sana?

(b) Kama watumishi hao waliochanganywa kama chumvi na sukari watakapostaifu, je, Serikali itajitoa katika utoaji wa huduma za ugani kama ilivyojitoa katika biashara?

(c) Je, ni Afisa gani kati ya hao angefaa zaidi kuwaongoza wenzake kati ya yule wa Kilimo au Mifugo au wa Ndonobo kwenye eneo lenye Ndonobo wengi?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a), (b) na (c), ningependa kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa 1990, Serikali iliamua kuwapa wanafunzi waliokuwa wakichukua mafunzo ya Astashahada Vyuoni mafunzo ya taaluma za kilimo cha mazao na ufugaji kwa pamoja, uamuzi huo ultokana na ukweli kwamba, kulikuwepo na upungufu mkubwa wa Wataalam wa Kilimo na Mifugo. Aidha, ulilenga kumpa uwezo mtaalam mmoja kumhudumia mkulima kwa kilimo cha mazao na kwa ufugaji pia. Katika mwaka 1998, iliamuliwa kwamba, Wataalam wa Ugani wa Kilimo na Mifugo wawekwe chini ya Serikali za Mitaa chini ya Mpango wa kuhamishia Madaraka ya Serikali kwenye Serikali za Mitaa. Watumishi hao wanapangiwa kazi na kusimamiwa na Serikali zao za Mitaa na siyo Wizara zinazohusika.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

(a) Kuzorota kwa Utendaji kazi wa Maafisa Kilimo na Mifugo hakutokani na wataalamu hao kuwa na taaluma za kilimo na mifugo kwa pamoja. Kuunganishwa kwa taaluma hizo kungemrahisishia mkulima kupata utaalam kwa wingi na kwa urahisi zaidi.

Tatizo linatokana na usimamizi hafifu, ugumu wa Maafisa Ugani kuwafikia wakulima wengi wanaolima maeneo madogo na yaliyosambaa katika maeneo makubwa na ukosefu wa vitendea kazi hususan usafiri na vifaa vya kupimia udongo na mifugo.

(b) Serikali haikusudii kujitoa katika utoaji wa huduma za ugani. Serikali inaendelea kuwapatia wataalamu hao mafunzo na kuwasambaza Wilayani kulingana na mahitaji ya maeneo mbalimbali ya nchi. Katika mwaka uliopita tulisambaza magari 52 ili kuwarahisishia usafiri.

(c) Afisa anayefaa kumwongoza mwenzake ni yule mwenye sifa bora za uongozi zikiwa ni pamoja na elimu, uzoefu, uwezo wa kuongoza na uadilifu. Chini ya Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya, wapo wataalam bingwa wa mazao, mifugo, zana za kilimo na kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na kadhalika, ambao wanasaidia kuongoza wenzao.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, amesema wataalam hawa wanasmamiwa na Serikali za Mitaa, lakini kwa uhakika Viongozi wa Serikali za Mitaa, yaani Mkurugenzi kwa kawaida sio mtaalam wa kilimo na mifugo, ndorobo na kadha wa kadha. Je, Serikali inathibitishaje kwamba, huyu Mkurugenzi ni kweli anawasimamia ipasavyo wakati ye ye mwenyewe hana utaalam, wakimdanganya atasemaje? (*Makofii*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya halazimiki kuwa na taaluma zote zinazohitajika katika Wilaya yake. Yeye ni Meneja, kazi yake ni kushirikiana na wataalam wake ili waandae mipango na washirikiane kusimamia katika kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, nimewahi kuwa Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya na tulifanya kazi zetu kwa ufanisi kwa kushirikiana kama timu ya Wilaya na ninategemea Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya ndivyo wanavyofanya kazi. (*Makofii*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba watumishi hawa wamekuwa wakiwijibika kiutaalam katika Wizara ya TAMISEMI, kiutendaji na kiutaalam katika Wizara zao mama husika.

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba hilo linawafanya wajikanganye katika utendaji wao wa kazi na hasa katika suala zima la utoaji wa ripoti za taarifa zao mbalimbali za kiutendaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, jibu swali la mwisho la nyongeza.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naomba tuelewane, hawa watumishi hawawajibiki kwa TAMISEMI, hawawajibiki kwa Wizara ya

Kilimo, hawajibiki kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, wanawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya yao. Kwa hiyo, wameunganishwa kwa pamoja katika Wilaya kuunda timu ya wataalam katika Wilaya. Kwa hiyo, wataandaa ripoti zao watazipeleka kwa Mkurugenzi Mtendaji, ambaye atazisambaza *accordingly* kwenda kwenye Wizara mbalimbali zinazohusika. Kwa hiyo, sitarajii wajikanganye hata kidogo, labda wapende tu kufanya hivyo. (*Makofî*)

Na. 359

### **Utoaji wa Hati za Kusafiria Nje ya Nchi**

#### **MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Uhamiaji hapa nchini ndiyo pekee inayohusika na utoaji wa hati za kusafiria:-

- (a) Je, kwa nini kunakuwa na usumbufu wa kupatikana kwa hati za kusafiria kwa Wananchi wanaoishi Zanzibar (Unguja na Pemba)?
- (b) Je, ni hati ngapi za kusafiria zilitolewa kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2003 ukiondoa za wale raia wanaokwenda Makka kwa Ibada ya Hija?
- (c) Je, ni gharama kiasi gani kwa ujumla ambazo Mtanzania anapaswa kulipa ili apate hati ya kusafiria?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Jimbo la Gando, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Hati za Kusafiria Nje ya Nchi hutolewa kwa kuzingatia Sheria ya Pasipoti na Hati za kusafiria Na.20 ya mwaka 2002. Sheria hiyo imetoa masharti kadha kwa waombaji wa pasipoti, mionganu yakiwa, mwombaji kuthibitisha uraia wake na mmoja wa wazazi wake kwa kuwasilisha Cheti cha Kuzaliwa au Kiapo cha Kuzaliwa nchini. Kuwasilisha ushahidi au sababu ya safari yake, kwa mfano, matibabu, masomo, biashara, utalii na kadhalika.

Masharti haya yamewekwa sio kwa ajili ya kuleta usumbufu kwa Wananchi, bali yana nia ya kuweka udhibiti wa matumizi mabaya ya hati ya kusafiria. Baadhi ya Watanzania hutumia pasipoti kufanikisha vitendo vya uhalifu. Kwa mfano, kusafirisha madawa ya kulevyia (*Drug Trafficking*). Aidha, utaratibu na masharti haya hutumika pande zote za Muungano bila ya ubaguzi wowote.

- (b) Mheshimiwa Spika, jumla ya pasipoti 14,644 zilitolewa Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba kati ya mwaka 2000 hadi 2003. Kwa mchanganuo ufuatao:

Mwaka 2000 zilizotolewa pasipoti 3,003. Mwaka 2001 zilizotolewa pasipoti 3,343. Mwaka 2002 zilitolewa pasipoti 4,189 na mwaka 2003 zilitolewa hati 4,109. Idadi hii ni baada ya kuondoa wale waliopata pasipoti kwa ajili ya kwenda Makka kuhiji.

(c) Mheshimiwa Spika, gharama za hati za kusafiria hutofautiana kulingana na aina ya hati inayohitajika kama ifuatavyo: Hati ya kusafiria kawaida (*Ordinary Passport*), gharama yake ni Sh.20,000/=. Hati ya kiutumishi (*Service Passport*), gharama yake ni Sh.15,000/=. Hati ya kidiplomasia gharama yake ni Sh.15,000/=, hati ya Afrika Mashariki (*East African Passport*), gharama yake ni Sh.10,000/= na hati ya dharura (*Emergency Traveler's Document*), gharama yake ni Sh.5,000/=.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Waziri, amesema nia siyo kuleta usumbufu, lakini kutafsiri neno usumbufu nafikiri napata tabu kwa sababu kumtoa mtu Bukoba kumwambia akachukue *passport* Dar es Salaam, sijui kama huo sio usumbufu. Hata hivyo, napenda kuelewa ni lini Serikali itaamua kutoa *passport* angalau kanda maalum kama si mikoa yote ili kuwaondolea Watanzania matatizo ya kupata hati?

Pili, suala la upatikanaji wa *passport* kuna utaratibu mwingi ambao unaashiria namna ya kukatiwa mtu kitu kidogo ili ipatikane *passport* kwa urahisi. Ni lini Serikali italifanya hili suala la kupata *passport* ni haki ya raia ni siyo *privilege* ili Watanzania walio na nafasi ya kununua *passport* wasisumbuliwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la usumbufu kwamba, mtu akiwa Kigoma anafuata *passport* Dar es Salaam, nataka kusema kwamba, utaratibu uliopo ni kwamba, mtu kama yuko Kigoma au yuko katika Mkoa wowote, fomu za kuomba *passport* zinapatikana pale pale katika Ofisi ya Uhamiaji katika Mkoa wake anajaza, akishakamilisha kila kitu pale ni wajibu sasa wa Afisa Uhamiaji wa Mkoa ule yeye kuzipeleka kule Dar es Salaam kuchukua *passport* na kuziacha katika Mkoa unaohusika. Kila raia anaipatia pale pale kwenye Mkoa wake. Lakini baadhi ya watu kwa sababu zao hupenda tu wao wenye kwenda Dar es Salaam, Makao Makuu, kuzifuata kwa hiari yao wenye. Lakini kwa kweli *passport* zinapatikana katika Mkoa ule alipo.

Sasa ametoa wazo kwamba, je, haiwezekani *passport* zikakaa huko huko kwenye Mkoa au kwenye Kanda. Zamani tulikuwa na utaratibu kama huo, bahati mbaya ukatumika vibaya. Ndiyo maana zote zikapelekwa Makao Makuu, sasa hivi tuko katika hali ya kutazama kama tunaweza tena tukarudisha utaratibu wa zamani baada ya kuweka udhibiti.

Kuhusu utaratibu kwamba, utaratibu mrefu, unaashia rushwa. Kama nilivyoleza utaratibu siyo mrefu, mtu unajaza fomu katika mkoa wako kila kila kitu kinaishia pale na *passport* utaletewa pale pale kwenye mkoa wako, hakuna usumbufu, najua baadhi ya watu wanalamika kule kuambiwa kaape, lete cheti cha kuzaliwa, kaape Mahakamani, baadhi wanatafsiri kama huo ni usumbufu. Lazima tujiridhishe kwamba, huyu

tunayempa *passport* ni raia wetu. Lazima tujiridhishe, vinginevyo tutatoa tu *passport* kwa watu ambao sio raia wa nchi hii. (*Makofî*)

Kwa hiyo, naomba Watanzania waelewe kwamba, baadhi ya shughuli ambazo wanatakiwa wafanye ni kwa ajili ya kudhibiti utoaji wa *passport* zisiangukie katika mikoa katika mikono ya watu ambao sio raia. (*Makofî*)

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalî la nyongeza. Kwa kuwa waombaji wengi wa *passport* wanatoka Kisiwa cha Pemba ambao wanakuwa na asili ya uarabu, kumbukumbu zao huwa zinaonekana za kiuraia, hazieleweki vizuri zaidi. Lakini pia hata wale ambao ni weusi kama mimi, wengine hujiandika ni Waarabu, je, hiyo inaonekana kwamba pengine inaleta usumbufu katika kutambua ni nani raia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Taifa letu ni Taifa lenye mchanganyiko mkubwa sana. Ni Taifa ambalo lina Watanzania wa aina mbalimbali, makabila mbalimbali, dini mbalimbali na rangi mbalimbali. Lakini wote ni Watanzania na wote hao wakija wa rangi mbalimbali, kabila mbalimbali, utaratibu ni huu huu tutake kujiridhisha, uraia wake na kila kitu. Ahsante sana. (*Makofî*)

Na. 360

### **Askari Polisi na Gari - Kituo cha Polisi Nduguti**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni kweli usiofichika kwamba, Polisi wamejitahidi sana kufanya kazi nzuri ya kulinda usalama wa raia na mali zao hapa nchini pia tunaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mwaka hadi mwaka kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, ununuzi wa vifaa, mafunzo na kadhalika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza askari katika Vituo vya Polisi vya Nduguti, Mkalama na Iguguno ambavyo vina maeneo makubwa ya kufanya kazi?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa gari kwa kituo cha Nduguti ambacho kiko mbali na Wilaya na ndicho kituo kiichoko katika Wilaya ya Iramba Mashariki kwa ajili ya kuyahudumia maeneo yote yale yanayopakana na Mikoa ya Manyara, Arusha na Shinyanga?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Nduguti badala ya kukaa kwenye nyumba ambayo haina mahabusu na chumba cha kutunzia silaha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalî la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za Jeshi la Polisi, idadi ya askari katika Kituo cha Polisi hutegemea wingi na uzito wa makosa yanayotendeka katika eneo husika, iwapo eneo husika linakabiliwa na matukio mengi na makubwa ya uhalifu, Serikali hupeleka askari wengi katika kituo hicho ili kukabiliana na hali ya uhalifu uliopo. Ni kweli kuwa vituo vya Polisi vya Nduguti, Ibaga na Iguguno, vina maeneo makubwa, lakini hali ya uhalifu si mbaya kulinganisha na maeneo mengine kiasi cha kuhitaji kuongeza idadi ya askari katika vituo hivyo.

Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu mwaka 2001 hadi 2003, idadi ya makosa makubwa katika kituo cha Nduguti na Ibaga kwa pamoja yalikuwa ni jumla ya makosa 28. Katika Kituo cha Iguguno katika hii miaka mitatu makosa makubwa yalikuwa ni 16 tu. Yako maeneo ya nchi ambako idadi ya makosa katika kipindi kama hicho huweza kufikia hata zaidi ya 200. Kutokana na takwimu hizi, Serikali kwa sasa inaona ipo nguvu ya kutosha kukabili hali ya uhalifu katika maeneo hayo, hivyo hatuna mpango wa kuongeza nguvu ya ziada.

(b) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Nduguti hivi sasa kinahudumiwa na gari *STJ 879 Land Rover 110*, ambayo ipo Kiomboi, Makao Makuu ya Wilaya, hasa yanapotoka matukio makubwa yanayotakiwa kufuatiliwa kwa kutumia gari. Serikali kwa sasa inao mpango wa kuongeza gari la pili katika Ofisi ya OCD Iramba, lakini bado haina uwezo kifedha wa kununua magari kwa vituo vilivyo nje ya Makao Makuu ya Wilaya, kama Kituo cha Ibaga.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kujenga jengo la Kituo cha Polisi cha Nduguti. Lengo la Serikali kwa saa ni kujenga kwanza majengo ya vituo vya Makao Makuu ya Wilaya hasa zile Wilaya ambazo hazijapata majengo ya Polisi ya Wilaya na kazi hiyo tunaifanya kuzingatia hali ya bajeti. Tunawashauri Wananchi wa Nduguti waanzishe ujenzi wa Kituo hicho na Serikali tutaunga mkono kulingana na uwezo wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mgana Msindai, kwa kufuatilia na kupigania maendeleo ya Jeshi la Polisi katika Jimbo lake. (*Makofî*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba, gari inayohudumia Iramba ya Mashariki inakaa Kiomboi ambako ni mbali na eneo hilo karibu kilomita 50. Je, Serikali haioni kwamba, sasa kuna umuhimu wa kupeleka gari likae Iramba Mashariki ambako Makao Makuu yake ni Nduguti liweze kuhudumia eneo hilo lote hasa wakati huu ambapo Bunge limepitisha bajeti nzuri kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi? (*Makofî*)

Pili, kwa kuwa Wananchi wa Nduguti toka zamani walikuwa tayari kujenga kituo chao, lakini Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walikuwa hawajaonyesha nia ya kusaidia. Je, sasa Wananchi waanze kujenga na Serikali iwe tayari kusaidia kwa ujenzi wa kituo hicho? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu itapeleka gari lingine la Polisi katika Wilaya ya Iramba. Sasa Mheshimiwa Mbunge, anasema gari hilo litakaloongezeka liende Iramba Mashariki, ni kwamba, kwa taratibu za kazi za kipolisi, hili gari ambalo tutaongeza si kwa Wilaya ya Iramba tu ni katika baadhi ya Wilaya, hili litakuwa ni kwa matumizi ya Afisa Upelelezi wa Wilaya na ni gari moja, yatakuwa magari mawili, moja la *OCD* la pili ni la Ofisa Upelelezi wa Wilaya (*CID*), ili kazi ziweze kwenda vizuri. Kwa hiyo, halitakwenda Iramba Mashariki.

Lakini nataka kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Kituo cha Nduguti iko *Radio Call*, kwa hiyo, kama likitokea jambo ambalo ni la dharura linahitaji gari, basi Mkuu wa Kituo cha Nduguti, atawasiliana na *OCD* halafu huduma ya gari itatoka Kiomboi. Miaka ijayo bajeti ikiruhusu, tunao mpango vilevile kufikisha magari katika Vituo vya kwenye Tarafa.

Suala lake la pili kwamba, Wananchi wa Nduguti walikuwa na nia ya kujenga Kituo lakini Wizara yangu ilikuwa haijaonyesha nia. Sasa katika jibu langu msingi imedhihirisha kwamba, sasa nia tunayo, waanze kujenga na sisi sasa nia ya kuwaunga mkono kuwachangia sasa ipo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane.

Na. 361

### **Mikanda ya Vitanda kwenye Train**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA (k.n.y. MHE. ESHA H. STIMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, akina mama wengi wanapenda kusafiri kwa treni wakiamini kuwa wanapata usalama na utilivu katika safari zao hasa wale wanaosafiri kwa Daraja la Kwanza na la Pili na kwa kuwa kuna kero moja katika vitanda vya kulala kwa kukosa mikanda ya kufunga wakati wa kulala sehemu ya juu na kati. Je, Shirika litafanya matengenezo ya kuweka mikanda ya vitanda ili akina mama wa kawaida, watoto na wagongwa, wajisikie salama wanapolalia vitanda hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esha Hassan Stima, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika limefanya matengenezo ya kuweka mikanda ya vitanda kwenye mabehewa ya Daraja la Kwanza na Daraja la Pili ili kuhakikisha usalama wa abiria wakiwemo akina mama wa kawaida, watoto na wagonjwa wakati wanapolalia vitanda hivyo unapatikana.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, lakini nilikuwa napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa akina mama kulingana na majukumu yao kimaumbile wakati mwagine hulazimika kusafiri wakiwa wajawazito na wakati mwagine wakiwa na watoto wadogo, lakini Shirika la Reli linapowapanga katika vyumba halizingatii kwamba inawapanga akina mama hao ni wangapi wenye watoto au wajawazito kwa sababu kama mjamzito kwa kweli kupanda kitanda cha juu au katikati inakuwa ni hatari kwake na vilevile watoto.

Je, ni lini Shirika la Reli litazingatia kuwapanga akina mama katika vyumba kwa kukadiria wenye watoto wasio wengi sana katika chumba kimoja ili watoto wasafiri kwa raha na mama zao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Elizabeth Batenga kuwa, kama akina mama wajawazito watafanya *booking* zao mapema na kuashiria kwa *TRC* kwamba, mimi nafanya *booking* mama mjamzito na mwenye watoto, shughuli hiyo itafanywa. Lakini hivi hivi tu, *TRC* haiwezi kujua kwamba, huyo aliyefanya *booking* leo ni mjamzito au huyu ana watoto wachanga ambao lazima wakae chini. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane katika hilo ili *TRC* ifanye wajibu wake ipasavyo. (*Makofi*)

Na. 362

### **Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa haki za watoto na kwa kuwa umri unaoruhusu mtu kuingia katika ndoa Tanzania ni miaka kumi na sita:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani za kulinda haki za watoto hususan wa kike kwa kukabili na kuzuia mila potofu za baadhi ya makabila za kuwaoza watoto wa kike kabla ya kufikia umri wa ndoa?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kujenga shule za sekondari za kutwa, hosteli za watoto wa kike, ili wapate malezi mazuri, usalama wa elimu nzuri na kulinda mpango wa elimu ya msingi kwa waliokosa (MEMKWA) pale ambapo baadhi ya wanafunzi wamekuwa wana ndoa kabla ya kuandikishwa shule?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na hiyo Mikataba ya Kimataifa aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, imetunga Kanuni inayomlinda mtoto wa kike mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari, iitwayo "*The Education (Imposition of Penalties to Persons who Marry or Impregnate a School Girl) Rules, 2003*". Kanuni hii ambayo ilitungwa mwezi Novemba, 2003 inatoa adhabu kwa wale wote wanaowakatiza masomo watoto wa shule kama ifuatavyo:-

(i) Mzazi au mlezi ye yeyote atakayemwoza mwanafunzi atapata adhabu ya faini isiyozidi shilingi 100,000/= au kifungo kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili.

(ii) Mtu ye yeyote atakayepatikana na kosa la kumwoa mwanafunzi, anastahili adhabu ya faini isiyopungua shilingi 300,000/= na isiyozidi shilingi 500,000/= au kifungo kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili kama Mahakama itakavyoona ifaa. (*Makofi*)

(iii) Mtu ye yeyote atakayepatikana na kosa la kumpa mimba mwanafunzi anastahili adhabu ya kifungo cha miaka isiyopungua mitatu na isiyozidi miaka sita bila faini. Pale ambapo vifaa viro, utatumika ushahidi wa *DNA* wa kupima mate au damu ya mtoto na huyo mtuhumiwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maelezo ya utekelezaji wa kanuni hii yametolewa hivi karibuni katika Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2004 wa tarehe 15 Aprili, 2004, uliotolewa na Afisa Elimu Kiongozi kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, unaowataka kuwachukulia hatua wote wanaowakatiza masomo wanafunzi wasichana kwa kuwapa mimba, kuwaoa au kuwaoza na taarifa za hatua hizo ziwasilishwe Wizarani.

(b) Mheshimiwa Spika, kuititia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES 2004 - 2009), jumla ya madarasa 5,633 yatajengwa katika shule za sekondari za kutwa ifikapo 2009 na shule mpya 1,500 zitaanzishwa. Aidha, Serikali inakusudia kutoa ruzuku ya maendeleo kwa shule za kutwa kwa ajili ya ujenzi wa hosteli hususan za wasichana katika Wilaya zenye mazingira magumu. Hatua hii itachangia kuhakikisha kuwa watoto wa kike wanapata malezi mazuri, yenye usalama na elimu nzuri.

(c) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Elimu ya Msingi kwa walioikosa (MEMKWA), ni wa mpito na sio wa kudumu na inategemewa kuwa watoto wote wa umri wa miaka saba watakapokuwa wanaandikishwa kuanza darasa la kwanza bila kukosa, MEMKWA haitahitajika. Mpango huu una sehemu mbili:-

(i) Kundi rika la kwanza, wa miaka 11-13 amba ni wa elimu ya msingi na watakaofaulu Darasa la IV katika kundi hilo wataingia Darasa la V katika mfumo rasmi kutegemea umri; na

(ii) Kundi rika la pili, wa miaka 14 -18, ambapo endapo mtoto au endapo mhusika atakuwa katika ndoa kabla ya kuandikishwa shule, katika kundi rika hilo, ni

lazima kuwepo na makubaliano kati ya wanandoa kabla ya kuanza masomo na atakayefaulu Darasa la VII ataendelea Kidato cha Kwanza katika sekondari.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri na kazi nzuri anayofanya katika Wizara ya Elimu na Utamaduni. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wahalifu wanaovunja hii Sheria baada ya hapo aidha wanafungwa ama wanapewa adhabu. Je, isingekuwa vyema wale wahalifu wakapewa jukumu la kuwasomesha hawa vijana na kuwalipia gharama zao badala ya kuwaacha?

(b) Kwa kuwa Sheria hi inatoa adhabu kwa mhalifu na kumwacha mwanafunzi wa shule bila kujua hatima yake. Sheria inasema nini kuhusu mtoto huyo aliyepewa mimba au kuozeshwa wakati ambapo amekatishwa masomo, Serikali haina mpango wa kumlipia?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, sikusia vizuri pale mwisho.

**SPIKA:** Swali lako la pili, Mheshimiwa Waziri hakulisikia sawasawa, lile la pili, hebu lirudie.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Kwa kuwa Sheria inatoa adhabu kwa wahalifu, lakini haisemi ni vipi itamsaidia mwanafunzi yule ambaye amepata mimba ama kuozeshwa. Je, Serikali haina utaratibu wa kusomesha watoto wa aina hiyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, hili la kwanza la kwamba hawa wahalifu wangepewa jukumu la kuwasomesha, lakini utakuta kwamba, katika kila eneo wahalifu hawa tunategemea wafungwe waende gerezani. Kwa hiyo, jukumu la kusomesha na mtu yuko gerezani si rahisi.

Hili la pili, kwamba, Serikali ina mpango gani kwa hawa watoto ambao wamepatwa na matatizo haya, sasa mpango uliopo ni wa Kiserikali, mtoto akipata mimba ni kosa la kufukuzwa shule kwa sababu ya ile kanuni nyingine ambayo nimekwishaitolea maelezo haya. Kwa hiyo, kusema tutamlipia naye amepata mimba, kwa utaratibu wa sasa narudia kusema, kupata mimba mtoto wa shule ni kosa la kufukuzwa shule.

Napenda nirudie nilivyowahi kusema, huu ni utaratibu tunauweka sisi wenyewe, kama itafikia wakati muafaka tunaona tubadilishe, itabidi tuweke utaratibu. Maana yake shulen ni mahali penye utaratibu. Haitegemewi uende shulen ukute wanafunzi wengine wamevaa mavazi ya wenye mimba au wengine wana watoto wananyonyesha. Kwa hiyo, inabidi tuweke utaratibu kwa sababu shulen ni mahali pa utaratibu. (*Makofi*)

### **Wilaya zilizo Nyuma Kielimu**

#### **MHE. GWASSA A. SEBABILI aliuliza:-**

Kwa kuwa, Wilaya ya Ngara ni mionganini mwa Wilaya nchini zilizo nyuma kielimu na kwa kuwa hivi sasa Wananchi wa Ngara wanachemka mno kujijengea shule za sekondari sita mwaka huu na tangu mwaka 2001 ziemfunguliwa sekondari nane za Ngara, Mugoma na Kibogora na kufanya idadi yake kuwa tano ikiongezewa na zile mbili za Kabanga na Muyenzi:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kusaidia Wilaya hiyo kwa kupandisha daraja sekondari za Kabanga na Muyenzi kuwa sekondari za juu, *Higher Secondary Schools?*

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, wakati sasa umefika wa kuzichambua Wilaya zote zilizo nyuma kielimu kama Wilaya ya Ngara na kuzipa kipaumbele kwa elimu ya sekondari?

(c) Kwa kuwa, Wilaya ya Ngara imekuwa ikifaulisha wanafunzi wengi tangu mwaka 1999 na 2003 ilikuwa ya kwanza kimko na kikanda na kuwa ya nne Kitaifa na wanafunzi wengi wenye alama za juu hadi 170/2000 walikosa nafasi na wako vijijini tu, je, Serikali ina mikakati ipi ya kuiunga mkono Wilaya hiyo ambayo kwa miaka mingi sasa imeshindwa kufuatilia mipango ya maendeleo ya Serikali kutokana na athari za wakimbizi za mara kwa mara?

#### **WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Gwassa Angus Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Wilaya ya Ngara, kwa kujenga shule za sekondari nane mwaka huu. Shule hizo zitasaidia sana katika kuongeza nafasi za sekondari Kidato cha Kwanza kwa wanafunzi wanaofaulu Mtihani wa Darasa la VII katika Wilaya hiyo ya Ngara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuongeza Shule za Sekondari za Juu (*A Level*) nchini kwa kusaidia kujenga shule mpya au kuzifanya baadhi ya shule za kawaida (*O-Level*) zilizopo ziwe sekondari za juu, kama nilivyoeleza katika Hotuba ya Bajeti. Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES 2004 - 2009), Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka za Mkoaa, itabaini na kupanga kikamilifu shule zitakazokuwa Sekondari za juu na muda wa kuanza kwa shule hizo. Endapo sekondari za Kabanga na Muyenzi zitabainishwa kuwa zinatafaa kuwa sekondari za juu, hapana shaka zitabadilishwa kuwa sekondari za juu. Lengo ni kuwa na shule za aina

hiyo, yaani za *A-Level* zenyе michepuo mbalimbali ya masomo katika maeneo mbalimbali ili kupunguza gharama za usafiri wa wanafunzi kwenda kuzifuata huko ziliko mbali.

(b) Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa MMES 2004 -2009 utafanywa uchambuzi wa kubaini kwa usahihi kabisa Wilaya zilizo nyuma kielimu, ili kuzihamasisha na kuziwezesha kwa ruzuku ya maendeleo katika kuongeza nafasi za elimu ya sekondari katika Wilaya hizo. Kigezo kitakachotumika katika kubaini Wilaya hizo ni idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuingia Kidato cha kwanza katika Wilaya hizo ikilinganishwa na kiwango cha Kitaifa cha mwaka husika ambacho kwa mwaka huu, yaani kwa wale walio darasa la saba mwaka huu ni asilimia 35 ya watahiniwa hao wa Darasa la VII.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika sehemu (b) ya jibu, Serikali imepitisha MMES 2004 - 2009 itaziwezesha Wilaya zilizo nyuma kielimu (*Under-served Areas*), ikiwa ni pamoja na Wilaya zenyе mahitaji maalum kama vile Wilaya ya Ngara na nyingine katika kupata nafasi zaidi za elimu ya sekondari, kwa kufanya shule zote zilizoko ziwe za mikondo minne na kuwapa ruzuku ya maendeleo ya kujenga madarasa na shule mpya na kuzipatia shule hizo walimu na ruzuku ya uendeshaji ya kutosha kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**MHE. GWASSA A. SEBABILITY:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri na ya kutia moyo na ninaamini kwamba, haya anayoyazungumza yatatekelezwa. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kigezo cha *ku-up grade secondary schools* za kawaida kuwa *high secondary schools* ni idadi ya watoto; na kwa kuwa Ngara watoto waliofanya mitihani mwaka 2003 walikuwa ni karibu asilimia 98 na ninajua mwaka huu watafikia asilimia 100:-

(a) Je, atakuwa tayari kutuhakikishia kwamba katika orodha ya wale watakaopewa kipaumbele cha kwanza Wilaya ya Ngara itakuwa ni mojawapo?

(b) Kwa kuwa Waswahili wanasema siri ya kazi ni kwenda pale kazi ilipo na Ngara inafanya kazi hii nzuri katika mazingira magumu, Mheshimiwa Waziri, atakuwa tayari kufika Ngara na kuungana na Wananchi wa Ngara katika kuhakikisha kwamba kazi wanayoifanya ni ya kweli na kwa hiyo anahitaji kuwapa msaada ambao ana uhakika nao?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kwamba kutokana na takwimu alizozitoa tutoe kipaumbele katika Wilaya ya Ngara, napenda nichukue nafasi hii kufafanua wazi kabisa kwamba, suala la kujenga shule za sekondari za *A-Level* litahusu Wilaya zote. Nichukue nafasi hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuwa na mawasiliano na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya ili kama kuna shule inapendekezwa kuwa ya ngazi ya Daraja A (*A-Level*), tafadhalii mapendekezo hayo yaletwe Kimko kwa sababu kama mnavyoona mpango huu wa MMES, umelenga kutoa elimu ya sekondari kwa usawa. Kwa hiyo, tungependa

mapendekezo haya yaoanishwe Kimkoa tupate Wilaya inavyoona, tupate Wilaya, Mkoa unavyoona halafu uchambuzi utafanywa na wataalam wa Wizara lakini itahusu kila Wilaya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba, kwa Waswahili wa kule Ngara siri ya kazi ni kwenda kuiona, basi namshukuru kwa kunikumbusha kwamba sijafika katika Wilaya ya Ngara. Napenda kukiri sijapata nafasi ya kutembelea Mkoa mzima wa Kagera, lakini imo katika mipango yangu kwamba mapema iwezekanavyo, nafasi itakapopatikana, nitapanga kufika katika Mkoa huo ikiwemo pia Wilaya ya Ngara.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibowi. Sasa matangazo ya vikao vya Kamati kwa leo, Kamati tatu zimepangiwa kufanya vikao kama ifuatavyo:-

Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, anawaomba Wajumbe wakutane kwenye kikao saa tano asubuhi hii katika chumba cha mikutano Na.227, ghorofa ya pili. Kamati ya pili ni Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Njelu Kasaka, anawaomba Wajumbe wake wakutane saa tano hiyo hiyo chumba cha Kamati Na.231, ghorofa ya pili. Kamati ya tatu ni Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anawatangazia Wajumbe wake kwamba, kutakuwa na kikao leo tarehe 2 Agosti, 2004 kuanzia saa tano asubuhi, chumba Na.219, ghorofa ya pili.

Tangazo lingine ni kwamba, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambayo inawasilisha hoja yake leo, ina Shirika linaitwa NYUMBU, ambapo kazi yake ni kutengeneza magari. Sasa Shirika hilo limechukua nafasi ya Wizara yao, ambayo inawasilisha makadirio yake leo, kuleta magari mawili waliyoyatengeneza wao ili Waheshimiwa Wabunge, waweze kuyaona na kuona jinsi walivyopiga hatua kiteknolojia, yaani wanaweza kutengeneza magari. Magari yapo hapo nje kwenye Viwanja vya Bunge. Kwa wakati wenu Waheshimiwa Wabunge, mnaweza kuyaona mkishatoka nje. (*Makofii*)

Mwisho wa matangazo, Katibu tunaendelea na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa likubali kupitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake kwa Mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Dr. John Samwel

Malecela na Wajumbe wa Kamati yake, kwa jinsi ambavyo wamepitia na kuyachambua makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuwasilisha Taarifa kwenye Bunge lako Tukufu. Wajumbe wa Kamati wamekuwa karibu nasi katika kutuasa, kutuelekeza na kutetea hoja za Wizara yetu pale ilipobidi; nawashukuru sana. Vilevile, ningelipenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick T. Sumaye, kwa Hotuba yake ya kina na ambayo imetoa dira ya utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Nawapongeza pia Mawaziri wenzangu, ambao Hotuba zao zimekwisha kujadiliwa na kupidishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi na Wapiga Kura wa Jimbo la Rarya, nami napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa rambirambi zangu kwa Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, familia, jamaa na marafiki wa aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Mheshimiwa Yetet Sentimule Mwalyego, aliyefariki tarehe 24 Juni, 2004. Napenda pia kutoa rambirambi zangu kwa Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, familia na marafiki wa aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, aliyefariki tarehe 22 Julai, 2004. Vifo vya ghafla vya Marehemu hao vimetusikitisha na kutuhuzunisha sote hasa ikizingatiwa kwamba, tulikuwa nao katika Bunge hili linaloendelea. Marehemu Mheshimiwa Yetet Sentimule Mwalyego na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, walikuwa Wabunge hodari, wachapakazi na wazalendo ambao Wananchi wa Mbeya Vijijini na Ulanga Mashariki, walikuwa wanawategemea sana kwa maendeleo yao. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azipumzishe roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi, Marehemu Omar Kigoda. Mwenyezi Mungu, awape moyo wa kustahimili na subira. Napenda kutoa pole pia kwa Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan na Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, kwa kufiwa na watoto wao wapendwa. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, azipumzishe roho za Marehemu wote mahali pema peponi. *Amin.*

Napenda vilevile kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wenzetu, waliokumbwa na mikasa mbalimbali nikianza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, aliyevamiwa na majambazi, majambazi ambayo yalipora mali na kumjeruhi kijana wao na dereva. Tunashukuru kuwa majambazi hayo yamekwisha naswa na yanashughulikiwa kulingana na sheria. Wengine ni Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, aliyejata ajali ya gari na kuumia na ambaye hivi sasa anaendelea na matibabu, Mheshimiwa Estherina Kilasi, aliyejata ajali ya gari, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, aliyevamiwa na majambazi na Mheshimiwa Rosemary Nyerere, aliyevamiwa na majambazi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Makamanda, Wapiganaji na Wafanyakazi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kumpa pole nydingi Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kuugua. Tunamwombea aweze kupona haraka na hivyo kuweza kuendelea vyema na jukumu lake la kuliongoza Taifa letu. Wakati huo huo, kwa masikitiko makubwa, nami naungana na Watanzania

wenzangu, kutoa Salamu zangu za pole kwa Rais wetu na mama Anna Mkapa, kwa kuunguliwa na makazi yao Ikulu Dar es Salaam tarehe 13 Aprili, 2004.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3 Januari, 2004, Taifa lilipata msiba wa kuondokewa na mmoja wa Mashujaa na Mwanamapinduzi wake, Marehemu Jenerali (Mstaafu) Abdallah Twalipo. Marehemu Jenerali Twalipo, alilitumikia Taifa kwa miaka 41 katika nyadhifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mkuu wa Mkoa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Marehemu Jenerali Twalipo, alikuwa mzalendo, mtiifu na mwaminifu kwa Amiri Jeshi Mkuu, mtetezi wa Muungano na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Atakumbukwa daima kwa ushujaa wake na hekima ya kivita alipoliongoza Jeshi letu la Ulinzi katika vita dhidi ya majeshi ya Nduli Iddi Amin na kuliletea Taifa letu ushindi na heshima kubwa. Alipewa jina la Jenerali Chakaza, kwa jinsi alivyoyachakaza majeshi ya uvamizi. Alizikwa kwa heshima zote za kijeshi na mazishi yake kuhudhuriwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Viongozi wengine mbalimbali. Tunamwomba Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, katika mwaka 2003/2004, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu, walipata nafasi ya kuchaguliwa kutuwakilisha katika Taasisi mbalimbali za Kimataifa. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Ranya, ningelipenda kuwapongeza sana wote waliohusika na chaguzi hizo na kwa moyo wa dhati kabisa, tunawapongeza Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr Amani W.A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchaguliwa kwao na Bunge lako Tukufu kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika. Tumefarijika tena sana kwa Mheshimiwa Getrude Ibengwe Mongella, kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Bunge hilo la kwanza la Afrika. Uchaguzi wake ni kielelezo tosha kuhusu jinsi Wabunge wa Afrika walivyo na imani naye na nchi yetu. Tusisahau kuwa Wilaya ya Ukerewe ina sifa ya pekee ya kutoa Maspika. (*Makofi/Kicheko*)

Vilevile nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuteuliwa kuiwikilisha Tanzania katika Baraza la Bunge la SADC. Nawapongeza Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mawaziri wa Elimu katika Bara la Afrika na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. Nampongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Kwa nafasi ya kipekee, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwake na Wananchi wa Jimbo la Bariadi Mashariki kuititia CCM kuwa Mbunge wao katika Uchaguzi Mdogo wa Ubunge uliofanyika tarehe 30 Mei 2004. Mheshimiwa Danhi Makanga, karibu tena nyumbani kwa baba mzazi, CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kufunga mjadala kuhusu makadirio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2003/2004, Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia, mlitoa ushauri kuhusu jinsi ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara

ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa moyo mkunjufu, naomba kutoa taarifa kuwa, kwa kiwango kilichowezekana, tumezingatia ushauri na maelekezo ya Waheshimiwa Wabunge, kulingana na uwezo wa Bajeti tuliyopewa. Taarifa ya utekelezaji imeandaliwa na Waheshimiwa Wabunge wamepewa nakala kama sehemu ya Hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuandaliwa rasmi kwa taarifa ya utekelezaji, naomba niitumie nafasi hii pia kuelezea kwa ujumla kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Jeshi letu la Ulinzi lilifanya kazi nzuri sana katika kudhibiti ipasavyo ulinzi wa mipaka ya nchi yetu. Hali ya Ulinzi wa Mipaka ya nchi yetu imeendelea kuwa shwari licha ya tatizo la wakimbizi na wahamiaji haramu kutoka nchi jirani zenyenye machafuko, hasa nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kuendelea kuingia na kujificha nchini mwetu. Baadhi yao wameendelea kushiriki katika vitendo viovu vya ujambazi wa kutumia silaha dhidi ya wananchi wetu katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Rukwa, Shinyanga na Mwanza. Hali hii imeendelea kuzorotesha hali ya usalama wa wananchi na mali zao. Baadhi ya wananchi wetu wamepoteza maisha, kujeruhiwa na kuporwa mali zao.

Mheshimiwa Spika, jukumu mojawapo la msingi la Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni kusaidia mamlaka za kiraia katika kulinda usalama wa Wananchi na mali zao. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya dola, Kamati za Ulinzi za Mikoa na Wilaya, ili kuhakikisha kuwa upo usalama wa Wananchi wetu na mali zao. Jeshi la Ulinzi limeimarisha doria za kudumu katika mipaka ya nchi yetu na hasa katika Mikoa ya Kigoma, Kagera, Rukwa na mwambao mzima wa Ziwa Tanganyika, ambako kumekuwapo na matukio ya mara kwa mara ya ujambazi na uharamia dhidi ya wavuvi na wafanyabiashara kutoka nchi jirani. Ili kudumisha usalama ndani ya Ziwa Tanganyika, pale ilipobidi Jeshi la Ulinzi limeshiriki katika kusindikiza meli za kibiashara kati ya Burundi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Doria za Jeshi la Ulinzi katika mpaka wetu wa Magharibi na Operesheni mbalimbali zinazoongozwa na Mamlaka za Mikoa inayohusika dhidi ya majambazi yanayotumia silaha za kijeshi zimewezesha kukamatwa kwa wahalifu ambaa baada ya kunyanga'nywa silaha zao walikabidhiwa kwa vyombo vinavyohusika. Baadhi ya mali za wananchi zilizoporwa ziliokolewa na kukabidhiwa kwa wenye mali hizo. Silaha za aina mbalimbali zikiwemo Bunduki *SMG/AK 47* idadi 17 na risasi 377 zilizokuwa zinatumwa na majambazi katika kuwaua, kuwajeruhi na kupora mali za wananchi wetu zilikamatwa. Majambazi waliokaidi kutii amri ya kujisalimisha toka kwa wanajeshi wetu walishughulikiwa kwa mujibu wa kanuni na taratibu za kijeshi. Napenda kutoa pongezi kwa Wakuu wa Mikoa ya Kagera, Jenerali Kiwelu (Mstaafu), Kigoma Kanali (Mstaafu) Mahawa na Rukwa Kepteni (Mstaafu) Mkuchika, kwa kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Ulinzi katika operesheni mbalimbali zilizofanyika kuwadhibiti wahalifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hali ya Ulinzi na Usalama katika mipaka mingine ya Tanzania ilikuwa shwari isipokuwa kwa upande wa Bahari ya Hindi ambako kuna tatizo la uvuvi wa kutumia baruti. Doria za Jeshi la Ulinzi katika eneo hilo zimeendelea kutoa msaada kwa Idara ya Maliasili na Polisi ili kudhibiti tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la Ulinzi na Usalama wa nchi, ni ukweli usiopingika kuwa, hali ya utulivu katika mipaka ya nchi yetu na nchi kwa ujumla, kwa kiasi kikubwa imechangiwa na Serikali ya nchi yetu inayosisitiza ujirani mwema na nchi tunazopakana nazo, pamoja na ulinzi imara unaotolewa na Jeshi letu la Ulinzi likishirikiana na vyombo vingine vya dola na Wananchi katika ujumla wao. Wote hawa napenda kuwashukuru sana, kwa ushirikiano wao na Jeshi letu la Ulinzi katika kulinda na kudumisha usalama wa mipaka ya nchi yetu, Wananchi wetu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliendelea kutekeleza awamu ya kwanza ya mpango kamambe wa miaka kumi na tano wa kuliimarisha na kuliboresha jeshi kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2000, Ibara ya 94(vii), yaani Tanzania kuendeleza Sera ya Chama cha Mapinduzi ya kuwa na Jeshi dogo la Ulinzi, lenye wataalamu waliofuzu vizuri, na lenye zana na vifaa vya kisasa. Utekelezaji wa mpango huo ulioanza mwaka 2002/2003, umelenga katika kulipatia Jeshi zana bora kwa ajili ya kuimarisha ulinzi, mafunzo na kujenga mazingira mazuri ya kazi. Mpango huo umeendelea kuleta unafuu katika upatikanaji wa huduma za msingi kama vile vyombo vya usafiri na usafirishaji, ukamilishaji wa viprovo vya nyumba na ukarabati wa majengo na makazi, upatikanaji wa huduma za mafunzo, lishe, sare na huduma za matibabu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ufinyu wa Bajeti wa miaka mingi ambaeo matokeo yake yamekuwa ni kuahirishwa kwa utatuzi wa matatizo mwaka hadi mwaka, napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kutetea na hivyo kuwezesha kuongezeka mwaka hadi mwaka kwa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi. (*Makofî*)

Katika utekelezaji wa mpango wa kutatua matatizo ya Jeshi, katika mwaka 2003/2004, mambo muhimu yafuatayo yalipewa kipaumbele:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, huduma za chakula na mabwalo vikosini zinazozingatia utaratibu wa kutumia kantini zimeendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa sare kwa wanajeshi na kwa vijana wa JKT imekuwa ni ya kuridhisha. Sare muhimu zilitolewa kwa ukamilifu kwa vikosi vyote na kwa wakati. Pale ilipowezekana sare hizi zilinunuliwa kutoka humu humu nchini na uagizaji kutoka nje ulifanyika kuziba pengo. Tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili mahitaji yetu yatokane na viwanda vyetu nchini na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo ya ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, huduma za tiba Jeshini zinaendelea kuboreshwa kufuatia kuimarishwa kwa Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo. Ufungaji wa vifaa vya kisasa vya tiba na uchunguzi wa maradhi katika Hospitali za kanda za Mbeya na Mwanza ambazo

ukarabati wake umekamilika, unaendelea. Vilevile ukarabati/ujenzi wa Hospitali ya Bububu - Zanzibar unaendelea. Mashine ya *X-ray* imeshapelekwa Hospitali ya Bububu na itaanza kutoa huduma baada ya kufungwa. Kwa ujumla dawa za kutosha zinapatikana katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Jeshi. Pale ambapo dawa hazipatikani katika vituo hivyo wagonjwa wamekuwa wakinunuliwa dawa kutoka nje ya Hospitali hizo. Wataalam wa kada mbali mbali nao wamekuwa wakipatiwa mafunzo kulingana na taaluma zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na Sera safi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuhusu ushirikiano wa Kimataifa na nchi mbalimbali, Serikali ya Shirikisho la Ujerumanî, kuptitia chombo chake cha Jeshi (*German Armed Forces Technical Advisory Group - GAFTAG*), imeonyesha nia ya kutoa msaada kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika kujenga upya hospitali saba za jeshi ambazo kwa sasa ziko katika hali mbaya. Hospitali zinazohusika na mpango huu ni Hospitali za Kanda za Kijeshi ambazo ni Hospitali ya Mirambo - Tabora, Munduli, Bububu na Songea. Hospitali zingine ni za Navy - Dar es Salaam, Mzinga, na Nyumbu. Kutegemeana na makubaliano yanayotarajiwa kukamilishwa, ujenzi wa Hospitali hizo utaanza mwezi Machi, 2005 na utakuwa kwa awamu. Kituo cha Afya, Kambi ya Wawi - Pemba kitafanyiwa ukarabati kwa kutumia fedha za Bajeti. Kwa niaba ya Makamanda, wapiganaji na Serikali ya Tanzania napenda kuishukuru Serikali ya Shirikisho la Ujerumanî kwa msaada wake wa kuboresha na kuimarisha huduma za Afya kwa wanajeshi na wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi ni sehemu mojawapo muhimu ya mpango wa kuimarisha Jeshi. Katika mwaka 2003/2004, Wanajeshi wetu waliwezesewa kufanya mafunzo na mazoezi mbalimbali kulingana na fani zao ndani na nje ya nchi. Wanajeshi pia wamewezeleshwa kufanya mazoezi ya medani vikosini katika ngazi mbali mbali kwa viwango vilivyotakiwa. Jeshi letu lilishiriki katika mazoezi yaliyohusisha majeshi ya nchi nyingine nje ya Tanzania. Mazoezi hayo ni pamoja na zoezi la Askari wa miavuli (*Ex-PARAZAM*) lililofanyika nchini Zambia.

Wanajeshi wetu walitia fora na kupata sifa nyingi kutokana na uhodari na umahiri wao. Napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru sana Serikali za China, Afrika Kusini, Australia, Canada, Finland, Ghana, India, Mali, Marekani, Misri, Netherlands, Norway, Sweden, Switzerland, Ubelgiji, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Ujerumanî, Zambia na Zimbabwe kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, huduma ya nyumba za Askari kuishi makambini ni kati ya mambo yanayopewa kipaumbele kwa madhumuni ya kutanzua uhaba wa nyumba za kuishi wapiganaji wetu makambini. Hii ni pamoja na kuwarejesha Wanajeshi wanaoishi uraiani kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya kijeshi. Serikali imeanza kukamilisha ujenzi wa viporo vya nyumba katika Makambi ya Ihumwa - Dodoma, SOFA - Arusha na Makoko - Musoma. Katika mwaka 2003/2004, viporo vya ujenzi wa nyumba 38 vilikamilishwa kujengwa katika kambi ya SOFA - Arusha kwa gharama ya shilingi 674.5 milioni. Hii inafanya idadi ya nyumba zilizokamilishwa kujengwa SOFA Arusha kufikia 90. Zoezi la ukamilishaji wa viporo vya nyumba 84 katika Kambi ya Makoko-Musoma ikiwa ni pamoja na kuweka mtandao wa maji lilianza mwezi Machi 2004. Tayari

nyumba 20 zimekwisha kukamilishwa na inakadiriwa kuwa ujenzi wote utagharimu shilingi 995.5 milioni. Ukamilishaji wa viporo hivi unafanywa na JKT na inatarajiwa kuwa kazi hii itakamilika ifikapo Septemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, kulingana na mpango kamambe wa kukamilisha ujenzi wa vporo vya nyumba za kuishi wanajeshi makamabini ulioanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2001/2002, ujenzi wa nyumba 264 zitakuwa zimekamilika ifikapo Septemba, 2004 kwa gharama ya shilingi 2.47 bilioni. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Serikali imetenga shilingi 4.00 bilioni kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vporo vya nyumba katika makambi ya Makambako - Iringa, Nguvumali na Kange Tanga, Mwanza, Kibaha - Pwani, Makoko - Musoma, Mukalama - Dodoma na kufanya ukarabati nyumba za kuishi katika kambi ya Wawi - Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi kwa kutumia Brigedi za Ujenzi za JWTZ na JKT zilizoko katika kanda, imeendelea kukarabati nyumba na majengo kwa kutumia fedha za bajeti zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (*Other Charges*). Hii ni pamoja na Majengo 60 ya kuishi familia nane kila moja katika kambi ya Lugalo, jengo la maafisa kapera Kituo cha Usafirishaji wa Anga (*Air Wing*), mabweni na majengo mbalimbali katika kambi ya Jenerali Twalipo, kantini ya Makao Makuu ya Jeshi, Mess ya Maafisa Upanga, majengo na ofisi mbalimbali Makao Makuu ya Wizara, Makao Makuu ya Jeshi na Makao Makuu ya JKT, yote ya Dar es Salaam. Majengo haya yamefanyiwa ukarabati mkubwa na sasa yanapendeza. Wakati huo huo, ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa maji, visima vya maji vimechimbwa Makao Makuu ya Wizara, Makao Makuu ya Jeshi na pampu mpya ya maji ilinunuliwa kwa ajili ya kulitanzua tatizo la ukosefu wa maji katika kambi ya Chabruma Songea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa kudumu wa shughuli za ujenzi katika makambi ya Jeshi, Serikali ilikwishatoa maelekezo kuwa jukumu hili litekelezwe kwa kutumia Brigedi za Ujenzi za Jeshi zilizoko katika kanda. Hatua hii imechukuliwa kwa lengo la kuepuka makosa yaliyofanyika huko nyuma ya kutumia Wakandarasi na kuingia gharama kubwa za ujenzi wa nyumba chache. Jeshi la Ulinzi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa yana uwezo, utaalamu na ujuzi mkubwa wa kujenga na kukarabati nyumba zetu kwa gharama nafuu na kwa muda mfupi. Wizara imeandaa mkakati wa Ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Wanajeshi kwa kujitegemea utakaoanza mwaka 2004/2005. Mkakati huo pia utahusisha uimarishaji wa vikosi vyetu vya ujenzi, ikiwa ni pamoja na kuvipatia vitendea kazi vya kisasa na vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Jeshi ni pamoja na Jeshi kuendesha shughuli zake katika maeneo yanayo julikana rasmi. Katika mwaka 2003/2004 upimaji wa maeneo ya Jeshi umeendelea. Maeneo hayo ni pamoja na yale ya makazi, makambi, maeneo ya mazoezi na kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uchunguzi uliofanywa kuhusu maeneo ya Jeshi yenye migogoro umebaini kuwa maeneo hayo ni ya Jeshi kwa kuwa yalikabidhiwa rasmi kwa Jeshi na Serikali. Ukweli ni kuwa maeneo

hayo kuwa mapori au vichaka ndio “ujeshi wenyewe”. Kuwepo kwa majengo ni sehemu tu ya utekelezaji wa shughuli za Jeshi. Napenda kusisitiza tena kuwa siyo vema na ni jambo la hatari kwa Wananchi kuvamia na kuishi karibu au ndani ya maeneo ya Jeshi. Nawaomba sana wananchi kutambua jambo hili na kujenga utamaduni wa kuyaheshimu maeneo ya Jeshi. Jeshi la Ulinzi la Wananchi ni Jeshi letu sote, liko kwa ajili ya kuwalinda wananchi na mali zao na pia kutoa msaada wa hali na mali kwa wananchi wakati wa maafa. Jeshi linahitaji msaada wa wananchi na wananchi wanahitaji msaada wa wanajeshi wao. Ni wajibu wetu sote kuepusha migogoro baina ya Wananchi na wapiganaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hitajio la upimaji wa maeneo, maeneo ya Jeshi yaliyopo Kimbiji, Changanyikeni, Mbagala, Mgulani, Kigamboni, Kipunguni na Kunduchi katika mkoa wa Dar es Salaam; Pangawe-Morogoro, JKT Ruvu na Kibaha Pwani na Mwakidila Tanga yalipimwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005, maeneo yaliyopangwa kupimwa ni pamoja na Makao Makuu ya Wizara (yanayojumuisha Makao Makuu ya Jeshi), eneo la Mafunzo katika Bonde la Lulunde na Zanka Mkoani Dodoma na Kambi ya Sokoine katika Mkoa wa Arusha. Makambi mengine yatakayohusika ni yale yaliyoko katika Mkoa wa Mtwara, JKT Itaka Mbeya, Eneo la Mafunzo-Msata, Eneo la Mafunzo Wami/Mbiki-Dakawa, Kituo cha Kilwa-Lindi, Kaboya, Kyaka na Biharamlo katika Mkoa wa Kagera.

Kwa niaba ya Makamanda, Maafisa Wapiganaji wote, napenda kuwapongeza, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mkuu wa Wilaya ya Muleba na Mbunge wa Muleba Kusini Mheshimiwa Masilingi kwa kuwapatia JKT eneo la kujenga kambi mpya Wilayani Muleba. Pia nampongeza Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa kuwa karibu na Wanajeshi katika Kambi ya Kaboya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo ya Jeshi kuvamiwa na hivyo wavamizi kutostahili fidia yapo maeneo machache ambayo ili kumaliza migogoro iliyopo, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekubali fidia itolewe kwa baadhi ya wananchi kwa ajili ya mali zao zilizoko/zilizokuwa kwenye maeneo hayo kama vile maeneo ya Tondoroni-Kibaha, Welezo-Zanzibar na Oldonyo Sambu-Arusha.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za kulipatia Jeshi zana za kutosha na zinazostahili kwa ajili ya shughuli za Ulinzi wa nchi yetu zimeendelea. Kwa kuwa mahitaji yanayohusika ni mengi, mahitaji hayo yanashughulikiwa hatua kwa hatua. Kipaumbele kimetolewa katika kulijengea Jeshi uwezo wa usafiri na usafirishaji ili liweze kutekeleza majukumu muhimu kama vile doria za mipakani, baharini na kwenye maziwa, uwezo wa kukabiliana na majanga au maafa hapa nchini na pia uwezo wa kudhibiti vitendo vyta kigaidi na hujuma mbali mbali. Katika mwaka 2004/2005, Wizara inatarajia kupata boti kadhaa za Doria kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa Baharini na kwenye Maziwa. Wizara pia inatarajia kukamilisha taratibu za kupata helikopta mbili mpya kwa ajili ya shughuli za uokoaji.

Ipo mipango pia ya kupata magari ili kupunguza tatizo la usafiri vikosini ikiwa ni pamoja na magari ya kubeba wagonjwa. Kutokana na Tanzania kuwa mwanachama

makini wa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, Serikali itaendelea kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia uwezo wa kivifaa ili liweze kushiriki kwenye majukumu ya kulinda amani sehemu mbalimbali duiniani pindi nchi yetu itakapoombwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudini za kulinunulia Jeshi zana mpya, zana zilizopo zinafanyiwa ukarabati ili kuziweka katika uwezo wake wa awali wa utendaji. Zana nyingi za zamani zimeweza kufanyiwa ukarabati kwa kuweka vifaa vya kisasa na kuweza kutumika tena kwa kiwango cha kisasa. Matengenezo na ukarabati wa zana pia ni pamoja na ukarabati na uimarishaji wa miundombinu ya karakana mbalimbali na uimarishaji wa maghala na sehemu za kutunzia zana kwa madhumuni ya kuzikinga na mvua, juu na mavumbi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuimarisha Ulinzi wa Umma (Mgambo) kwa kuboresha mafunzo na uundaji wa kombania za ulinzi umeendelea kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Mafunzo ya Mgambo yameendelea kutolewa katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Dar es Salaam, Dodoma, Lindi, Pwani, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Tanga, Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga. Mafunzo hayo yameendeshwa katika ngazi ya awali na kujikumbushia chini ya wakufunzi wa Jeshi la Ulinzi. Mafunzo yameimarishwa zaidi kwa kupeleka rejea za masomo yaliyoboreshwa kwa kila Wilaya ili kuweka viwango vya masomo kwa nchi nzima. Zoezi la kutoa vitambulisho vya wana mgambo linaendelea katika Mkoa wa Dar es Salaam na litaendelea katika mikoa mingine katika kipindi cha mwaka 2004/2005. Hii ni pamoja na utoaji wa vyeti kwa wahitimu ambao utafanyika kikanda. Mafunzo ya uongozi wa mgambo yaliyositishwa mwaka 1992 sasa yataanzishwa tena kikanda.

Mheshimiwa Spika, Tanzania siku zote inasisitiza ushirikiano na kuishi kwa amani na nchi nyingine duniani na hasa majirani zake. Kwa misingi hii Tanzania imekuwa mstari wa mbele kudumisha mshikamano katika nyanja ya ushirikiano wa kijeshi na Serikali za nchi mbalimbali duniani. Ushirikiano umeimarishwa baina ya nchi yetu na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Australia, Canada, China, Finland, Ghana, India, Indonesia, Italia, Ireland, Mali, Marekani, Misri, Netherlands, Norway, Sweden, Switzerland, Ubelgiji, Ufaransa, Uingereza, UAE na Ujeruman. Nchi hizo zimechangia kwa kiasi kikubwa jitihada za Serikali yetu kuimarisha ulinzi wa nchi yetu. Nazishukuru Serikali za nchi hizo kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, katika azma ya kuimarisha ushirikiano wetu Kijeshi na nchi mbalimbali duniani, katika mwaka 2003/2004, zilifanyika ziara za Viongozi wa Wizara na Jeshi katika nchi za nje kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa Kijeshi kama ifuatavyo:-

- Mwezi Septemba, 2003 Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alifanya ziara nchini China kwa mwaliko wa Waziri wa Ulinzi wa China Mheshimiwa Cao Gangchuan. Wakati wa ziara hiyo yalifikiwa makubaliano ya kimkataba ambapo Serikali ya China imeipatia Serikali ya Tanzania misaada mbalimbali ya kijeshi. Kwa niaba ya Makamanda na Wapiganaji wote napenda kuwashukuru marafiki zetu wa jadi ndugu zetu

wa China kwa kuendelea kusaidia Jeshi letu kwa hali na mali. Katika mwezi Januari, 2004 Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alifanya ziara Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*) kufuatia mwaliko wa Waziri wa Ulinzi wa Umoja huo Mtukufu Sheikh Mohamed Bin Rashid Al-Maktoum. Kufuatia ziara hiyo Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia Wizara yake ya Ulinzi imeipatia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa vifaa mbalimbali vikiwemo magari, mahema na vifaa vingine kwa ajili ya kuimarisha vikosi vya ujenzi. Naomba niitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Ulinzi wa Umoja wa Falme za Kiarabu kwa msaada waliotupatia.

- Mwezi Novemba, 2003 Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Waitara alifanya ziara nchini Kenya kwa mwaliko wa Mkuu wa Majeshi wa Kenya Jenerali Kibwana. Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Luteni Jenerali Gahhu, alifanya ziara nchini China.
- Wakati huo huo, mwezi Mei, 2004, Naibu Mkuu wa Jeshi la Ukombozi la China (*PLA*), Luteni Jenerali Zhang Li, alifanya ziara nchini Tanzania.
- Mwezi Mei 2004 Naibu Waziri wa Ulinzi wa Ujerumani alifanya ziara nchini Tanzania kukagua maendeleo ya ukarabati wa Hospitali za Jeshi unaosaidiwa na Serikali ya Ujerumani. Vilevile Brigedia Jenerali Mubaraka Mal Allah Suwaid Al Amri, Msaidizi wa mwana wa Mfalme wa Umoja wa Falme za Kiarabu (*UAE*), alifanya ziara nchini Tanzania mwezi Mei, 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, hatukuwa nyuma katika kuendeleza ushirikiano wa Kijeshi Kikanda. Tulishiriki kikamilifu katika shughuli zote muhimu zilizohusiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika azma ya kuimarisha ushirikiano wa kijeshi baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, tarehe 29 hadi tarehe 30 Aprili, 2004, Mawaziri wa Ulinzi wa Jumuiya hii walifanya kikao cha Sekta ya Ulinzi ya Jumuiya, mjini Zanzibar. Kikao hicho kilifunguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Amani Abeid Karume. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho Mawaziri wa Ulinzi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa pamoja walikubaliana juu ya mambo makuu matatu yafuatayo:-

(i) Kubadilishana ujuzi na uzoefu na kufanya mazoezi ya pamoja ya kijeshi kama ifuatavyo:-

- Zoezi la ongoza njia: Kwa ajili ya majukumu ya kulinda Amani, litakalofanyika nchini Tanzania Mwezi Februari, 2005.
- Zoezi la *Trend Maker*: Kwa ajili ya kudhibiti vitendo vya kigaidi litakalofanyika nchini Kenya Mwezi Septemba, 2005.

-       Zoezi la *Hot Spring*: Kwa ajili ya majukumu ya kukabiliana na majanga litakalofanyika nchini Uganda Mwezi Februari, 2006.

(ii)   Kuundwa kwa chombo cha pamoja cha upashanaji wa habari kuhusu majanga na migogoro.

(iii)   Kupeana tahadhari kuhusu ugaidi.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kiulinzi na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*), umeendelea kuimarika. Kikao cha nne cha Kamati ya Mawaziri wa Ulinzi wa chombo cha *SADC* cha Siasa, Ulinzi na Usalama kilifanyika Maputo Msumbiji tarehe 7 Agosti, 2003 na kufunguliwa na Mheshimiwa Joachim Chissano, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji. Kamati ya Mawaziri katika kikao chake hicho ilipitisha mionganoni mwa mambo mengine, Maazimio na mapendeleko kuhusu hali ya kisiasa katika nchi za *SADC*, hali ya Ridhaa ya Itifaki za Ulinzi na Usalama katika nchi za *SADC*, Sera ya pamoja ya Ulinzi na Usalama Barani Afrika na ufadhili wa Nje katika maeneo maalum kwenye chombo cha *SADC*.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa wa “Operesheni miaka 40 ya JKT”, walimaliza mafunzo ya ukakamavu katika Makambi ya Makutupora, Oljoro na Ruvu. Baada ya mafunzo hayo vijana 1,508 walipelekwa katika Makambi ya Mgulani, Ruvu, Makutupora, Maramba na Mlale, kwa ajili ya mafunzo ya ufundi stadi. Vilevile, vijana 977 walipelekwa katika makambi ya Oljoro, Mafinga, Itende na Mbweni kwa ajili ya mafunzo ya kilimo na mifugo, na vijana 98 wenyewe ujuzi walajiriwa na JKT kufanya kazi katika makambi ya JKT kulingana na ujuzi wa kila mmoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kuwa kati ya vijana 2,491 wa “Operesheni Mkapa” waliomaliza mafunzo Oktoba, 2003, vijana 1,772 walipata ajira katika taasisi mbalimbali hapa nchini. Vijana 1,554 waliandikishwa JWTZ, vijana 100 walajiriwa *TANAPA*, vijana 50 walajiriwa na Usalama wa Taifa na vijana 68 walajiriwa na Idara ya Magereza. Vijana 561 waliojiunga na mafunzo ya ufundi stadi katika makambi ya Mgulani (vijana 344), Maramba (vijana 143) na Ruvu (vijana 74) walimaliza mafunzo yao Desemba, 2003 isipokuwa vijana wa Kambi ya Maramba ambao walibaki hadi Juni, 2004 walipomaliza mafunzo yao. Vijana 29 walipatiwa mafunzo ya kilimo na mifugo katika Kambi ya Oljoro.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kusisitiza kuwa madhumuni ya kutoa mafunzo ya JKT ni kuwaandaa vijana wa Tanzania kielimu, kimaadili na kinidhamu ili kuwa raia wema, wanaopenda kuitumikia nchi yao kwa kushirikiana na Wananchi wengine na pia kuwa na silika ya kupenda kazi za mikono na kujitegemea. Mafunzo ya ufundi wa aina mbalimbali kama vile, ujenzi, kilimo na ufugaji bora, yote yana lengo la kuwawezesha kujajiri wenywewe.

Hakuna utaratibu wa kuwapatia ajira vijana wote wanaomaliza mafunzo ya JKT katika Jeshi la Kujenga Taifa. Suala la kupata ajira katika Taasisi za Umma hapa nchini

baada ya kumaliza mafunzo ya JKT linategemea mipango ya Taasisi zenyewe. Hata hivyo, Taasisi nyingi za Serikali na zisizo za kiserikali zimeonyesha nia ya kuwaajiri vijana waliomaliza mafunzo ya JKT kutokana na nidhamu, ukakamavu, uaminifu na moyo wao wa kupenda kazi.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka JKT inatoa utaratibu unaotakiwa ufuatwe katika kuwateua vijana wa kujiunga na mafunzo ya JKT. Uteuzi huo hufanywa na Mamlaka za Wilaya na Mikoa na baada ya uteuzi huo, Makao Makuu ya JKT hufanya zoezi jingine la kuwachambua wote waliopendekezwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na nidhamu ya hali ya juu na uwezo wa kuhimili mafunzo JKT kiafya. Lengo kuu ni kuwachukua vijana wenye nidhamu isiyoyumba.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wake wa kuboresha mazingira ya makambi ya JKT. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 makambi ya Mafinga, Oljoro na Bulombora yalifanyiwa ukarabati mkubwa na hivyo kuyaweka katika hali nzuri. Mpango wa kupeleka umeme katika kambi ya Oljoro unaendelea kukamilika kwa kugharamiwa na TANESCO Mkoa wa Arusha. Umeme unatarajiwa kufikishwa kambini Oljoro mwaka huu wa 2004. Tumefanikiwa pia kufanya ukarabati, ujenzi wa karakana na madarasa mapya pamoja na ununuzi wa vifaa vyta kufundishia katika makambi ya Maramba, Mgulani, Mlale, Bulombora, Oljoro, Mafinga, Itende na Ruvu. Katika mwaka 2004/2005, JKT inatarajia kuchukua vijana 2,700 kwa ajili ya mafunzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Mtandao wetu wa Mawasiliano ya Kipekee (*ITN*) una uwezo mkubwa kuzidi mahitaji ya Jeshi na kwamba awamu ya tatu ya mradi wa *ITN* unalenga kutekeleza Sera ya Taifa ya teknolojia ya mawasiliano kwa kujenga muundombinu wa Serikali - Elektroni (*E-Government*), pamoja na kuhudumia watumiaji wengine. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa utekelezaji wa mradi huo umeanza na unaendelea vizuri. Timu ya wataalamu waliobobea kwenye fani ya mawasiliano imeundwa ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mradi huo ambao utatumika pia kwenye uanzishaji wa mfumo wa *E-Government* unaendelea vizuri na unakuwa na ufanisi unaotakiwa. Matokeo ya mradi ni kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa imepata mtandao wa kisasa wa mawasiliano yenye uhakika ambao utakuwa umeziunganisha Wizara zote hadi ngazi ya Makao Makuu ya Mikoa, Wilaya, Hospitali za Rufaa, Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotaarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara inafanya kila jitahada kuhakikisha kuwa utafiti wa magari ya Nyumbu unaimarishwa ili uzalishaji endelevu uweze kufanyika hapa nchini. Wizara pia ilikuwa inafanya majadiliano na makampuni mbalimbali ya nje kwa lengo la kuingia ubia na Shirika la Nyumbu na hivyo kuweza kuzalisha magari haya kibiashara kwa kutumia teknolojia ya Makampuni yenye sifa. Kwa sasa yako Makampuni mawili makubwa ya Kimataifa ambayo tumeanza majadiliano nayo. Haya ni kutoka China na India. Wakati huo huo, kwa kutambua umuhimu na historia ya Shirika la Nyumbu kwa Taifa, mwaka 2003/2004, Wizara ilitoa shilingi 350 milioni kama fedha za maendeleo kwa Shirika hilo ambazo zimeliwezesha kutengeneza magari saba hapa hapa nchini, kwa kuwatumia wataalamu

wetu. Mwaka 2004/2005, Shirika la Nyumbu limetengewa shilingi 600 milioni kwa ajili ya kutengeneza magari 14. Magari haya yote yatatumika Jeshini kama sehemu ya uendelezaji wa utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Shirika la Mzinga mwaka 2003/2004, Wizara ya Ulinzi imekamilisha mpango wa ununuzi wa Mitambo ya kisasa ya kutengeneza risasi. Usimikaji wa Mitambo hiyo utaanza mwaka huu wa 2004 na kutaliwezesha Mzinga kutengeneza risasi za aina mbalimbali kwa matumizi ya kiraia. Shirika la Mzinga pia limeendelea kutengeneza mashine ndogo ndogo na vipuri kwa ajili ya soko la ndani ya nchi. Shirika limeingia mkataba na Shirika la Reli Tanzania kwa ajili ya kutengeneza *brake blocks* 2,000 za treni kwa mwezi kwa kutumia *foundry* ya kiwanda. Shirika pia kwa mujibu wa Sheria limeendelea kuagiza kutoka nje silaha, risasi na milipuko ya aina mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya kiraia.

Mheshimiwa Spika, Shirika la SUMA JKT katika kipindi cha mwaka 2003/2004, limeweza kujizatiti kwa kutumia mbinu za kibashara za kufufua na kuimarisha uzalishaji mali. Mbinu hizo ni pamoja na kupata vibali vya kufanya biashara, kutathmini mali za Shirika, upimaji wa maeneo ya JKT na kutayarisha michanganuo ya miradi mbalimbali kwa lengo la kupata miliki na hatimaye kuingia ubia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, SUMA JKT ilijiwekea malengo ya kuzalisha bidhaa na kufanya kazi zenyet thamani ya shilingi 5.09 bilioni kwa kutumia shilingi 4.46 bilioni na hivyo kutegemea kupata faida ya shilingi 633 milioni kutokana na miradi yake ya kilimo, ufugaji, viwanda, biashara na ujenzi. Katika kipindi cha mwezi Julai 2003 hadi mwezi Machi, 2004, SUMA JKT ilizalisha na kuuza bidhaa na kufanya kazi mbalimbali zenyet thamani ya shilingi 4.81 bilioni kwa kutumia shilingi 3.77 bilioni na hivyo kupata faida ya shilingi 1.04 bilioni.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuifanya JKT iwe ni Taasisi ya uzalishaji mali inayojitegemea yenye na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa uendeshaji. Kutokana na SUMA JKT kupata faida, Shirika hilo limeweza kutumia shilingi 750.2 milioni zitokanazo na faida kwa ajili ya ununuzi wa magari, vitendea kazi, kushona sare za vijana, kukarabati makambi, kupima maeneo ya JKT na huduma nyingine kutokana na fedha zake nje ya fedha zinazotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, SUMA JKT ilikamilisha ujenzi wa nyumba 153 za watumishi wa Serikali eneo la Mbweni Dar es Salaam zenyet thamani ya shilingi 3.4 bilioni. Ujenzi huo ulifanyika ndani ya kipindi cha miezi mitatu na hivyo kutokana na kazi nzuri ya kujivunia iliyo fanywa, Shirika limepewa kazi nyingine ya kujenga nyumba 250 za Maafisa Waandamizi wa Serikali kwa thamani ya shilingi 10.7 bilioni hapa Dodoma. Ujenzi wa nyumba hizo utakamilika kwa muda uliowekwa. Jiwe la msingi la ujenzi huo uliowekwa na Amiri Jeshi Mkuu, tarehe 1 Agosti, 2004. Nieleze pia kuwa SUMA JKT imepata usajili wa Ukandarasi Daraja la Kwanza kutoka Daraja la Tatu. Kwa niaba ya Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa JKT, Makamanda, Vijana wa JKT na wapiganaji wote napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa moyo wake wa kimapinduzi na uzalendo kwa JKT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 katika kikao cha Bunge lako Tukufu la Bajeti nilielezea kuhusu kiwanda cha kutengeneza madawa ya binadamu cha *TANZANSINO* kinachoendeshwa kwa ubia kati ya SUMA JKT na kampuni ya *Shanxi Provincial Technical Renovation and Equipments Corporation* ya China. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kiwanda hicho kimeendelea na kutengeneza madawa kwa viwango vya kimataifa. Aidha, licha ya madawa yanayotengenezwa sasa, kiwanda kinakamilisha taratibu za mwisho za upatikanaji wa kibali (leseni) kwa ajili ya kutengeneza dawa iitwayo “*Artecom*” ambayo inatibu ugonjwa wa Malaria kwa haraka. Hatua hizo zimewashirikisha kwa pamoja Wizara ya Afya, wataalamu wa Wizara ya Ulinzi na JKT, Tume ya Kudhibiti Madawa na Chakula (*Tanzania Food and Drug Authority*) pamoja na *NIMR* na Uongozi wa *TANZANSINO*. Hivi sasa dawa hiyo ipo katika hatua ya kufanyiwa utafiti hapa nchini. Mara baada ya utafiti huo kukamilika utengenezaji rasmi wa dawa hiyo utaanza na hatimaye wananchi wa Tanzania wataweza kupata dawa inayotibu ugonjwa wa Malaria kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu kuanza kwa uzalishaji wa dhahabu katika Mgodi wa Buhemba unaomilikiwa na *MEREMETA LTD*. Mgodi umejengwa katika eneo lililokuwa kambi ya Jeshi ambapo shughuli za uchimbaji na uzalishaji zinasimamiwa na Idara ya Madini. Tangu ulipoanza uzalishaji mwezi Januari mwaka jana hadi Juni, 2004, Mgodi umezalisha jumla ya kilo 4,400 za dhahabu zenyenye thamani ya Dola za Marekani 46,270,300. Gharama za uzalishaji na uendeshaji zilikuwa Dola za Marekani 35,702,000. Mgodi umelipa Serikalini mrabaha, yaani royalty, jumla ya Dola za Marekani 1,340,000 na umetumia jumla ya Dola za Marekani 156,700 katika miradi ya jamii. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Polisi na Shule ya Sekondari ya Butiama, uezekaji wa shule za msingi mbili za Buhemba na Biatika; uboreshaji wa visima vya asili kwenye vijiji vinne kati ya vijiji sita vinavyouzunguka mgodi, viwili bado. Aidha, Mgodi umeweuka pampu za maji sita, moja ikiwa ni ya umeme.

Mheshimiwa Spika, faida inayotokana na mgodi wa Buhemba itaendelea kutumika katika kuimarisha mgodi huo na huduma mbalimbali za kijamii. Wakati huo huo, maandalizi yanaendelea ili *MEREMETA* iweze kuanza tena kuwasaidia wachimbaji wadogo na kununua dhahabu yao Wilayani Geita.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya Ugonjwa wa Ukimwi vimeendelea kupiganwa kwa juhudzi zote katika Wizara ya Ulinzi na Taasisi zake. Kampeni kuhusu kinga dhidi ya maambukizi kwa Wanajeshi katika ngazi zote imeendelea kwa kushirikiana na *TACAIDS* pamoja na Wizara ya Afya. Utekelezaji wa mpango wa kuwapatia madawa yanayorefusha maisha na madawa yanayotibu magonjwa tegemezi walioathirika umeanza kwa kutoa madawa hayo kwa wanajeshi na familia zao. Matokeo yake ni kuwa waathirika wengi wameendelea na kazi zao na hivyo kuendelea kutoa mchango wao katika Ulinzi na Taifa letu. Mpango wa kupata madawa hayo kwa njia ya misaada unaendelea. Wizara kuitia Wizara ya Afya na *TACAIDS* imeahidiwa madawa kutoka kwa mashirika ya kimataifa, kama vile *Global Fund, Clinton Foundation, Pharmo Access* na *USAID*. Baadhi ya mashirika hayo yameanza kuleta madawa.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa huduma katika maduka ya bei nafuu Jeshini umeendelea. Tathmini iliyofanywa na Kamati iliyoteuliwa kuhakiki ufanisi wa maduka hayo ilibaini kuwa baadhi ya maduka yalikuwa hayafuli kwa ukamilifu utaratibu wa utoaji wa huduma kulingana na makubaliano yaliyofikiwa katika mikataba ya uendeshaji wa maduka hayo. Madhumuni ya uanzishaji wa maduka hayo ni kutoa huduma kwa wanajeshi kwa bei nafuu, kuuza bidhaa zenyne manufaa kwa lengo la kuendeleza na kuboresha maisha ya wanajeshi. Bidhaa hizo ni pamoja na vifaa vya ujenzi na vifaa vya matumizi ya nyumbani.

Hivyo, wote wenye kasoro wameagizwa na Mkuu wa Majeshi kurekebisha kasoro zilizojitokeza mara moja. Vinginevyo itabidi wafutiwe mikataba waliyoingia na Jeshi. Utekelezaji wa agizo hili unafuatiliwa kwa ukaribu sana na Uongozi wa Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya elimu ya msingi katika shule zake nane zilizoko katika makambi ya Bulombora (Kigoma), Ruvu (Pwani), Oljoro (Arusha), Makutupora (Dodoma), Mgambo na Maramba (Tanga), Chita (Ifakara) na Mlale (Ruvuma). Shule zote hizi zina jumla ya wanafunzi 2,630 na zimekuwa za msaada sana katika kuwapatia elimu siyo tu watoto wa familia za Maafisa na Askari wa JKT, bali na watoto wa familia za wananchi wanaoishi jirani na shule hizo ikiwa ni pamoja na kuwapatia ajira waalimu na wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha uboreshaji wa mafunzo ya ufundi (*Vocational Training*), hatua zimechukuliwa za kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali iliyopo. Hii ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika makambi ya Makutupora, Mlale, Maramba na Bulombora. Ukarabati huo bado unaendelea. Vijana wa kuitolea wa Operesheni Mkapa na Operesheni Miaka 40 ya JKT wapatao 2,195 wamekwisha pata mafunzo ya ufundi stadi, kilimo na usugaji.

Mheshimiwa Spika, JWTZ na JKT yameendelea kuimarisha huduma za elimu ya Sekondari katika shule tisa zinazomilikiwa na Jeshi. Shule hizo ni *Makongo High School*, Sekondari ya Airwing, Kigamboni, Nyuki, Unyanyembe, Ruhuwiko, Kizuka, Kawawa na Jitegemee. Jumla ya wanafunzi wapato 11,428 wanaendelea na masomo yao katika shule hizi ambazo wengi ya wanafunzi waliopo ni watoto wa raia kutoka sehemu mbalimbali nchini. JWTZ na JKT pia yameendelea kuwafadhili na kuwadhamini wanajeshi na watumishi raia kwa kuwapeleka kusoma katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, michezo kwa wanajeshi wote katika Fomesheni, Brigedi, vikosi na vyuo katika Jeshi la Ulinzi na JKT imefanyika kama inavyotakiwa kwa kila mwanajeshi kushiriki katika michezo. Timu teule za Jeshi za mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa wavu na masumbwi zimeshiriki katika mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na kuibuka washindi wa kwanza na wa pili. Tunawapongeza sana mashujaa wetu hawa kwa kulijengea Taifa letu sifa na heshima. Katika Michezo ya Majeshi ya Dunia iliyofanyika Desemba, 2003 nchini Italia wanamichezo wetu walishiriki na kurudi na ushindi wa kujivunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa utendaji katika Idara zake unazingatia misingi ya sheria na taratibu zilizowekwa. Lengo ni kuongeza ufanisi katika shughuli za vyombo vya kiulinzi. Hii ni pamoja na watusika wote katika sehemu zao za kazi kuwa waadilifu, wanaozingatia nidhamu na busara katika matumizi ya fedha na mali za Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa misingi hiyo hiyo vitendo vya rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali za Umma havitavumiliwa. Maafisa, askari na wafanyakazi wameendelea kupatiwa elimu kuhusu vitendo hivyo viovu.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara imeshiriki katika kuandaa mpango maalum wa Serikali wa kuimarisha huduma zake ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na Wizara na Taasisi zake zinalingana na matarajio ya wananchi na wadau wengine. Mpango huu ambao uko katika hatua za mwisho utaiwezesha Wizara kuweka malengo yanayopimika na kutekelezeka kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa Hotuba yangu nimetoa maelezo kuhusu jinsi wanajeshi wetu walivyoshiriki kwa nguvu zao zote katika operesheni mbalimbali za kusaidia mamlaka za kiraia na wananchi kwa ujumla wakati wa amani, lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kuwa wananchi na mali zao wanaishi kwa usalama. Kwa ujasiri mkubwa Wanajeshi wetu wamediriki hata kuyaweka maisha yao rehani wakati wa kukabiliana na baadhi ya matukio na majanga hatari kwa Taifa na wananchi wetu. Taifa halitasahau ajali mbaya sana ya treni iliyotokea katikati ya maeneo ya Igandu na Msagala mkoani Dodoma ambako ndugu zetu 283 walipoteza maisha. Kama mtakavyokumbuka, wanajeshi wetu walishiriki kikamilifu katika shughuli za uokoaji katika ajali hiyo mbaya. Walishiriki pia katika kazi ya uokoaji kufuatia ajali ya kivuko cha Mto Kilombero na katika mazoezi mengine ya uokoaji na urejeshaji wa miundombinu inayoharibiwa na mafuriko sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wetu kwa kushirikiana na mamlaka za kiraia, wameweza kushiriki pia katika ujenzi wa shule, hospitali, matengenezo ya barabara na madaraja na hata kutoa damu kwa lengo la kuokoa maisha. Vivyo hivyo, katika kutambua michango ya viongozi wetu wa Kitaifa, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa yamechukua hatua za kuweka ipasavyo kumbukumbu za kihistoria za Waasisi na Viongozi wa Taifa letu kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Katika hili makaburi ya waasisi wa Taifa letu yaani Marehemu Julius K. Nyerere, Marehemu Aman Abeid Karume na Marehemu Edward M. Sokoine, yameweza kujengwa kwa kiwango cha Kimataifa. Mipango ya kuyajengea makaburi ya Marehemu Dr. Omar Ali Juma na Marehemu Abdul Wakil, inaandaliwa. Makaburi yote hayo yataendelea kutunzwa na JWTZ/JKT. Wakati huo huo, mbali na makaburi, ukarabati mkubwa umekamilishwa katika makazi ya Mheshimiwa Abdu Jumbe, Rais wa Zanzibar na Makamu wa Rais Mstaafu. Jeshi letu pia lina mpango wa kuhakikisha kuwa makazi ya Marais wetu na Mawaziri Wakuu wastaafu kila wakati yanawekwa kwenye hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya katika kipindi cha mwaka uliomalizika katika sehemu chache nchini, yamekuwapo matukio ya Wanajeshi wachache kugombana au kuwaonea raia. Matukio haya yametusikitisha na kutufedhehesha sana, kwa kuwa yametia doa sifa nzuri ya wanajeshi wetu. Naomba nikiri kuwa wanajeshi sio malaika. Wao pia ni binadamu, na hakuna binadamu aliyekamilika. Yaliyotokea ni makosa ya kibinadamu yaliyofanywa na wanajeshi wachache. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara na uongozi wa Jeshi hatutasita kuwachukulia hatua za kinidhamu wanajeshi wanaokwenda kinyume na Sheria. Kwa upande mwingine ningelipenda kuwaomba wananchi nao kutotumia lugha chafu au kufanya vitendo vya kuwadhalilisha wanajeshi wetu. Kitendo cha kumvamia nyumbani kwake mwanajeshi na kumuua kikatili mbele ya familia yake, ni kitendo cha kinyama na cha kulaaniwa na wote wanaopenda haki na amani. Hivyo, ni wajibu wetu sote kudumisha upendo, mshikamano na ushirikiano ili kuliepusha Taifa na vurugu.

Mheshimiwa Spika, ukamilishaji wa Sera ya Ulinzi ya Taifa umechukua muda kuliko ilivyotarajiwa kutokana na umuhimu wake kwa maslahi ya Taifa letu. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, rasimu ya Sera hiyo imekamilika na itawakilishwa kwa vikao vya kitaifa vinavyohusika na Ulinzi na Usalama kulingana na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litasherehekeza miaka 40 tangu kuundwa kwake. Wale wanaopenda ukweli wanautambua mchango mkubwa wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na hasa katika nchi za sasa za *SADC*. Kwa nyakati mbalimbali, kuanzia mwaka 1960 hadi 1990, Watanzania walilazimika kuchangia nguo, chakula, fedha, mifugo na hata damu kwa ajili ya wapigania uhuru wa nchi za Namibia, Angola, Msumbiji, Zimbabwe na Afrika Kusini. Baadhi ya Mashujaa wetu walipoteza maisha yao katika vita vya ukombozi na katika kutetea uhuru na utu wa wananchi wa Namibia, Angola, Msumbiji, Zimbabwe, Seycheles, Afrika Kusini, Uganda na Comoro. Ili kuwaenzi wote walioutoa uhai wao kwa kuiweka historia bayana, Serikali imeamua kurudisha nchini masalia ya mashujaa wetu waliozikwa Msumbiji na nchi nyingine na kuyazika upya kwa heshima zote za kijeshi kuanzia Agosti, 2004 katika eneo maalum lililotengwa karibu na mji wa Mtwara. Shughuli hizi zitakuwa ni sehemu ya Sherehe ya Jeshi kutimiza miaka 40 tangu liundwe na zitafikia kilele chake tarehe 1 Septemba, 2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia itajenga mnara wa makumbusho ya mashujaa wetu wote walipoteza maisha yao katika kuitetea Tanzania na Afrika. Uamuzi ni kuujenga mnara huo Makao Makuu ya Serikali yaani Dodoma. Katika kuutekeleza mpango huu wa kihistoria, nimemteua aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Jackson Makwetta, kuuratibu mpango huu kwa kushirikiana na Makao Makuu ya Jeshi. Nampongeza sana Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwa kuwa mstari wa mbele tangu alipokuwa Waziri wa Ulinzi, kubuni na kutetea wazo hili la kurudisha nyumbani masalia ya mashujaa wetu na kuwajengea Mnara wa Kumbukumbu wa kihistoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa kwa mwaka 2003/2004, katika mwaka 2004/2005, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeazimia kuendelea na mkakati wa kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia vitendeakazi bora vya kisasa, kuimarisha mafunzo na kujenga mazingira mazuri ya kazi. Mambo muhimu yanayotarajiwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Ununuzi wa madaraja ya muda (*Bail Bridges*) kwa matumizi ya dharura;
- (ii) Kuendelea na ukamilishaji wa viporo vya nyumba za kuishi wanajeshi katika makambi ya Makoko (Musoma), Kange (Tanga), Makambako (Iringa), Kibaha (Pwani) na Lugalo (Dar es Salaam) ili kupunguza tatizo la makazi kwa wanajeshi;
- (iii) Kuendeleza matengenezo/ukarabati wa baadhi ya nyumba za kuishi na majengo mengine muhimu katika makambi; ikiwemo majengo katika kambi ya Wawi Pemba;
- (iv) Kuimarisha mafunzo kwa njia ya mazoezi ya kijeshi ili kuendelea kuyaimarisha majeshi yetu pamoja na kutoa taaluma mbalimbali kwa watumishi na vijana wanaojiunga na JKT;
- (v) Kuendelea na ukarabati wa Kiwanda cha Mzinga;
- (vi) Kuendeleza kwa nguvu zaidi ukarabati wa mabweni, vyumba vya kusomea na miundombinu katika baadhi ya makambi ya JKT ambayo yanatarajia kuendesha mafunzo kwa vijana;
- (vii) Kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatoo ya Mradi wa Mtandao wa Mawasiliano ya Kipekee (*ITN*);
- (viii) Uendelezaji wa utafiti wa magari ya NYUMBU;
- (ix) Uimarishaji wa maghala ya silaha;
- (x) Ukarabati/ufufuaji wa zana za kijeshi;
- (xi) Kuendelea na ukarabati na ujenzi wa Hospitali saba za Jeshi kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumanii kuititia shirika lake la kijeshi la *German Armed Forces Technical Advisory Group (GAFTAG)*. Hospitali zitakazohusika ni Mirambo (Tabora), Monduli (Arusha), Bububu (Zanzibar), Mazao (Morogoro), Nyumbu (Pwani), Navy (Dar es Salaam) na Makao Makuu ya Brigedi ya Kusini, Songea (Ruvuma).
- (xii) Matengenezo ya magari, mitambo na vifaa vya kijeshi;
- (xiii) Kulipia malipo ya awali ya helikopta mbili mpya na magari ya Jeshi kulingana na mikataba itakayofikiwa;

- (xiv) Kuimarisha mafunzo ya ufundi, kilimo na taaluma nyinginezo kwa vijana wa JKT;
- (xv) Ununuzi wa sare za kutosheleza mahitaji ya Wanajeshi na vijana wa JKT; na
- (xvi) Kukamilisha malipo ya mwisho ya ndege mbili za usafirishaji za Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu ningelipenda kuchukua fursa hii tena kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa uongozi wake thabiti na makini kuhusu suala la ulinzi wa nchi yetu. Amiri Jeshi Mkuu amekuwa akifuatilia kwa karibu sana jukumu zima la ulinzi wa nchi yetu ikiwa ni pamoa na kuwa karibu na hatua za utatuza wa matatizo ya wanajeshi. Amefanya jitihada kubwa kuliimarisha Jeshi lake kwa kulipatia vitendeakazi na huduma nyingine zile za msingi kwa Askari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ningelipenda kuwashukuru kwa dhati Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Aman Abeid Karume na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, kwa kuwa karibu nasi. Nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu katika shughuli zake kwa ufanisi na umahiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda pia kutoa shukrani kwa Serikali za nchi zifuatazo zilizoshirikiana nasi katika maendeleo mbalimbali: Jamhuri ya Watu wa China, Shirikisho la Ujerumani, Ufaransa, India, Uingereza, Canada, Marekani, Falme za Nchi za Kiarabu, Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bwana Bernard S. Mchomvu. Shukrani zangu pia ziwaendee Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George M. Waitara, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Luteni Jenerali Iddi S. Gahhu na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali David A. Mwamunyange. Wote nawashukuru kwa msaada walionipatia katika kuendesha shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nitakuwa mtu asiye na fadhiba kama sitamshukuru sana Bwana Vincent F. Mrisho, Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, ambaye amenisaidia sana katika kipindi chote alichokaa nami. Ninamtakia mafanikio katika Wizara yake mpya. Nawashukuru pia Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Makamanda na Wapiganaji wote wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa. Wote nawashukuru kwa ushirikiano mkubwa walionipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, namshukuru Mpiga Chapa wa Serikali na wafanyakazi walio chini yake, kwa kuichapisha Hotuba hii na kuikamilisha kwa wakati na wafanyakazi wa vyombo vyote via habari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hakuna Taifa lolote lenye nguvu za kiuchumi, kiteknolojia au kijeshi ambalo litakuwa tayari kutoa majeshi yake kwenda kulinda nchi nyine iliyo huru. Jukumu la Ulinzi wa Taifa lolote lile ni la Taifa lenyewe. Kama aliviyotuasa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, wakati alipokuwa akifunga zoezi la kijeshi lililoshirikisha vikosi via Kamandi ya Ulinzi wa Anga katika eneo la Msata - Bagamoyo mwaka 2001, Rais alisema: "Jukumu la Ulinzi wa Taifa letu ni suala la Taifa lenyewe kutokana na unyeti wake kwa maslahi ya Umma wa Tanzania. Jukumu la ulinzi wa Taifa ni jukumu la Taifa na wala haliwezi kuachiwa nchi wahisani kama inavyofadhiliwa miradi mbalimbali ya kimaendeleo hapa nchini, wala suala hili sio la kufanya mzaha. Ulinzi wa Taifa ni suala muhimu na la pekee kwa umuhimu wake na Taifa litajizatiti kuendelea kugharamia, kuimarisha na kuboresha Jeshi lake kwa maslahi ya Taifa". (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa ya Majeshi yetu katika utekelezaji wa majukumu yao ya ulinzi wa Taifa letu yanatokana na hekima, busara na upeo wa kuona mbali wa waasisi wa Taifa na Jeshi letu, Marehemu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Aman Abeid Karume, uongozi thabiti wa Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litaendelea kuwaenzi na kuwakumbuka kwa kazi nzuri waliyolifanyia Taifa letu. Ushirikiano wa Umma wa Tanzania wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, hii ni pamoja na Sera safi na mafunzo bora ya ulinzi ambayo nguzo zake muhimu ni utii, uhodari, uzalendo na nidhamu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na misingi hiyo, Jeshi la Ulinzi litatumia kila lilicho nacho katika kulinda na kutetea Muungano wetu, uhuru wetu, umoja wetu, mshikamano wa Taifa letu, Katiba ya Jamhuri, amani na utulivu wa nchi yetu, halitavumilia nchi au mtu ye yoyote kuvuruga/kuchezea Mungano wetu, uhuru wetu, umoja wetu, mshikamano wa Taifa, amani na utulivu wa nchi yetu. Hawatavumilia nchi yoyote au mtu ye yoyote kumdhihaki Amiri Jeshi Mkuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake liweze kutekeleza majukumu yaliyoelezwa katika hotuba hii kwa mwaka 2004/2005, naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 214,158,052,800/= fedha za hapa nchini ambazo kati yake shilingi 169,148,052,800/= zitatumika kwa ajili ya kulipia mishahara, chakula cha wanajeshi na vijana wa JKT na matumizi mengine na shilingi 45,010,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mgawanyo ufuatao:-

(a) Matumizi ya Kawaida:

(i) Fungu 38 - Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, shilingi 136,634,251,500/=.

- (ii) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa, Sh. 27,561,135,300/=.
- (iii) Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 4,952,666,000/=

(b) Matumizi ya Maendeleo:

- (i) Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 45,010,000,000/=

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JOHN S. MALECELA - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Wizara hiyo ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Laurence M. Gama, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Gertrude I. Mongella, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Thomas S. Nyimbo, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Major Jesse J. Makundi, Mheshimiwa Frank G. Maghoba, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nasoma kwa mara ya kwanza taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda kuanza kwa kumpa pole Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa operesheni aliyofanyiwa hivi karibuni huko Uswiss. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ili apone haraka. Aidha, tunampongeza kwa jitihada zake za kuimarisha uwezo wa vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon M. Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Ndugu Bernard S. Mchomvu, Katibu Mkuu na Sekretarieti ya Wizara, kwa kazi yao nzuri ambayo wameifanya na kuiwezesha Kamati hii kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kupata Ubunge kuitia Chama cha Mapinduzi. Pia nawapongeza Wabunge wengine wote, waliopewa nyadhifa za Kitaifa na za Kimataifa nikianza na Mheshimiwa Balozi Gertrude I. Mongella, ambaye ni Mjumbe wa Kamati hii, tunapongeza kwa kuchanguliwa kwake kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo natumia fursa hii kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, kwa kufiwa na baba yao. Aidha, nawapa pole Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama na Mheshimiwa Parmukh S. Hoogan, kwa kufiwa na watoto wao. Natoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yet S. Mwalyego na wakazi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kufiwa na Mbunge wao na kwa familia ya Marehemu na wakazi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kifo cha Marehemu Mheshimiwa Kapteni Theodos James Kasapira, kilichotokea tarehe 22 Julai, 2004. Mungu aziweke roho za Marehemu wote mahali pema peponi. *Amina.* Vile vile nawapa pole Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa kupata ajali wakiwa njiani kuja Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwa niaba ya familia yangu, kutoa shukrani kwa pole nyingi tulizozipata kufuatia mkasa wa kuvamiwa na majambazi alioupata mke wangu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, akiwa njiani kuja Bungeni Dodoma. (*Makofî*)

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, aliwasilisha mbele ya Kamati taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Wizara yake alizozitoa Bungeni pamoja na utekelezaji wa ushauri wa Wabunge uliotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara ya mwaka uliopita. Kamati inaipongeza Wizara hii kwa kutekeleza kwa kiwango kikubwa malengo yaliyokuwa yamepangwa. Zaidi ya yote, Kamati inalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi kudumisha utulivu na amani.

Mheshimiwa Spika, tunalipongeza Jeshi la Wananchi pia kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya ujenzi wa nyumba za Serikali Mbweni kule Dar es Salaam na Mwangaza hapa Dodoma na nina hakika kwa Wabunge wote mlionhudhuria uwekaji wa jiwe la msingi jana na Rais wetu wa Jamhuri, mlajionea wenyewe kazi nzuri inayofanywa na wanajeshi wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ilieleza kuwa mpango wa kulipatia Jeshi vitendea kazi bora vya kisasa na kujenga nyumba za kuishi askari unatekelezwa hatua kwa hatua kutokana na ufinyu wa bajeti. Pamoja na nyongeza za fedha zinazotolewa kwa Jeshi hilo, mahitaji bado ni makubwa. Aidha, upimaji wa ardhi ya majeshi ili yapewe hati za kuyamiliki unaendelea kufanyika isipokuwa kwenye maeneo yenye migogoro kati ya majeshi yetu na Wananchi wanaozunguka maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua kwa undani kuhusu suala la Jeshi la Ulinzi wa Majini (*Navy*) na kutathmini baadhi ya mapungufu yanayolikabili Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza na kusisitiza kwamba, Serikali iendelee kuchukua hatua thabiti katika mambo yafuatayo:-

- Kuimarisha mafunzo kwa Maafisa na Wapiganaji wa Jeshi hilo ili kufikia utaalam wa juu.
- Kuimarisha ulinzi wa majini hasa katika mipaka yetu ya majini ambayo ni maili za majini 200 ambayo ni sawa na kilomita 320 kutoka nchi kavu pamoja na kudhibiti uvuvi haramu uwe ule uvuvi ambao watu hawana leseni kutoka nchi za nje na uvuvi haramu wa kutumia bahari au baruti katika bahari yetu.
- Kuimarisha karakana ya kukarabati na kutengeneza meli na mitambo. Karakana hiyo hivi sasa, haifanyi kazi kwa ukamilifu. Endapo kituo hicho kitawekwa chelezo chenye uwezo mkubwa, karakana hiyo itaokoa fedha za kigeni kwa kutokupeleka meli zetu nchi za nje kwa matengenezo na pia karakana hiyo itakuwa na uwezo wa kutengeneza meli za watu binafsi na kwa njia hiyo kuipatia nchi yetu mapato.
- Kuboresha nyumba za kuishi askari na Maafisa pamoja na majengo mengine yaliyojengwa miaka ya nyuma ambayo yamechakaa hivi sasa.
- Kuboresha upatikanaji wa maji katika baadhi ya vikundi vya Majeshi yetu.
- Kuwa na magari yanayokidhi usafiri wa kikazi.
- Kuwa na huduma ya zimamoto na uokoaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza China kwa misaada mingi ambayo kwa unyeti wake hatuwezi kuitaja ambayo inatoa kwa Jeshi letu la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati imeona mapungufu ni la kuharibika kwa barabara za ulinzi ambapo katika baadhi ya maeneo sasa hivi hazipitiki kabisa. Katika mpaka wa magharibi ambako hali ya usalama kwa nchi jirani si nzuri, barabara za ulinzi zinahitajika kupitika muda wote. Aidha, Askari walioko huko wanastahili kuongezewa motisha, kama vile nyongeza ya posho ya chakula (*Ration Allowance*), pamoja na kupunguza muda wa kukaa huko mipakani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa mwaka uliopita, Waziri aliwasilisha mbele ya Kamati, maombi ya fedha za matumizi ya kawaida na matumizi kwa ajili ya maendeleo ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitafakari taarifa ya utekelezaji ya mwaka wa fedha uliopita pamoja na malengo na makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2004/2005 na kutoa maoni na ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati kuhusu shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni huu ufuatao:-

- Serikali iongeze kasi ya kulipatia Jeshi la Wananchi wa Tanzania vitendea kazi bora veya kisasa na kuwapatia askari nyumba za kuishi. (*Makofî*)
- Serikali iongeze kasi ya kupima maeneo yote ya Majeshi na kutoa hati za kumiliki maeneo hayo. (*Makofî*)
- Serikali idhibiti matumizi ya ardhi yasiyo ya kijeshi kwenye maeneo ya majeshi. Tulikuta kwamba kuna eneo kubwa la kijeshi halafu watu wanaanza kulima mle ndani na kadhalika sasa tunasema haya yadhibitiwe. Aidha, migogoro ya ardhi katika maeneo ya Jeshi itafutiwe ufumbuzi mapema.
- Serikali idhibiti kufanyika shughuli za kitalii na raia kujenga karibu na maeneo ya majeshi. Hapa tulichotaka kusema ni kwamba, mahali pengine tuna *vital installations* za Jeshi, sasa unakuta watu wanaanza kujenga karibu na sehemu hiyo, sisi tunasema jambo hili kwa kweli lidhibitiwe. (*Makofî*)
- Serikali itunge sheria ya kuweka kipimo maalum cha eneo la wazi kati ya maeneo ya majeshi na yale ya raia. (*Makofî*)
- Serikali iimarishe ulinzi wa majini na kuongeza jitihada za kuinua viwango veya elimu kwa askari wa majini.
- Serikali iimarishe barabara zote za ulinzi na tunaomba kwamba jambo hili lipewe Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ndio liangalie barabara hizi badala ya kusema ziangaliwe na Ujenzi au na Mikoa au na Wilaya, tunataka Jeshi lenyewe ndio lipewe fedha kuangalia barabara hizi. (*Makofî*)
- Askari wanaofanya kazi kwenye mipaka yenyé mazingira magumu wapewe motisha. (*Makofî*)
- Vifaa vyote veya Jeshi la Ulinzi vilivyochakaa vitengenezwe, kama haviwezi kutengenezwa basi viharibiwe ili vyuma vile viweze kutumika kwa kutengeneza vitu vingine na hii itasaidia kuweka mazingira ya mahali pa Jeshi kuwa mazuri.
- Kamati inaishukuru Serikali kwa kuongeza bajeti ya Mashirika ya Mzinga na NYUMBU. Hata hivyo, mashirika hayo yaendelee kuimarishwa zaidi ili yaweze kuzalisha bidhaa bora na kwa wingi na ningependa kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, hapo nje yapo magari mawili ambayo yametengenezwa na kiwanda cha Nyumbu na vijana wetu wenyewe na tutaomba mtakapopata nafasi, mwende mkayaone ili muweze kuona kazi nzuri ya vijana wetu.
- Serikali itunge sera ya kudhibiti uingizaji, usambazaji na utumiaji wa baruti, kwa sababu wengi tunajiuliza hivi hawa wavuvi haramu hizi baruti wanazipata wapi, kwa hiyo, kama wanaweza kuzipata basi Serikali inahitajika kudhibiti jambo hilo.

- Brigedi za Ujenzi za Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, zipewe tenda za kujenga barabara za ulinzi, madaraja na majengo ya Serikali. Tunapenda pia kumpongeza Waziri wa Ujenzi, kwa jitihada zake za kuzipa tenda vyombo hivi nya ulinzi na usalama. (*Makofi*)
- Serikali ipeleke maji ya bomba kwa vikosi vyenye matatizo ya maji.
- Serikali ikamilishe uandikaji wa sera mpya ya ulinzi na katika sera hiyo suala la kustaafu kwa Wanajeshi liangaliwe upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ilichambua makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2004/2005 na kuyapitisha bila marekebisho na tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, wakubaliane nasi wayapitishe bila marekebisho. Matumizi ya Kawaida: Ngome - Fungu 38, Sh. 136,634,251,500/=, Jeshi la Kujenga Taifa - Fungu 39, Sh. 27,561,135,300/= na matumizi ya Wizara - Fungu 57, Sh. 4,952,666,000/= na fedha kwa ajili ya maendeleo - Fungu 57, Sh. 45,010,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu, ningependa tena, hata kama ni kurudia, kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yetu kwa usikivu wake aliyoipa Kamati hii ya Ulinzi na Usalama. Kutokana na yeye kuvipa vyombo vya Dola umuhimu mkubwa, tumeshuhudia ongezeko la bajeti ya vyombo hivyo mwaka hadi mwaka. Ongezeko hilo limesaidia kuboresha vitendea kazi na huduma kwa waendeshaji wa vyombo hivyo katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, ulinzi wa Tanzania ni jukumu la sisi Watanzania. Tunampongeza sana Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2004/2005. Aidha, nakushukuru wewe binafsi na kukupongeza kwa jinsi ulivyoledesha Bunge letu kwa ufanisi wa hali ya juu. Pia napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa ushirikiano wao mkubwa ulioiwezesha Kamati hii kuweza kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia tena, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu, lijadili na kuidhinisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 43(5)(b)(c) na 81(1),

Toleo la 2004, naomba kwa ruhusa yako niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005, nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na Wananchi wa Jimbo la Vunjo, napenda kuungana na wenzangu, kutoa rambirambi zetu za dhati kabisa kwa Wananchi na familia za Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijiji na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kwa msiba mkubwa wa kuondekewa na waliokuwa wapendwa Wabunge wao. Mwenyezi Mungu, azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi. Mwenyezi Mungu ndiye anatoa na ndiye anatwaa, jina lake lihimidiwe. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapa pole Wabunge wote waliopatwa na mikasa katika kipindi chote hiki. Mungu atawasaidia sana katika majeraha waliyoyapata. Hii ni hali ya dunia, poleni sana. Namtakia Amiri Jeshi Mkuu, afya njema na Mwenyezi Mungu amponyeshe mguu wake mapema.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Mbunge wa Ranya na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake nzuri ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2004/2005, inayoweka matumaini mema na ya kuwatia moyo Maafisa na Wapiganaji wa JWTZ na JKT.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake, wapitie upya hotuba za Waziri mwenyewe na Waziri Kivuli za tangu mwaka 2001 hadi 2004, waone ni yapi yametekelezwa na ni yapi hayajatekelezwa na ufumbuzi wake ni nini. Hii itakuwa ni *Checks and Balances* ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamshukuru Waziri wa Fedha kwa kuipa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, fedha mara mbili zaidi ya bajeti ya mwaka 2003/2004 na inaamini kuwa fedha hizo zitatumika kwa malengo yaliyowekwa. Ubahirifu wa aina yoyote usipewe nafasi ndani ya Jeshi letu. Watakaobainika wachukuliwe hatua kali ikiwa ni pamoja na kufilisiwa. Tunaamini pia Mahakama ya Kijeshi (*Court Marshal*), imetengewa fedha za kutosha kwa kazi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niangalie baadhi ya masuala kuhusu Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama ifuatavyo:-

Kambi ya Upinzani inasikitika sana kwani inaamini kuwa kati ya idara zenye nidhamu ya kila kitu ni Jeshi kwa ujumla, lakini hiyo inaonekana ni tofauti na mtazamo wetu na Watanzania kwa ujumla, kwani ukiangalia taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali utaona kuna ubahirifu mkubwa na matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi yasiyo na maelezo. (*Makofî*)

Matumizi ya Sh. 5,351,595,809/= hayakuwa na utaratibu unaoelewaka, *outstanding imprest balance* Sh. 42,966,778/=, aidha, Wizara imeshindwa kutoa vielelezo nya matumizi ya Sh.109,833,911/= kama ilivyotakiwa na *Auditor General*.

Mheshimiwa Spika, pesa zilizolipwa kama manunuzi kwa Sam Brown Belts, ziliongezwa (*Over Payment*) kwa Sh. 125,538,000/=, mishahara yakutatanisha kwa askari jumla ya Sh. 544,804,734/. Aidha, zipo zabuni zinazotolewa katika vikosi mbalimbali kama ilivyoonyeshwa kwenye taarifa hiyo ambazo hazifuati kanuni na taratibu za zabuni, jambo ambalo linalitia aibu jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inamshauri Waziri pamoja na Mkuu wa Majeshi, aangalie na kuyatafutia ufumbuzi matumizi mabaya ya pesa za walipa kodi kama inavyoonyesha kwenye taarifa ya Mkaguzi na Mdhhibitii Mkuu wa Serikali, mpaka Juni, 2003 kulikuwa na jumla ya *audit queries* 48, mpaka sasa tunamwomba Waziri, alieleze Bunge ni ngapi zimejibowi na ngapi bado na kwa nini?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, Kambi inashauri mambo yafuatayo yatiliwe mkazo na kuangaliwa upya:-

(a) Ujira, maslahi na kiwango cha maisha (*Standard of Living*) ya Maafisa na Wapiganaji siyo ya kuridhisha sana. (*Makofi*)

(b) Shughuli za kiuchumi ndani ya majeshi yetu inaonyesha ni nzuri na inatia moyo katika Jeshi la kujenga Taifa, lakini kwenye Mradi wa Jeshi la Ulinzi kwenye uchimbaji wa Dhahabu (MEREMETA), bado mambo hayako bayana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni vyema Viongozi wetu Wakuu wakajenga utamaduni wa kuiweka karibu na vikosi nya Askari wetu. Mfano mzuri mno na wa kuigwa ni ule wa Amiri Jeshi Mkuu wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alipovaa sare ya Jeshi (*Combat Dress*) na kutembelea vikosi nya mpakani Mtukula pindi tulipovamiwa na Marehemu Nduli Iddi Amini mwaka 1978/79. Mwalimu Nyerere pia alikuwa anatembelea vikosi vyote na mara nyingi alikuwa anatoa taarifa ya saa chache sana. Hii ilikuwa inalipa Jeshi letu *morale* ya hali ya juu sana na uwajibikaji mzuri.

Kambi ya Upinzani inamwomba Amiri Jeshi Mkuu, apange utaratibu utakaowawezesha Viongozi wetu Wakuu wa nchi kupata muda wa kukaa na Askari wetu hasa wale waishio vikosini mbali na mijini, ili kuelewa mazingira na hali halisi wanamoishi na kufanya kazi, kitu kitakachosaidia kuwapa moyo na kujiona na wao ni sehemu muhimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, umilikaji wa ardhi kwa shughuli za kijeshi utenganishwe na makazi ya kiraia, kwani imeonyesha Askari wanajenga makazi yao binafsi kwenye maeneo yanayomilikiwa na jeshi, pindi wanapostaa fu inaleta migogoro kwani inakuwa ni vigumu kuhama makazi yao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Majini (*Navy*), litumike kukomesha wavuvi haramu toka nje ya nchi, wanaovua bila vibali kwenye eneo letu la bahari, hivyo Jeshi lishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii, kitengo cha uvuvi kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini baadhi ya mambo yafuatayo watakumbana nayo wakati wakitembelea vikosi hivi:-

(a) Malalamiko ya mishahara isiyoendana na wakati hasa kwa kushuka thamani ya shillingi, vyakula kupanda bei, vifaa vya kukidhi maisha kupanda bei na hali ngumu ya kutunza familia kwa mshahara huo.

(b) *Ration Allowance* ndogo kwa kapera na waliooa ambayo haiendani kabisa na kupanda kwa gharama za maisha.

(c) *Hardship Allowance* kwa wale wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu na ya kuhatarisha maisha yao hasa wanaolinda mipaka ya nchi yetu.

(d) *Instructors Allowance* (Posho ya Wakufunzi) iliyowekwa mwaka 1984 irekebishwe iendane na wakati.

(e) Kutopandishwa vyeo kwa wakati japo sifa zote stahili zimekamilika na kwa kuwa kupandishwa cheo na uhamisho ni utamaduni wa Majeshi yote duniani. Hilo lifanyike ili kudumisha nidhamu JWTZ na JKT.

(f) Mafunzo ya *Peace Keeping Operation* yaimarishwe na kudumishwa na kama ikiwezekana yawahuvishe hata watu wengine makazini na sio kwa Askari tu, kitu kikubwa ni kuweka utaratibu mzuri.

(g) Wanajeshi wapelekwe kwenye *Peace Keeping Operations* duniani pote watakapohitajika. Hii itaimarisha sana Jeshi la Tanzania.

(h) Mazoezi ya Kivita ya pamoja na Majeshi ya nchi za nje yadumishwe ndani na nje ya Tanzania. Hii pia italikomaza Jeshi la Tanzania kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi kama sehemu ya nchi na uchumi, bado ina jukumu kubwa katika kuongeza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo na viwanda, hivyo jeshi kuwa na wataalam katika nyanja nyingine za uzalishaji ni muhimu na wao wako katika nafasi kubwa ya kuongeza uzalishaji kutokana na nidhamu kubwa inayotawala katika chombo hiki. Aidha, tunaishauri Serikali na Jeshi liingizwe kwenye kandarasi za kujenga barabara na miradi mingine mikubwa na hii itakuwa ni moja ya ajira ya kuliingizia Jeshi letu mapato.

Mheshimiwa Spika, Sheria za kustaafu zibadilishwe kama ifuatavyo:-

- Miaka 70 ya kuzaliwa iwe ni kustaafu kwa lazima.

- Miaka 60 ya kuzaliwa na kutumikia Jeshi miaka 30 mfululizo iwe ni rekebisho la *Forces Routine Order* ya Novemba, 1992 inayomtaka Mwanajeshi aombe kustaafu baada ya kuwa Jeshini miaka 20 tu.
- Mwanajeshi mstaafu wa cheo chochote anaweza kuajiriwa Jeshini kwa mkataba maalumu pale inapoonekana inafaa kutokana na taaluma yake na avae kiraia au kijeshi kama itakavyoamuliwa.

Mheshimiwa Spika, wanaostaafu kwa umri mdogo huikimbia nchi na kuajiriwa nchi za nje kama vile Uganda na *DRC* na kudhoofisha Jeshi letu kitaalam na kunufaisha Majeshi ya nchi nyingine, jambo ambalo ni hatari sana kivita kwa nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumfundisha Afisa mmoja *Staff College* Marekani kwa mwaka 1990 ni *USD* 125,000 na kwa sasa ni *USD* 140,000 na eti mara tu baada ya kutoka huko na ameshafanya kazi Jeshini miaka 20 mfululizo kwa mujibu wa *FRO* ya Novemba, 1992, anaomba kustaafu na eti anaruhusiwa baada ya fedha zote za jasho la Watanzania kupotea.

Mheshimiwa Spika, pensheni ya waliostaafu ni kilio na adhabu kwa wale waliostaafu miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, inaombwa pensheni zote zilingane kwani Afisa wa Cheo chochote na mpiganaji wa cheo chochote anastaafu baada ya kufanya kazi iliyotukuka na kufikia cheo kilichotukuka. Hakuna tumbo dogo kwa aliystaafu 1970 na tumbo kubwa kwa aliystaafu mwaka 2004. Wote wapewe pensheni sawa na inayoendana na hali ya maisha ya sasa. Hii itaondoa kabisa umamluki na ujambazi uliokithiri hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Tanzania Legion* idumishwe, iendelezwe na wahanga wa vita vya kwanza vya dunia, vita vya pili vya dunia na vita vya ukombozi wa Bara la Afrika watunzwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu zake zote, lipimwe eneo la ekari 20 za ardhi tambarare kama maeneo ya Dodoma ili ujengwe ukuta imara wenye kuwekwa vibao vya majina (*Plate Names*) kwa wale wote waliofia vitani. Eneo hilo liboreshwe na liwe ni kivutio cha watalii na kumbukumbu kwa vizazi vijavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa majambazi hawachagui ni nani wa kufanyiwa ujambazi, jambo lililopelekea wanajeshi wetu kuuawa na kuporwa mali zao, Kambi ya Upinzani inawataka Wanajeshi wasiwe wapole kama kondoo. Wapange operesheni zao vikosini mwao na wawasake kwa kuwastukiza popote pale walipo, siyo lazima kushirikisha Polisi. Hii ni kuzuia siri isivuje. Kwenye ujangili washirikiane na Polisi kama walivyoshirikiana kwa kutokomeza ujangili Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunashukuru Wanajeshi wetu hawana itikadi ya Chama chochote, ila wanatakiwa wajiandikishe kupiga kura na kupiga kura kila mmoja kwa siri yake na achague kiongozi yeote imani na moyo wake unavyomtuma, wasikubali kutumiwa kwa manufaa ya chama chochote kupata ushindi, wao wanatakiwa wawe mstari wa mbele kuhakikisha kuwa, matokeo ya ushindi wa haki yanalindwa na kuheshimiwa na yeote yule na Watanzania wanaongozwa na yule waliyemchagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *Nyumbu Project* waongezewe wataalam watatu toka Japan wenye ujuzi uliobobea kuhusu uundaji wa magari ili *Nyumbu Project* iwe kitovu cha uzalishaji magari hapa Tanzania na tuweze kuwauzia nchi nyingine za Afrika na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu zake zote, JKT iendelezwe na idumishwe. *Recruitment* ya Askari yeote yule atoke JKT tu. Mawazo potofu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya kuchukua vijana vijijini na mitaani kupeleka CCP Moshi, ikome na kulaaniwa. JKT inapata vijana wake toka kila Wilaya bila upendeleo wowote. Askari bila kupitia JKT hatakuwa na uzalendo wowote wa nchi hii. Atafikiria unyanyasaji, wizi, ujambazi na rushwa tupu na bila huruma. Bila Askari kupitia JKT nchi hii itajaa udhalimu mtupu. Ndiyo maana Amiri Jeshi Mkuu, Rais Benjamin William Mkapa, aliamua kuanzisha upya JKT baada ya kuwa imesimamishwa kwa miaka mingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, samani za SUMA JKT zitafutiwe masoko katika taasisi zetu, nchi za *SADC*, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kadhalika, ili kupata fedha za kigeni hatimaye waweze kutengeneza vifaa/samani bora zaidi kukidhi mahitaji ya soko na wanunuzi.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini yale yaliyotolewa ushauri, Waziri atayafanya kazi kwamanufaa na ufanisi wa JWTZ na JKT.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kwa kuwa taaluma yangu inaniruhusu, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

**MHE WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya wachangiaji wa jumla kuchangia hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri, hotuba inaonekana kweli kwamba, kipara kina busara. Mimi mwanzo nilifikiri kwamba mtu kama ni Profesa wa kuungaunga mifupa kwamba akipelekwa kuunga vyuma anaweza akachemsha, kumbe anaweza kabisa. Nampongeza sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafurahi kwamba, mtazamo mzima na mwelekeo wa Wizara na Serikali kwa ujumla, unaanza kujielekeza zaidi katika kuli-*transform* Jeshi letu na kuweza kwenda na wakati na kwenda na ulimwengu wa utandawazi ambapo kwa

kiasi kikubwa ile *concept* ya uchumi inaanza kupata mwelekeo na kupewa kipaumbele ndani ya Majeshi yetu. Nawapongeza sana kwa hilo. Kwa sababu Tanzania na nchi nyingi za Kiafrika zilikuwa zimechelewa katika suala hili, lakini Mataifa mengine makubwa, majeshi yalishaingia siku nyingi katika mfumo wa kiuchumi na utafiti. Mataifa kama Marekani, Uingereza, Ufaransa ambako teknolojia ya kisasa na inayokwenda kwa kasi inayotumika katika jamii, kwa mfano, simu, ujenzi wa meli zinazokwenda kwa kasi zinazotumiwa na raia, utafiti huu umepewa sana kipaumbele na umeanzia katika matumizi ya Kijeshi. Kwa hiyo, Jeshi letu tunapoanza kuli-*transform* kwa mwelekeo huo mimi kwa kweli napenda kuipongeza Serikali pamoja na Jeshi kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya kazi nzuri ni kazi iliyonekana siku ya jana, wakati Mheshimiwa Rais anaweka jiwe la msingi kwa nyumba 300 hapa Dodoma. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, pamoja na kuzungumza sana kwamba, Kambi ya Upinzani mnaona sasa, mnaona sasa, mimi naomba hata suala hili tulione katika matinki ya manufaa na faida za kuwepo Upinzani. Hii Serikali imekuwa na watu wale wale na sura zilezile kwa miaka 42, lakini sijui kwa nini akili zilikuwa zime-*jam* mpaka kasi ya vichwa vya watu kuanza kufanya kazi kwa uzuri na kupanga mipango kama hii na kutumia Jeshi katika mipango na shughuli za kiuchumi kama hizi, zimeanza kufanyika wakati wa kipindi cha Mfumo wa Vyama Vingi. Mimi nasema lazima tujivunie mfumo huu kwamba, pale mahali ambapo palikuwa pame-*jam*, Kambi ya Upinzani inafanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha kwamba, shughuli inafanyika na busara zaidi inatumika ili kinachotawala pale, ile *logic* badala ya maamuzi yanayopitishwa kwa kutumia nguvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wizara hii imeongezewa bajeti na mimi kama nilivyozungumza toka awali, ningeomba kabisa kwamba, bajeti hii ijielekeze zaidi na iendelee ku-*transform* Jeshi letu. Ikuze uchumi, ilikuze Jeshi katika mwelekeo wa kupanga mambo katika misingi ya kuinua uchumi wake ndani ya Jeshi na Uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kusikia kwamba, kuna utafiti mbalimbali unaofanyika kupidia ndani ya Jeshi na mojawapo hata wenzetu wa Nyumbu leo wametuletea magari. Nimepata bahati ya kuliona lile gari wakati nakuja Bungeni nilikuwa nyuma ya hilo gari japo linatoa moshi mwingi lakini nafikiri ni mwanzo mzuri. Hata ile sauti inayotoka kwenye hilo gari kwa sababu kama tunaingia kwenye ushindani wa kibidhaa, mimi nafikiri mteja anaangalia vitu vingi siyo tu kwamba gari liko barabarani linatembea, atasikiliza hata sauti kama sauti inatisha nafikiri anawenza akatafuta mahali pengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia mimi ningeomba suala hili la utafiti ambalo naomba liendelezwe na lipewe kipaumbele katika Jeshi letu liangalie masuala mengi ambayo sisi hatujayafanya utafiti, tusije tukajikuta tunapoteza muda mwingi kufanya kitu utafiti ambacho tayari kiko katika mfumo wa kiuchumi wa kidunia. Unawenza ukakuta labda mimi sijapata bahati ya kwenda pale Nyumbu na bahati nzuri mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani kwenye hotuba yake amelizungumza na ametaja

*specifically* kwamba, angeomba Idara hiyo itafute wataalam watatu waliobobeia katika utengenezaji wa magari kutoka Japan kwamba tusije tukakuta kikosi hiki kinapoteza muda mwingi kuangalia *mechanism* na *system* nzima ya gari linatengenezwaje wakati wako watu ambao walifanya utafiti huo karne nyingi zilizopita na kuna magari ambayo tayari yako katika mfumo wa kiuchumi na kibashara yanayofanya kazi. Kwa hiyo, wakati tunapofanya utafiti, tujue tunataka kutafuta nini, tunahitaji nini na tunataka kuendeleza nini na tunataka kuuza nini.

Mheshimiwa Spika, ila ningeomba kwamba, Jeshi lingekuwa mahali pazuri kwa ujumla kujenga mahusiano ya karibu kwa Taasisi mbalimbali za kiutafiti tulizonazo hapa nchini. Nazungumza hivyo kwa misingi kwamba, kutokana na uchumi huria ni kwamba, watu wamesambaratika kila mmoja kwa kutafuta anapata wapi au uchumi wake anauendelezea wapi? Kwa hiyo, Watanzania kuwapata katika *system* ile ile ya zamani ambapo mtu ulikuwa ukihitaji kuwapata wakulima unawakuta kwenye Kijiji cha Ujamaa, ukitaka kuwangojea watu wakati wa kununua bidhaa wewe wawekee sukari wote utawapata wanakijiji siku hiyo hiyo. Sasa hivi watu huwezi kuwapata. Lakini Jeshi ni mahali pekee ambapo namba nzuri na kubwa ya Wananchi wetu hao kama jamii wanapatikana katika sehemu moja, wanapatikana katika udhibiti ulio mzuri na mtandao wao wa kimawasiliano unaeleweka. Kwa hiyo, sehemu kama hii kuendeleza utafiti ambao tayari umefanyika katika Taasisi nyingine, mimi nafikiri ni mahali muafaka. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kuna tafiti mbalimbali ambazo tayari zimefanyiwa kazi katika Vyuo vyetu vya Kilimo, mimi naamini kukijengwa mtandao wa pamoja na wa kimashirikiano kwamba utafiti ule uliosanyika katika Vyuo vyetu au Taasisi zetu ambao uko tayari kutumika, ungeweza kuingizwa Jeshini katika mtazamo wa kuendeleza uchumi katika kuendeleza kilimo cha kisasa cha umwagiliaji na watu hawa ndani ya bajeti kubwa kubwa wanazopewa, wakajiwekea *target* ya kuutumia utafiti huo kama mfano hata kwa watu binafsi ambao wanaweza kutaka kuendeleza mafanikio ya utafiti huo. Mimi nafikiri kazi hii inaweza kufanyika vizuri kupitia katika Vikosi vyetu vya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, nigusie ndani ya dakika tano zilizobaki, baadhi ya mambo ambayo ningependa kuyazungumzia hapa. Taifa letu lilishiriki sana katika vita ya kutafuta ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika, ni kazi ya kujivunia na ni kazi iliyotujengea heshima kubwa na ni kazi ambayo mimi naamini hata vizazi vijavyo vitaweza kuienzi na kuiheshimu.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ningeomba kwamba mambo yanabadilika na kila mambo yanapobadilika hata watu mawazo na mitazamo inabadilika. Hivi sasa nchi nyingi ambazo tulizisaidia katika kutafuta ukombozi hata Marais wake waliokuwa pale au walioshiriki katika harakati hizo, wengine wanaanza kustaaful, wengine wanazeeka, wengine huko mbele ya safari watakufa na hata wale waliokuwepo ndani ya mapambano yale huenda hatutakuwa nao. Sasa katika mtazamo ule ule wa kuendeleza uchumi na kuangalia ile *concept* ya kiuchumi, mimi ningeomba tuenze kujuliza hivi pamoja na

harakati zote za kusaidia mapambano haya, tathmini inaonyeshaje Tanzania, tumeshafanikiwa na tumefaidika kwa kiasi gani katika nchi hizi ambazo tulizisaidia kwa kiasi kikubwa kupata uhuru wake? Ningombwa kujua tathmini hiyo imefanyika na kama hajjafanyika mimi ningombwa ifanyike haraka sana na kama imefanyika nitaomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa ana-*wind up* anieleze ni kwa kiasi gani tumekwisha nufaika kiuchumi kutokana na watu tuliowasaidia katika harakati za ukombozi wa nchi zao?

Mheshimiwa Spika, ulimwengu wa kivita hivi sasa unaangalia uchumi. Mmarekani alipohesabu kuingia Iraq na kazi yote aliyoifanya kumwondoaa Saddam Hussein kwenye madaraka, ameshaanza kujilipa kwa namna moja ama nyingine, analipwa na mafuta yale. Kwa hiyo, *at the end of the day*, utakuta zile *cost* zinarudi zinakuwa *Nil* kwa faida ya nchi yake, makampuni ambayo yanajenga Iraq upya mengi utakuta ni Makampuni yake.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilishtuka juzi wakati Mheshimiwa Rais Nujoma, alipokuwa hapa katika mazungumzo yake na kwa bahati kutokana na wadhifa wangu, nilikuwa na mimi karibu pale. Akasema bwana kule katika nchi yangu mimi nahitaji Tanzania mnilettee bidhaa, nileteeni kila kitu mimi nahitaji mananasi, nahitaji kahawa, which means inaonekana kwamba, pamoja na kazi nzuri tuliyoifanya ya kuwasaidia, Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko anakwenda kwenye masoko ya Asia, anakwenda kwenye masoko ya Marekani, anakwenda kwenye masoko ya Europe, lakini masoko ya Mataifa ambayo tuliwasaidia na ndugu zetu wengine kufariki wakiwa huko, bado kabisa hatujajielekeza kuyaangalia na kuyatumia. Ningombwa hili suala tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kumalizia kabisa, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amezungumza kwamba, wako katika taratibu za kutengeneza Sera ya Taifa ya Ulinzi na bila shaka italetwa. Mimi nafikiri usike wakati wa kuangalia baadhi ya maeneo ambayo tunapaswa kuwa na Sera za Kitaifa, tuwe na *National Policy* ambazo kila Chama ukiacha itikadi pembeni, itabidi hata kikiingia madarakani, lazima kiziheshimu hizo *policy*, tuwe na *policy* za Kitaifa. *Policy* za maeneo ya kiulinzi, *policy* za mambo ya nje, *policy* za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Ulinzi na Usalama, kwa ujumla. Mimi ningombwa ziwe *Policy* za Kitaifa, ambapo tutashirikishwa wote. Ahsante sana. (Makofî)

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru na mimi kwa kupata nafasi ya pili leo, niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kutoa pole kwa sababu ni mara yangu ya pili kuchangia katika kikao chetu hiki. Nafikiri nimebakisha kutoa pole kwa wafiwa wa Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, ambaye alifariki wakati tukiwa katika kipindi hiki cha Bunge. Kwa hiyo, nawomba Wapiga Kura wake na Wananchi kwa ujumla, nawapa pole na wanaone kwamba ni jambo la lazima kutokea, hivyo wawe

wavumilivu na wastahimilivu sana. Namwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya Marehemu peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo na mimi kama kawaida nisipoteze muda mrefu, kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga na Taifa, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Watendaji wake kwa ujumla na Maofisa wote wa Jeshi letu la Ulinzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia mada hii ambayo iko mbele yetu, sina budi kuanza kuyapongeza Majeshi yote, kwa utendaji wao mzuri ambao umetuhakikishia kwamba, tunaishi salama Tanzania. Tunapata muda mzuri wa kufanya shughuli zetu na tunahakikisha tuna usalama katika maisha yetu. Kwa hiyo, nayaomba Majeshi yaendeleee na hali hiyo na nidhamu yao iwe ni mfano kwa raia wema.

Pamoja na kwamba nataka kuchangia lakini nitangulie kusema kwamba, sina dukuduku wala matatizo na hotuba hii na niseme kwamba, hotuba ni nzuri sana, naiunga mkono mia kwa mia. Kwa sababu maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri, mengi yanaonekana kama yamekidhi haja na niseme tu kwamba, tuna haki ya kuikubali na fedha alizoziomba apewe ili ulinzi wetu uimarike. Sasa nichangie katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza nataka sana niendeleee katika nafasi moja ya ushirikiano wa Majeshi. Jeshi letu la Ulinzi na pia Majeshi mengine ambayo tunayo, kwa mfano, kama Polisi na Magereza, kwa sababu nimesema kwamba, sina dukuduku na hotuba hii, nimeona nichangie katika nafasi hii kwa sababu inatukumbusha mbali kabisa. Nikikumbuka kipindi cha vita ambapo ilikuwa ni kipindi cha taharika kubwa sana, Wananchi wetu wengi sana walikuwa na matatizo walihisi kwamba, tunaweza tukavamiwa na tukamalizika Tanzania. Lakini kwa bahati nzuri wakati wa vita vya Nduli Idd Dadaa, tulinusurika na hayo kwa ujasiri mkubwa wa Majeshi yetu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninavyokumbuka kipindi kile Mheshimiwa Marehemu Baba wa Taifa alipotangaza kwamba, “tunayo sababu”, maneno hayo nafikiri Watanzania wote wanayakumbuka hapakuwa na mchezo. Nakumbuka kwamba kila askari wa aina yoyote wa Jeshi lolote alipopewa vifaa alijiona kwamba ni askari sawa sawa na mwenzake mwingine. Waliichukua nafasi hiyo kwa ushirikiano mkubwa sana kuanzia walipotoka majumbani mwao walipofika makambini, walipoingia kwenye vyombo vya usafiri mpaka kufikia kwenye uwanja wa mapambano, Maaskari hao walikuwa na ushirikiano mzuri na ndipo wakaweza kufanikiwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi katika hotuba hii nataka nikumbushie nafasi hii ya ushirikiano baina ya Majeshi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Majeshi mengine. Ningeliomba tukakumbuke hatua hizo tuangalie kutokana na maslahi yao, utendaji wao wa kazi, nyenzo za kufanya kazi zitawasababisha wajione kwamba, wao ni watu wa hali moja na wanafaa kushirikiana. Kwa hiyo, mambo yetu yatakuwa mazuri kwa sababu watakuwa hawana tofauti ndogo ndogo. Kwa hiyo, kwa sababu nina uhakika kabisa kwamba, Waziri wa Ulinzi, Waziri wa Mambo ya Ndani, Maofisa wa Jeshi wa ngazi za juu,

Makamishna wa Polisi, Wakuu wa Vyuo vya Maaskari, wanakuwa na vikao vya pamoja. Ningelipenda katika mikutano yenu mkazungumzia namna ya Maaskari wetu kuwa katika hali ya kupendana na kuona kwamba wana haja ya kufanya kazi katika hali ya kushirikiana. (*Makofi*)

Nimezungumza hivyo kwa sababu naona kuna tofauti ndogo ndogo ambazo hazijaleta athari. Lakini baada ya muda ule upendo ambaao waliutumia wakati wa vita unaweza ukapungua kiasi ambacho itatusababisha mara nyingine kwamba, Mwenyezi Mungu, asijalie vitokee vita, lakini kama vikitokezea kama hawana ushirikiano wanaweza wakabaguana. Sasa naomba katika vikao vyenu mjaribu kulinganisha mambo ya Majeshi haya yanalingana, kuhusu mapato, matumizi yao, kuthaminiana na kuona kwamba wao wote ni Majeshi ya Tanzania na wana haki ya kuweza kufikiriana katika matatizo yao. Nazungumza hili kwa sababu kuna ndugu zetu ambaao wanakuwa katika shughuli zao za kazi, kwa mfano, kama Majeshi, wanapokuwa kidogo wanapitiwa na ubinadamu kufanya makosa yanayoingiliana na mambo ya uaskari, kwa mfano, mambo ya *traffic* au shughuli nyingine zinazoingilia mambo ya ndani, wanaoneshana ubabe. (*Makofi*)

Nafikiri ndugu zangu Maaskari wa Jeshi la Wananchi, mnanisikiliza vizuri, msinitafsiri vibaya. Ni kwamba, ndugu zetu wa Polisi wanapomkuta mtu amefanya makosa mara nyingi wanamsikiliza kwa nini amefanya kosa. Kama amefanya kosa Askari Polisi anayo haki pale pale ulipo kuweza kusema kwamba, usirejee kosa kama hili nenda na safari yako, makosa madogo madogo. Sasa si vizuri unamkuta Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ana kosa tu lakini hawezi kuelewana na mwenzake wa Jeshi la Polisi au Magereza. Kwa hiyo, hili walirekebishe kiasi ambacho isituletee hiyo dhana ya kwamba nani bora katika Majeshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ubora wa mtu ni hekima zake. Vilevile sisemi kwamba Askari Polisi hawana makosa. Maaskari Polisi wanapowakuta wenzao wana makosa madogo madogo, wasichukulie kwamba wao wana ubavu sana wa kuweza kuwanyanya Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Wanapokuta makosa madogo madogo ambayo yamefanywa na vijana wa Jeshi la Wananchi basi waone kwamba wale ni wenzao na wana haki ya kuweza kuwaelimisha kosa ulilofanya bwana lina madhara kwa namna fulani na linaleta sura mbaya kwa ndugu zetu raia.

Kwa hiyo, ni vizuri zaidi Polisi wakawachukulia Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wakawachukulia ndugu zao Askari Polisi kwamba, wao ni askari kama wengine. Hii itatuletea furaha katika kazi zetu na vilevile itatusababishia kwamba, iwapo inatokezea matatizo tutaweza kugawana mkate mdogo au sungura mdogo kama wakati ule ilivyotokea vita kiasi ambapo hapakuwa na mtu anasema kwamba, mimi natoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania, mimi natoka Mgambo, JKT, Magereza au Polisi. Kwa hiyo, wanapokuwa wanakubaliana na hawana uhasama, itatusaidia katika hali ya kuwfanya raia wetu waone Tanzania Jeshi letu ni moja na lina malengo sawa. Mheshimiwa Waziri, nafikiri *message* hiyo imefika na nitakuwa nimeelewaka vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala langu ninalolizungumzia linahusiana na mambo ya michezo katika Majeshi. Muda umeshaanza kunikimbia na inaonekana utakuwa haunitoshi. Ni kwamba, katika suala la michezo nafikiri Waziri akubali kwamba, wanamichezo bora, wazuri wanatokea ndani ya Majeshi. Tukiangalia vilabu vyetu hivi sasa vinaanza kuperomoka nguvu kwa sababu vijana wengi wanapata ajira kwenye Majeshi yetu. Kwa hiyo, kama wanapata ajira kwenye Majeshi yetu, tuhakikishe kwamba, Jeshi letu la Ulinzi lina haki ya kuwatunza vijana hawa amba wanapenda michezo. Sasa napendekeza kwamba, vijana hao wanapofika ndani ya Majeshi yetu basi tuwape kipaumbele katika shughuli zao za kazi na tuone kwamba wanathaminiwa kwa sababu wanatuletea sifa njema Tanzania.

Lakini pia si kuwapa kipaumbele tu, vilevile tuangalie katika maslahi yao. Wanamichezo wanapunjwa sana katika mambo ya kupandishwa vyeo. Kuna Wanajeshi ninaowajua mpaka sasa wana muda mrefu Jeshini lakini wao wanamichezo tu bahati mbaya hawapandi vyeo. Sasa Mheshimiwa Waziri, waangalie watu hawa na hii nasemea katika Majeshi yote. Lakini pia tuwaangalie katika nafasi ya kuwatunza wanapopata matatizo. Kwa mfano, kwenye michezo lazima kuumia kupo. Kama wanaumia basi Wanajeshi au wanamichezo waangaliwe katika hali ya kutunzwa. Wakishapata ajali inakuwa basi hawaangaliwi. Kwa hiyo, tuwaangalie wanapokuwa majumbani kwao, wanapopata ajali kazini wafikiriwe namna ya kuweza kutunzwa wao pamoja na familia zao. Mheshimiwa Waziri, nafikiri katika suala la michezo umenielewa.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kuajiriwa vijana wetu nashukuru sana vijana wetu wanapata ajira sana katika Majeshi kwa sababu ndiyo nafasi ambayo inaaajiri vijana wengi. Kwa hiyo, naomba katika utekelezaji wa ajira tuangalie namna ambayo vijana wanatoka Vijijini. Kwa sababu Vijijini kuna vijana amba wamesoma lakini hawana kazi, matokeo yake nafasi za ajira wanazikosa. Sasa ni vizuri tunapochukua nafasi ya kuajiri tuwachukue pia vijana wanaotoka Vijijini kiasi ambacho kwa upande mmoja muda hautoshi lakini wana masikitiko kiasi ambacho wanapimwa wanaonekana wanafaa, lakini inapofika katika hali ya kozi mara moja utaona anarejeshwa anaambiwa kwamba, aah ulipopimwa hukuonekana kwamba, uko-fit. Sasa ni jambo la ajabu kuonekana kwamba, Zanzibar nzima kuna sehemu ambazo zinaonekana kwamba, kuna nafasi nzuri za kuwapima watu na hospitali zipo lakini ajabu akishika nafasi nyingine unaambiwa kwamba, wako *un-fit*. Kwa hiyo, naomba kwamba nafasi hii katika ajira tuangalie sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho katika vitendea kazi, kambi zetu nyingi za Majeshi hasa Zanzibar ambapo nimejaribu kuziona kama Uyemba, Bububu na ni Makao Makuu ya Jeshi na sehemu nyingine. Wana matatizo ni kwamba, utakuta kuna baadhi ya Majeshi magari yao yanakuwa mabovu sana kiasi ambacho hata ukitaka kuwasaidia mara nyingine unashindwa. Kwa hiyo, tuangalie katika hii ruzuku ambayo inapatikana tujali kwamba wao wanachokizalisha ni usalama wetu.

Sasa Mheshimiwa Waziri, uliangalie suala hilo najua kwamba unajali lakini utililie maanani zaidi magari yao Maaskari mabovu kiasi ambacho mara nyingi magari yao yanakwenda hata *break* hayana, magari ya kijeshi. Wanategemewa sana kiasi

ambacho njiani hawaulizwi. Kwa hiyo, magari yao yawe yanatengenezwa kiasi ambacho hata wanapokutana wakiwasaidia wasiwe na wasi wasi. Kutokana na hatua hiyo ni kwamba, Wanajeshi wanapokuwa na magari mazima basi hata wao tunahakikisha usalama wao. Kumbukumbu zangu zinanionyesha mara moja gari la Jeshi limekwenda kugonga watu wanaokimbiza Mwenge. Kitu hicho kimetusikitisha tumeona kwamba, ilikuwa bahati mbaya. Lakini hatukuonyesha kwamba magari ya Wanajeshi mara nyingi yanakuwa mabovu si kwa sababu wanapenda.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofit*)

**MHE. JINA KHATIB HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia leo nikiwa mwanamke wa kwanza.

Nawaomba wataalamu wasije wakaniona mwanamke mkorofit ni wa kawaida tu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea, naishukuru Wizara yenewe, sina haja ya kutoa rambirambi kwa vile nilishachangia na nilishawapa rambirambi na waliopata maafa nimeshawapa pole vilevile. Kwa hiyo, naipongeza Wizara ya Ulinzi na JKT kwa juhudhi zao walizozifanya. Juhudi yenewe hapo nyuma walikuwa wanaonekana askari wetu wana hali duni, dhaifu na wanyonge. Lakini sasa hivi *alhamdullilah*, tunajikongoja kidogo kidogo. Nikisema tunajikongoja kuna mambo yamenifurahisha ingawa hayanihusu lakini yananihusu kwa kuwa nipo Tanzania hii kuona kila askari amepata *uniform* jozi tatu, ni jambo zuri. Viatu wanavyo, kofia wanazo, sasa hili ni jambo zuri na tunasema tunapiga hatua tusitake twende moja kwa moja wakati mtoto huanza kukaa kitako, hutambaa na kuendelea. Kwa hiyo, nalishukuru Jeshi na Wizara kwa ujumla. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zangu, naendelea na nilichokikusudia. Nilichokikusudia kimo ukurasa wa 47 namba 11 ya Kirumi, Hospitali ya Bububu. Ingawa zimeandikwa ukarabati kwa ujumla wa kambi zote. Kule Zanzibar tuna Hospitali ya Bububu wale wenye Wilaya yao na mkoa wao wasinishangae, ile tunatumia sote imekuwa ni kinyang'anyiro. Hospitali ya Bububu ni hospitali nzuri sana inatusaidia vizuri na hivi sasa naishukuru Wizara, imejenga jengo zuri lakini jengo lile lipo tu halijaezekwa wala halijafanywa chochote. Nilitaka nijue tumekwama wapi? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumepata mashine ya *X-ray* pale Bububu, lakini tangu ilivyopatikana bado haijafungwa mpaka leo. Vilevile nataka tujue tumekwama wapi? Ikiwa tumekwama fedha kidogo leo ndio tunaunga mkono hoja. Kuunga mkono hoja hatuungi mkono hoja kwamba tunapenda, tunaunga mkono hoja ya kwamba nipe nikupe. Tumeiunga mkono hoja kwa nipe nikupe kwamba, hospitali vifaa vifungwe, mabati yaezekwe, tuwe tunakwenda bila ya matatizo na kwa furaha. Ujumbe wa hospitali naona umefika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni usafiri, yaani magari yetu, magari ya Jeshi sio ya raia au la Mbunge. Magari ya Jeshi mengi kama alivyosema Mheshimiwa Ali Machano Mussa, ni machakavu sana. Halafu na jambo lingine unyonge umetushika

lakini tusiukaribishe kama vile tunavyoambizana uzee tusiukaribishe na unyonge tusiukaribishe. Nazungumzia hapo hapo Bububu bado ningali naranda Bububu kama mcheza dansi anaporanda pale pale. (*Makofit/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, siku moja nilienda kumtazama mganjwa wangu Bububu. Kwa bahati kulikuwa na mganjwa taabani alitaka kupelekwa *X-ray*. *X-ray* hapana pale Bububu, gari halina mafuta, sasa tufanye nini. Kwa bahati pana mwanafunzi wangu niliyemsomesha, nikamwambia eeh fulani njoo, akaja, nikamwuliza kwani mna shida gani mbona mmeingia kizaazaa na kizunguzungu, sihusiki lakini niambieni. Aah Mwalimu pana pana, nikatoa bahasha kwenye kipochi, msitangaze shida, shida haitangazwi. Ahsante Mwalimu. Akaenda akatoa yule mganjwa wetu akachukuliwa hanihu wala simjui na kwa bahati akapelekwa hospitali ya Rufaa Mnazimmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kuna ombi lingine katika bajeti hii tuichangie mafuta tuweke katika kifungu cha mafuta mle kwenye vituo muhimu na mwenye shughuli muhimu. Vilevile magari mengi utakapopita Jeshini utayakuta yamepangiwa vigogo. Leo tunaambiwa tuna Nyumbu inatengeneza magari, ningomba hii Nyumbu ianze kutengeneza haya magari machakavu kwanza yaanze kutembea halafu ndio tutafute kipyä.

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja mkoa wangu wa Kusini. Asili ya wivu ni choyo. Tunaoneana wivu kwa choyo. Ukimwona mwenzio anafanyiwa vizuri wewe hufanyiwi vizuri. Katika hotuba Wawi haikutajwa Ubaga wala Dunga, vipi? Sisi tulelewe na nani? Kwa hiyo, Dunga tuna Kambi ya Jeshi, Ubaga kuna Kambi ya Jeshi, vilevile naomba kwa hotuba ijayo izungumzwe. Nikisema hivyo, Dunga nakumbuka Jeshi walipewa eneo kubwa wakati ule mimi nilikuwa mfanyakazi Dunga. Sijui eneo lile limekwenda kwendaje? Kwa sababu sasa hivi katika ziara zangu za mkoa ninapozunguka kuna baadhi ya sehemu naona zinamegwamegwa sijui eneo lile kama hatimiliki wamepata au ndio tena limeisha au sijui vipi kwa sababu naona kuna miembe imeshaanza kubalehe balehe mikubwa mikubwa. Ilikuwa huyu Kiongozi sijui kama ndiyo Brigadia au Jenerali, anisamehe kwa kupotosha cheo chake, kwa sababu nimetokea ualimu na kwingineko. Afuatilie hili suala kwa sababu alipewa eneo kubwa na tulikaa kitako tukalijadili na tukawaita Wananchi tukawaambia halina ruhusa kujengwa. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri haelewi naanza kumzindua na nimemalizia hapo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaiunga mkono hoja hii mia kwa mia au kwa zote au kwa wingi kama mchanga wa Pwani. (*Makofit*)

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumsifu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na msaidizi wake, Mkuu wa Majeshi, Jenerali Waitara. Amani ya nchi yetu iko chini ya Jemadari Mkuu wa Majeshi ya Tanzania, Rais Benjamin William Mkapa, akisaidiwa na Jenerali Waitara, Mkuu wa Majeshi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi ni chombo kizuri, chombo chenye heshima, chombo chenye nidhamu ya hali ya juu na kwa hakika ni mfano wa kutosha kabisa. Nimeshayaona Majeshi mengi, lakini hakika Majeshi yetu nidhamu yake ni ya ajabu sana. Lakini Jeshi letu lazima niseme kwa sauti ndogo kabisa kwamba, mwaka 2000 lilitumiwa vibaya hasa kule kwetu Pemba. Lakini sitaki niseme nini kilitokea kwa sababu yaliyopita si ndwele, tugange yajayo.

Mheshimiwa Spika, ilisemwa juzi hapa Bungeni na Mbunge fulani kwamba, ili CCM ishinde Zanzibar, yahitaji msaada mkubwa kutoka Bara. Si vibaya hata kidogo, ina wajibu hasa Bara kuisaidia Zanzibar CCM ishinde. Lakini msaada huo usiwe katika vyombo vya Ulinzi, Jeshi pamoja na Polisi. Msaada utolewe vya kutosha, wapelekewe fedha nyingi za kampeni, wapelekewe huduma za kila aina za kuwajengea Wananchi barabara, kuwapelekea maji, madawa na Wazanzibar wataamua. Lakini vyombo vyetu vya Ulinzi visitumike.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia kwako, kuomba yafuatayo: Namwomba Mheshimiwa Waziri, ikifika siku ya uchaguzi 2005 ile siku ya kupiga kura, amtake Mkuu wa Majeshi mwenyewe aende Pemba na Unguja na wala asikae Dar es Salaam akasubiri simu, aende mwenyewe Zanzibar.

La pili, vifaru na kwata hizi za Majeshi zisifanywe barabarani. Hizi kwata na vifaru vikae kambini *standby*. Askari wote wa Jeshi wakishapiga kura zao, wakakae kambini wakiwa na sare zao na silaha zao, ndani ya kambi yao wakiwa *standby* wasubiri amri ya Mkuu wa Majeshi wasirande ovyo kupotosha Wananchi.

La mwisho, Mkuu wa Majeshi awe nayo Sheria ya Uchaguzi mkononi mwake. Aisome vizuri na kama endapo patatokea tatizo lolote awe ye ye ameshafika na atazame sheria, je, tatizo lililopo hapa inasemaje sheria na nani anayeipinda sheria? Ikibidi atoe Jeshi lake aje nalo uwanjani. Baada kujua nani amepinda sheria. Kwa sababu mgogoro hauanzi mpaka kuna mmoja amevunja sheria. Masanduku ya kura yahesabiwe kituoni, akitokea mtu akisema aah yakahesabiwe kwa Mkuu wa Wilaya, kwa sheria ipi? Sasa kama vurugu hapo itaanza ye ye awe yupo na ye ye ndiye mtunza amani wa nchi yetu. Aone kwa hili hapana hawa hawana kosa, hawa ndio wenye kosa na hii ifanywe hivi. Asisubiri Dar es Salaam simu kwamba kuna vurugu, kuna nini, halafu akawaleta vijana wetu bure bila sababu za msingi na kusababisha vurugu zaidi.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii ya Bunge lako kuwaambia Wananchi wa Jimbo langu la Chambani kwamba, siwezi kusema hapa Bungeni kwamba, kuna vijana wa vijiweni kutoka Zanzibar wanaopewa mafunzo ya kijeshi katika Kambi za JKT Mgulani na Makutopora, hilo siwezi kulisema hapa. Kwa sababu hamkuniletea ushahidi wa kutosha pindipo nikidaiwa. Kwa hiyo, siwezi kusema neno hilo mbele ya Bunge hili. Walakini kama mna ushahidi nileteneeni. Sidhani hata kidogo kwamba, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, atawenza kukubali kwamba, wachukuliwe vijana waje Bara wafundishwe kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2005. Siamini hata kidogo.

Kama hilo lipo ni kweli ndugu zangu wa Chambani nileteeni kwa maandishi nitamwambia hapa hapa kwa sababu Mheshimiwa Wazri ni mtu msikivu pamoja na Mkuu wa Majeshi. Nataka niwahakikishie kwamba, Mkuu wa Majeshi hii dhana basi ataifanyia kazi, jinsi ninavyomfahamu kwa sababu nilimwona jana jinsi alivyo mkakamavu katika ufunguzi wa nyumba kule Kisasa, kwa hakika haijapata kutokea. Kijana mzuri kama huyu, Rais Benjamin William Mkapa, kumchagua kuwa Mkuu wa Majeshi yetu, hakika mpaka ukipongezwa ni mtu wa aina yangu kwamba, wewe ni mchapakazi, basi kubali kwamba kweli ni mchapakazi. Kwa hiyo, nawathibitishia watu wangu wa Chambani kwamba, hawezi Mkuu wa Majeshi, Bwana Waitara, akakubali neno hili la kijinga lifanyike hasa kwa azma ya uchaguzi, nakwambieni hilo. Lakini kama mna ushahidi ni heri mnilettee.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake aliyoitoa asubuhi hii, kwa kweli inalingana na kufanana na yeze anavyoitwa Profesa.

Vilevile nampongeza Mkuu wa Majeshi, Viongozi mbalimbali ndani ya Wizara na nitakuwa mwizi wa fadhila iwapo sitampongeza Mkuu wangu wa Kikosi cha Twiga Brigedi cha Biharamulo, kwa namna ya pekee kabisa, kwa jinsi anavyoishi pamoja na Wananchi na anavyoiongoza ile kambi kwa namna wanavyoishi maisha mazuri pamoja na Wananchi. Ikumbukwe kwamba, ule mji ni mdogo sana lakini askari walioko pale kwa uongozi wa CO, tunaishi nao maisha mazuri sana. Napenda niwapongeze kwa utaratibu huo. Lakini huo wote ni uongozi thabiti na mwanana wa Profesa ambaye ni Waziri, pamoja na Mkuu wa Majeshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, niende katika hoja yenyewe ni kwamba, matatizo yaliyopo katika Kambi ya Jeshi ya Twiga Brigade ni mengi na ikumbukwe kwamba, kile kikosi cha pale Biharamulo kinafanya kazi nyingi katika historia, kama inavyofahamika kwamba, wakati wa vita ya kumng'oa Nduli Idd Amin pale ndipo ilipokuwa stopover kwa ajili ya askari wetu wapiganaji wetu.

Kulikuwepo na Uwanja wa Ndege ambaa ulikuwa unatumika katika kuhakikisha vifaa vya wapiganaji vinafikia pale. Kwa hiyo, matatizo haya ambayo nayatamka leo, naomba kwa makini na kwa usikivu wa hali ya juu, Mheshimiwa Waziri, ayatilie maanani. Leo katika maneno mengine, natega mtego ili mwaka 2005, Mwenyezi Mungu, akitujaalia kufika, maana hakuna aliyeingia mkataba na Mwenyezi Mungu kwamba, atafika akiwa hai, lakini naweka kumbukumbu, nitapenda mwaka 2005 au kuanzia leo ninapoyatamka, yaanze kushughulikiwa mara moja ili tunapokwenda huko yasitusababishie mtafaruku wa aina yake. Matatizo yanayowasibu wapiganaji, Maaskari pamoja na Maafisa yako katika mafungu yafuatayo:-

Malipo ya kiinua mgongo na fedha za nauli kwa Maaskari pamoja na Maafisa. Maaskari kwa kawaida wanapostaafu wanapaswa wapate haki zao, lakini wanacheleweshwa na wala hawapati fedha za kusafiria kutoka mahali walipostaafia

kurudi makwao. Tunachukulia kama Biharamulo, Wanajeshi anapostaafu anaishi labda katika Kijiji cha Nyakahura, yeche hatapata fedha anazostahili, itabidi aende mpaka Dar es Salaam, anajisafirisha mwenyewe anakwenda kuishi kwa taabu. Kwa hiyo, kwa namna ya pekee, naomba suala hili litiliwe maanani sana, litatuliwe kwa umakini na wakati Wizara inapotatua matatizo ifuate hali halisi ya mahali pale, isitatue tu maadam inatatua matatizo. Jambo lingine ni madai ya fedha za safari ambazo ziko katika mafungu mawili. Fungo la kwanza ni malipo yanayotokana na Askari wanapokuwa kazini.

Kama inavyooleweka, ile Kambi inatoa Maaskari wengi wa kwenda mipakani kule Ngara lakini baada ya kutimiza wajibu wao hawalipwi Askari hawa au wanapokwenda katika kozi mbalimbali, hawalipwi mafao yao. Haya nazungumza kwa kifupi ili Waziri ayachukulie maanani, yafanyiwe utafiti na tathmini ya hali ya juu kwa ajili ya kutatuliwa katika wakati muafaka.

Jambo lingine ni nyumba za kuishi Askari. Ikumbukwe kwamba, nyumba za kuishi Maaskari hawa hazipo katika Wilaya ya Biharamulo. Wanajeshi walio wengi wanapangisha na ukichukulia ile asilimia tatu ya mshahara ambayo ndiyo anatakiwa kupata ili aliye pango la nyumba yake, hii asilimia iko tangu mwaka 1980, kwa nini isibadilishwe? Maisha yanapanda, gharama za kuishi zinapanda. Asilimia tatu kwa mfano, chumba kimoja wanapanga labda kwa Shilingi 10,000/= na wanatakiwa wapange vyumba vitatu waweze kuishi maisha mazuri kwa kuwa wana familia. Sasa Sh. 15,000/= kwa mwezi ina maana unaendelea kumsababishia matatizo na kumfanya awe maskini, atakapostaafu aende kuanza kuhangai. Hiki kiwango cha asilimia tatu ambacho ni cha tangu mwaka 1980, nashauri kiongozwe. Twende na wakati, tuangalie gharama za maisha zinavyopanda. Tusikae na yale maisha ya kizamani. (*Makofii*)

Halafu jambo lingine ni la usafiri. Askari wa Kambi ya *Twiga Brigade* katika Wilaya ya Biharamulo, wanapaswa kusafiri kilomita sita kila siku kutoka majumbani mwao kwenda sehemu yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, labda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu, anawenza akasema kwamba, haya ni mazoezi, hapana. Sisi tunachokizungumzia hapa ni *efficiency*. Mtu kusafiri kila siku Kilometra sita, kama kweli ana malengo kwamba anakwenda kufanya kazi, kuna jambo maalum analokwenda kulifanya na akaenda akafika akiwa amechelewa, basi hapo hujamsaidia kitu chochote. Naomba kwa namna ya pekee kabisa, gari lipatikane la kuwasafirisha Askari wetu kutoka majumbani kwenda kazini na kurudi. Ukifika pale Biharamulo, utawahurumia Wanajeshi kwa sababu wanaomba mara magari ya raia, kama unavyojoua magari ya raia yaliyo mengi yanakuwa yamejaza, kwa hiyo, ni kuwdhalilisha kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, naomba gari lipatikane la kuwasafirisha kutoka majumbani kwenda kazini.

Vilevile kama wakipatikana wagonjwa, ni kwa bahati mbaya sana pale Biharamulo, hospitali yao ipo pale pale, lazima wasafirishwe wagonjwa kutoka mahali walipo kwa kilometra sita. Hakuna gari la wagonjwa na ifahamike pale Biharamulo, Askari wanapokuwa wanatoka huko mipakani, wengine wanaumwa, wana matatizo mbalimbali, kuja kufikishwa hospitali na kwa kutumia magari ya kuombaomba, hili

jambo ni aibu na kwa kweli lazima tulitilie maanani kuhakikisha kwamba, gari la wagonjwa linapatikana. Kama kwenye kitabu cha Waziri alivyozungumzia kuhusu suala la kupatikana magari ya wagonjwa, Biharamulo nayo ipewe kipaumbele kwa ajili ya kupata hilo gari la wagonjwa. Vilevile huduma ya tiba. Madawa yanayopelekwa pale ni kidogo mno. Isitoshe ile Hospitali kwa bahati nzuri inahudumia hatatwenyeji wanaoishi kandokando ya ile Kambi. Kwa hiyo, madawa ni machache, hayatoshi kwa kuwahudumia wagonjwa wanaopatikana au wanaofikia hatua ya kuwa mahututi, wanapofika kule huwa hawapati huduma wanayostahili.

Jambo lingine, hebu tuangalie na kuchunguza kwa makini Maaskari wanaokwenda kufanya kazi mipakani. Ile Kambi ndio inayotoa Askari wa kwenda mipakani kwa ajili ya kulinda mipaka yetu ya kule Ngara na kwingineko. Maaskari ambao wanakwenda kule wanaishi katika mazingira magamu.

Mheshimiwa Spika, nafahamu Mheshimiwa Waziri yuko peke yake katika Wizara hiyo. Serikali inapaswa kuelewa kwamba, Waziri huyu ni Waziri ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika maneno mengine, ana mambo mawili katika Wizara moja. Mimi napendekeza Serikali imwekee Naibu. Kwa sababu mambo yanayofanyika yaliyo mengi, napenda niseme kabisa kwa uwazi kwamba, hayafahamiki. Maana yake leo yuko kwenye Ulinzi, mara Jeshi la Kujenga Taifa, sijui kama anaweza akawajibika na hii Serikali lazima ilitilie maanani kwamba, Wizara hii inapaswa kuwa na Mawaziri wawili. Sijipigii debe, baadhi ya watu wanaweza wakasema ooh, sifanyi kitu kama hicho. Najua kwamba, Mwenyezi Mungu, ndiye anayegawa vyeo. Kwa hiyo, nasema Wizara hii ili ihakikishe inafanya kazi ipasavyo, lazima iwe na Mawaziri wawili, mmoja ashughulikie masuala la JKT na mwagine ashughulikie masuala ya Ulinzi, kwa sababu sasa hivi shughuli zinavyofanyika nyingi sana hazieleweki. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara hii ipewe Mawaziri wawili.

Kuhusu kiwanda cha Nyumbu, nilikuwa napiga mahesabu kwamba Shilingi milioni 950 ukizigawa kwa magari 21 unapata kila gari liligharamu Shilingi milioni 45. Sasa nikajiuliza kwamba, haya magari kweli yana thamani ya Shilingi milioni 45? Thamani, halisi ya gari. Naomba hiki kiwanda kifanyiwe utafiti wa hali ya juu, kuja na tathmini ambayo itakuwa ni gharama ya kukiwezesha hiki kiwanda kifanyiwe kazi kwa faida. Kwa utaratibu huu pesa zinavyokuwa zinatolewa kama shilingi milioni 950 ina maana ukichukua shilingi milioni 45 ukaenda kununua gari ambalo limetengenezwa kwa umadhubuti wa hali ya juu, hivi hili gari ambalo limetengenezwa kwa shilingi milioni 45 kwa Tanzania na gari ambalo litakuwa limetengenezwa kwa shilingi milioni 45 kwa Wajapan, ile *lifespan* yake vitalingana?

Kwa hiyo, nilikuwa naomba, kinachotakiwa hapa ni kuhakikisha kiwanda hiki kinafanya kazi kwa faida. Wanasema mara kwa mara kule Jeshini kwetu, zamani kulikuwa na matatizo madogo madogo ya mwanajeshi na mwananchi wa kawaida na jamaa mwagine kukwaruzana. Sasa kitu ambacho nilikuwa naomba niwajulishe Watanzania kwa ujumla, Wanajeshi, Askari Polisi na Askari Magereza kwamba, ili tuishi kwa pamoja, tuvumiliane, tuelewane tukielewa kwamba, hii nchi ni yetu, hakuna haja ya kukwaruzana. Naomba niwajulishe msemo ufuatao, wanasema: “*To live in the society*

*doesn't mean simply living side by side with others in a more or less close cohesion. It means living through one another and for one another."* Kwa hiyo, naomba tuvumiliane machafuko yasiwepo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu hoja ya Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwanza kabisa, ningependa kumshukuru Waziri na wataalam wake katika Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza Wizara hii. Katika gazeti la leo nimesoma jambo ambalo mimi nimeona sio la kawaida, nadhani ni vizuri tuenze kulikemea pia. Inapoandikwa kwamba, Rais anaomba asilaumiwe kwa kumsifu Waziri fulani, wanaoandika hivi wanakosea vilevile, kwa sababu gani? Rais ndio ameunda Serikali na ndio mwenye haki ya kutambua Mawaziri wake wanaofanya kazi vizuri, kwa nini watu wamsakame? Sasa nashangaa katika nchi hii, Rais akimsifu mtu inakuwa nongwa! Kwa nini? Nongwa inakujaje wakati Rais ndiye anayepima ufanisi wa wale alioamini kuwapa kazi? Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa moyo wa dhati kabisa, kwa sifa alizozitoa jana kwa Waziri wa Ujenzi na wenzake na leo tunarudia kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa vilevile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, nilikuwa nataka nisaidie kutoa maelezo kidogo. Mheshimiwa Karim Said Othman, amempa kazi Mkuu wa Majeshi ambayo siyo yake. Kazi aliyokuwa anaizungumza ya kwenda kusimamia ulinzi wakati wa Uchaguzi ni kazi ya Mahita, sio kazi ya Mkuu wa Majeshi kwa sababu yeye kazi yake ni kulinda mipaka ya nchi na Tanzania haina vita na wala Uchaguzi wetu sio vita. Uchaguzi ni *process* ya kidemokrasia ambayo inapofanyika ni lazima ifanyike chini ya amani na watakaofanya kazi hiyo, wanajulikana. Lakini vilevile kwa nini tunaanza kuwa na hisia za uwoga? Hata hao Polisi nani kasema ndio itakuwa kazi yao? Kwa hiyo nadhani lazima tukomae kisiasa na kuelewa. Lakini naomba Waheshimiwa Wabunge, mliomsikia mwenzetu, msimshangae kwa sababu yeye mwenyewe ndio Kamanda wa *Brigade* ya *CUF*, yule Msemaji ndio Kamanda wa *Brigade* ya *CUF*. Wamejanzishia kazi ambayo vilevile sio yao, ndio maana wana wasiwasi. Kwa hiyo, nataka jambo hili lieleweke hapa Bungeni. (*Kicheko/Makofi*)

Baada ya hayo nilikuwa na mambo matatu tu. La kwanza, nilikuwa nataka kuzungumza habari ya uzalishaji. Katika hali ya kawaida katika nchi za wenzetu kunapokuwa na utulivu kama ulivyo katika nchi yetu, kulilisha Jeshi la Ulinzi ni gharama. Lakini katika Majeshi yetu haya ya Ulinzi ndiko kuna ujuzi wa kila aina. Ndio maana utaona wao wenyewe ni Madaktari na wana Hospitali nzuri sana ya kisasa na watu wengi wanaokwenda kule kutibiwa wanapona. Sasa ile Hospitali vilevile inaweza ikawa ni ya huduma kwa Jeshi, lakini vilevile ikawa mradi wa kusaidia kuongeza mapato kwa kutibu na kutoza pesa. Pia katika nchi nyngine, nitatoa mfano mmoja wa nchi ambayo nimekwenda kama India. India, Jeshi ndilo linalokuwa na mashamba makubwa ya

kulima, ndio ina ma-ranch makubwa ya kufuga kwa sababu hawa watu wana utaalam wa kila aina. Inapotokea hata hapa Tanzania madaraja yakiharibika, tukipata maafa, watu wanaokuwa mstari wa mbele kufanya kazi hizo ni Majeshi yetu. Sasa nilikuwa nafikiria kwamba, kazi za uzalishaji mali na kupewa ukandarasi wa miradi mikubwa ya madaraja nao wawemo ili kuongeza pato la Jeshi kwa sababu wana ujuzi ambao hautumiki. Hatuko vitani wakati huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafurahi sana kwamba, Jeshi letu upande wa JKT, wana miradi mingi mizuri na vilevile kazi hii ya ujenzi wa nyumba tulizoona jana ni miongan mwao. Kwa hiyo, natoa pongezi kwa kazi nzuri ambayo tunaiona na ninadhani tungeweza kuwapa zaidi na zaidi ili waweze kujitegemea katika mambo haya.

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine ambalo naomba nilieleze bila kulionea haya. Ni hivi, Benki ya Dunia inatumiwa na wakubwa kusema kwamba, nchi zilizoendelea watumie *resources* zao kidogo walizonazo kwa ajili ya huduma za jamii na maendeleo ya nchi zao lakini wasinunue silaha. Lakini nchi hizo hizo zilizoiagiza Benki Kuu ziweke kiwazo hicho ndio wakubwa wa kutengeneza silaha za kisasa duniani ili kuwapiga watu wadogo na ndio wauzaji wakubwa wa silaha. Sasa haki iko wapi? *Justification* iko wapi? Wanazuia silaha zisiuzwe lakini ndio watengenezaji na wauzaji wakubwa na wakijua nchi fulani ya Kiafrika au nchi fulani inayoendelea haiptanii na jirani yake, watamwuzia silaha yule wanayempenda. Hata hapa katika kada yetu kuna watu wana silaha zaidi kuliko wenza na wanauziwa na hao hao na nyingine wanapewa bure kwa sababu walishawafanya baadhi ya Viongozi wa Afrika kuwa wakubwa zao ni Wajomba wao. Mambo haya yanatokea sasa kwa sababu mkubwa amebakia mmoja duniani hakuna ushindani. Kwa hiyo, anafanya anavyotaka Marekani. (*Makofi*)

Sasa Marekani haki iko wapi kuitumia Benki hii kuweka masharti kwa nchi nyingine wasinunue silaha na nyingine ziendelee kununua silaha? Wakubwa hawa, nataka kusema kwa roho moja tu, wala ugomvi unaotokea katika nchi zinazoendelea, kwao sio tatizo, ni furaha! Kwa sababu kwanza, wanapenda waje kutupatanisha kuonyesha sisi ni watu wa ovyo miaka yote na kugombana kwetu ndio fahari yao. Kwa hiyo, nataka niseme katika jambo hili, hakuna haki. Kama sisi tuna dhahabu yetu, tukitaka kununua silaha za kujilinda sisi hatutaki kupigana vita. Tanzania hata tulipopigana vita na Uganda tulichokozwa na tukashinda na imetuwekea heshima ya historia. Kwa hiyo, kama kuna nchi inaweza, waachiwe maana wanamzuia mwingine na mwingine wanakuruhusu. Kwa hiyo, katika jambo hili hakuna haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi moja inapoichokoza nchi nyingine, mara nyingine inatumwa na wakubwa kwamba, mtukaneni yule ili mgombane tuwasaidie. Hayo sisi tunayajua na wala sio siri. Kwa hiyo, jambo hili nadhani sio haki hata kidogo.

Halafu jambo lingine ambalo ningependa kulisema ni kuhusu utundu huu ambao unafanyika Nyumbu. Mimi nafikiri kwa kuanzia ingefaa tuwapongeze. Kule kwa Mao Setung wakati ule wataalam wake Wachina walipoanza utundu wa kutengeneza zana za kilimo walianza na trekta. Lile trekta lilipotengenezwa badala ya kwenda mbele lilitrudia nyuma, *reverse*. Mao akaita Mkutano na akawapongeza na Chama chao kikatoa pongezi

maalum kwa watundu wale walioanza kutengeneza trekta likarudi nyuma. Alisema hili trekta limerudi nyuma, lakini kesho litakwenda mbele. Kwa hiyo na mimi nasema tungewapongeza hawa, tuwasaidie namna ya kuongeza zana hii na kwenye *process* haya mambo yatakuwa mazuri na *commercial costing* zitaanza kufanyika sasa maana hatukuwa na kitu. Huwezi kuanza kuzungumzia *economics* ya gari moja wakati hata hunalo na uwezo wako wa kutengeneza mengi sio mkubwa. Kwa hiyo, nadhani tuwapongeze kwa hatua hii ambayo tulikuwa tumeshuhudia hapo nje. (*Makofi*)

La mwisho ambalo ningependa kulisema, hili ni la jumla kwa Wizara zote. Mimi nafurahia sana juhudhi hii tunayoifanya ya kampeni ya madhara ya ugonjwa huu wa Ukimwi. Lakini nadhani ingekuwa vizuri kama Tume ya Ukimwi ndio ingechukua jukumu la kutengeneza utaratibu na aina ya matangazo yatakayosaidia kampeni ya kusaidia kuzuia Ukimwi. Kwa sababu tumeachia wafanyabiashara watangaze Ukimwi kwa namna wanavyotaka. Mimi mtu akiniuliza haya ninayoona kila siku wanasema soo, sijui usichelewe sijui wahi, hiyo ni biashara tu! Haina tishio lolote kwa mtu kuweza kuogopa Ukimwi kwa sababu wale ni wacheza *dance*. Wanacheza *dance*, wanakatika viuno halafu wanasema usione soo. Usione soo ni nini!

**MBUNGE FULANI:** Sema naye! (*Kicheko*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Sema naye! Sasa maana yake nini? Sio tishio lile! Ni maneno ya kutongozana kwenye Televisheni. Sasa Hatuwezi kuachia hiki kitu *serious* kama ugonjwa wa Ukimwi ukawa ni biashara ya kuuza kondom. Maana ujumbe pale, nunua kondom. Ndio ujumbe! Wala usiogope Ukimwi, lakini ukichelewa kusema naye, tumia kondom. Kwa hiyo, hakuna tishio pale ni biashara tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa nasema, jambo kubwa kama hili ni kosa nchi kuachia wafanyabiashara kutangaza jambo kama hili. Naomba Serikali yenewe ichukue jukumu na vyombo, Taasisi na wafanyabiashara wote, wanaopenda kuisaidia nchi, watumie matangazo yatakayokuwa *designed* na kutengenezwa na Serikali yenewe. Hapana kuachia wafanyabiashara, jambo hili ni hatari sana! Mimi sijaona kwenye televisheni hiyo ya soo, usichelewe, kuna mtu amekufa na Ukimwi au aliyekonda mbavu. Wanakuja walionenepa, wamependeza, ndio wanatuchezza pale usione soo. Mgonjwa wa Ukimwi yuko wapi pale? Sasa jambo hili ni hatari sana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Bajeti ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabisa, naomba niweke msimamo wangu kwamba, naunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nimpungeze Mheshimiwa Waziri na timu yake, Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Makamanda wote, kwanza, kwa hiyo hotuba ambayo Waziri ameiwasilisha hapa, lakini na kwa kazi za dhahiri ambazo tunazona zinafanyika huko uraiani na katika Kambi zetu za Jeshi kutokana na Bajeti ambayo tunapitisha au tunazipitisha katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kitu kimoja ambacho nadhani kinatutia matumaini makubwa ni kwamba, tunaanza kuona kunakuwepo na ile *value for money* kwamba, utoaji wa fedha baada ya Bajeti ni kitu ambacho kimekuwepo kwa miaka mingi kwenye Serikali. Lakini je, kazi ambazo zilikuwa zikikusudiwa kufanywa baada ya Bajeti hizi kuitishwa zimekuwa zikifanyika? Hili ndilo limekuwa tatizo kwenye Bajeti katika Serikali yetu kwa muda mrefu sana. Lakini leo tunashuhudia pamoja na Bajeti ndogo ambayo tunaitoa kwa baadhi ya Wizara ikiwemo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tunaona kuna kazi zinafanyika. Tunasema hivyo kwa sababu ukisoma taarifa ya Waziri, ahadi alizokuwa ameahidi kutekeleza kwa kipindi cha fedha cha 2003/2004 ahadi hiso kwa kiasi kikubwa zimetekelawa. Kwa hiyo, nampongeza sana Waziri na timu yake. Lakini pia nampongeza Waziri kwamba, kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2003/2004, aliahidi kukamilisha ujenzi wa nyumba za Kikosi cha Jeshi pale Makoko. Nyumba hizi zilijengwa kisha yule Mkandarasi akakimbia miaka zaidi ya kumi nadhani. Lakini hatimaye sasa ninafurahi kwamba, ahadi ambayo ilitolewa na Wizara imeanza kutekelezwala na kweli kazi hii ya kukamilisha nyumba zile sasa inafanyika. Nawashukuru sana kwa hilo. (*Makofî*)

Lakini pia napenda nishukuru kwamba, kulikuwa na tatizo la maji kwenye Kambi ya Jeshi Makoko kwenye Jimbo langu la Musoma na nishukuru kwamba, huduma hii ya maji sasa imeanza kupatikana. Pamoja na kwamba kazi inaendelea kukamilika, lakini nishukuru pia kwa hilo kwamba ahadi ambazo nilikuwa nimeahidiwa na Wizara hii kwa mwaka uliopita zimetekelawa kwa kiasi kikubwa na kwa sababu hiyo kwa kweli sikuwa na sababu ya kutokuiunga mkono hoja hii na ndio maana nasema naiunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hii inatufundisha nini? Haimaanishi kwamba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa walikuwa hawapewi fedha siku za nyuma. Fedha zilikuwa zinatolewa, lakini inaonyesha kwamba, kulikuwa na kapu ambalo lilikuwa linavuja kwa siku za nyuma. Sasa kapu lile limezibwa na fedha hizi sasa tunaanza kuona zinakwenda kwenye malengo yaliyokusudiwa.

Kwa hiyo, napenda niupongeze sana Uongozi wa Jeshi chini ya Mheshimiwa Waziri na Mkuu wa Majeshi kwamba, kwa kweli wanatia moyo na tunataka watu wengine waige mfano kwamba, tunaweza kuzuia rushwa katika maeneo yetu kwa kuiga mfano wa Jeshi kwa sasa hivi kwa sababu hizi hatua ambazo zinachukuliwa na Wizara ya Ulinzi, fedha tunazowapa ni ndogo lakini tunaona kabisa kwamba, pamoja na ufinyu wa Bajeti, kuna kazi inafanyika. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hilo. (*Makofî*)

Nilipenda niongelee suala la ajira kwa vijana, maana kwenye hotuba ya mwaka 2003, nilizungumzia pia kwamba, bado tunaweza kutumia Jeshi la Kujenga Taifa

kupunguza sana tatizo la ajira kwa vijana wetu. Nilikuwa nadhani bado kuna umuhimu wa kuangalia upya ni namna gani tunaweza kuwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuitia kwenye muundo mpya uliopo sasa hivi kwamba idadi ya vijana waliojiunga na Jeshi iweze kuongezwa na nyenzo ambazo Jeshi la Kujenga Taifa wanapatiwa kwa ajili ya mafunzo stadi wanayotoa kwa vijana hawa kwa maana ya Bajeti waweze kuongezewa ili angalau vijana wengi ambao wamemaliza Darasa la Saba na Darasa la 12, waweze kupita ndani ya Jeshi hili waweze kupata mafunzo ya ufundi stadi ambayo yatawawezesha kupata ajira kwenye sekta binafsi.

Kwa sababu tunapozungumzia kwamba, tutaondoa tatizo au kupunguza tatizo la ajira ya vijana bila kuangalia namna gani tunawezesha hao vijana kupata ujuzi au utaalam fulani, bado naona ni ndoto ambayo haitatimia. Lakini nadhani kwa kutumia Jeshi la Kujenga Taifa, tunaweza bado vijana wetu wengi tukawasaidia kuitia kwenye huu utaratibu wa sasa hivi wakaweza kupata mafunzo ya ufundi stadi na wakaweza baadaye kujiajiri.

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna umuhimu wa Serikali, Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuwa na mkakati wa pamoja kuhusu tatizo hili la ajira ya vijana na kuwa na mpango maalum ambao unawenza kutusaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana.

Leo nadhani wengi wetu tumefurahi baada ya kuona magari hapo nje. Mwaka 2003 pia katika kuchangia nilizingumzia suala la NYUMBU. Inachekesha kama tutawalaumu au tutashindwa kuwapongeza wenzetu wa NYUMBU kwa hicho walichokifanya kwa kutokujua kwamba hata hiyo bajeti ambayo tunawapa NYUMBU kwa ajili ya kufanya hiyo bado ni bajeti ambayo ni ndogo sana. Kwa sababu hapa tunazungumzia *investment* ya shilingi milioni 300. Shilingi milioni 300 ukimwambia mtu kwamba una-*invest* kwenye teknolojia kwa shilingi milioni 300 ambazo ni sawasawa na dola laki tatu, ni mzaha mkubwa sana huu. Kwa hiyo, mimi nadhani Serikali kama ipo *serious* kwenye kuwekeza kwenye Jeshi na upande wa kuimarisha teknolojia kwenye hii Taasisi ya NYUMBU, tungealia upya namna gani tunaweza kuwa hata na *special package* kwa ajili ya kuwasaidia watu wa NYUMBU. Hatuwezi kukwepa kwamba gharama za uzalishaji ni lazima ziwe kubwa kwa sababu *unit* ambazo zinazalishwa pale NYUMBU ni ndogo. Kwa hiyo, ukifanya hesabu yoyote inakuambia tu kwamba, kwa sababu kiwango cha kuzalisha ni kidogo lazima gharama za uzalishaji zitakuwa kubwa. Lakini tukiwawezesha tukawapa fedha za kutosha, wakafanya utafiti wa kutosha, wakawa na kiwango kikubwa cha kuzalisha, watapunguza gharama za kuzalisha na hata gharama hiyo ya *unit* moja itakuwa iko chini kuliko hii ambayo tunaambiwa leo kwenye bajeti ambayo wanatusomea hapa.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, bado hatujawekeza kiasi cha kutosha kwenye teknolojia na tunesema kwamba kama alivyozungumza msemaji mmoja hapa, nchi nyingine zimewekeza kwenye majeshi. Maana yake huku kwenye majeshi ndiko ambako tuna *cream* ya Watanzania ambao kwa kweli wanaweza kutusaidia kufanya utafiti na wakatusaidia kabisa kutoka katika hatua tuliyoko kwenda mbele zaidi. Lakini hatuwezi kuzungumzia suala la utafiti kwa bajeti ambayo ni ndogo kiasi hiki

kwamba, tunazungumzia bajeti ya utafiti ambayo ni shilingi milioni 300. Sasa shilingi milioni 300 ni asilimia ngapi ya bajeti nzima ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa?

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiangalia bajeti ya Serikali, fedha zinazokwenda kwenye utafiti hazizidi asilimia mbili ya bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, hii bado haitusaidii sana maana sasa hivi kwenye mabadiliko haya ya Sayansi na Teknolojia, hatuwezi kutoka kwenye hatua tuliyopo kwenda kwenye hatua nyingine bila kuwekeza kwenye sayansi na teknolojia, kwenye *research*. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, kuna umuhimu kabisa wa Serikali kuangalia ni jinsi gani itatenga fedha za kutosha kuwawezesha ndugu zetu hawa wa NYUMBU kuweza kuzalisha zaidi ya hapa walipofikia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilitaka nichangie kwenye bajeti hii ya Ulinzi na Jeshi na Kujenga Taifa ni kwa upande wa MEREMETA. Nilikuwa nasoma hapa shughuli za MAREMETA mchango wake. Naomba niseme kwamba, shirika hili limefanya kazi nzuri, lakini nilikuwa nashangaa tu kwamba, gharama za uendeshaji ziko juu sana. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, hili lingeangaliwa upya kwamba angalau mradi huu basi ungeweza kuwa na faida kubwa kuliko ilivyo hivi sasa kwa maana ya kupunguza hizo gharama za uendeshaji. Lakini lingine ni kwamba, pale kulikuwa na dispensary na pale Buhemba kulikuwa pia na shule ya msingi na nakumbuka nilipofanya ziara na Mbunge mwenzangu, Mbunge wa Musoma Vijijini na moja ya ahadi ya wale wawekezaji ni kwamba, wangeweza kurejesha zile huduma za shule ya msingi, pamoja na Kituo cha Afya.

Katika haya ambayo yamefanywa pale sijaona hilo nimeona tu kwamba, imejengwa Shule ya Sekondari ya Butiama. Lakini kile kituo cha Afya ambacho kilikuwepo sina uhakika kama kimejengwa na kama kitakuwa kimejengwa basi ninshukuru. Lakini kwa ile Shule wanafunzi wengi walihamishiwa kwenye shule za jirani. Lakini kama ilikuwa ni ahadi basi Mheshimiwa Waziri, liangalie hilo kwamba katika kujenga mahusiano na wale wenyeji wa eneo lile la Buhemba, kuwepo na utaratibu wa kurejesha huduma ile ya shule pale Buhemba.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kabisa, ni kuhusu *recruitment* ya hawa vijana wanaoingia jeshi na JKT. Naomba niseme wazi kwamba, utaratibu ulioko sasa hivi si kwamba ni mbaya sana, lakini nadhani utaratibu huu ungeimarishwa ukawa *more transparent* kuwawezesha Wananchi wengi kupata taarifa za nafasi za ajira katika jeshi na nafasi hizi za kujiunga na mafunzo haya ya muda mfupi ya *national service*. Nasema hivi kwa sababu unaweza kukuta Wananchi wachache au wazazi wachache au vijana wachache, ambao wanapata taarifa za nafasi hizi za jeshi zinapotokea. Mara nyingi watu wanakuja kupata taarifa wakati watu wamekwishafanyiwa usaili, wamekwisha safiri kwenda kwenye kozi. Kwa hiyo, tunabaki na lawama za hapa na pale kwamba, labda kuna upendeleo fulani ambao labda unafanyika kwa wale viongozi ambao wamepewa dhamana hiyo ya kusimamia usajili au *registration* ya hao vijana. Kwa hiyo, nilichokuwa naomba ni kwamba, Wizara ingeangalia utaratibu ambao utawezesha tarifa hizi kuwafikia Wananchi wengi, hasa kwa kupitia kwenye redio na hata kupitia kwenye

magazeti kwamba kila mkoa, kila Wilaya iweze kupata taarifa kwamba, kuna nafasi za jeshi zimetolewa, kuna nafasi za Jeshi la Kujenga Taifa zimetolewa. Wananchi wengi zaidi waweze kupata taarifa hizi na kuwawezesha kupata hiyo nafasi ya kuweza kuomba nafasi hizo kulingana na sifa walizonazo.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana, lakini pia niishukuru Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kukamilisha ahadi ambazo walinipa kwenye kipindi cha bajeti kilichokwisha, isipokuwa tu niombe kwamba, tuna tatizo la usafiri pale kwenye Kambi ya Makoko na nina hakika tatizo la usafiri kwa jeshi, vikosi vingi vina matatizo ya magari. Lakini nina hakika kuna utaratibu ambao unafanyika, basi niombe na Kikosi cha Makoko kiweze kufikiriwa pale ambapo magari yatakuwa yamepatikana kwa ajili ya usafiri wa wapiganaji wa kikosi kile.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. SUMRI A. S. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa nafasi hii ulionipa niweze kuchangia katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, binafsi napenda kutoa pole nyingi kwa ndugu zetu tuliopotelewa hivi karibuni. Mpendwa wetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, vile vile kwa Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki. Pole nyingi kwa ndugu zetu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda. Mola aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, azifikishe salamu zetu za Wananchi wa Mpanda Magharibi za kumpa pole Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin Wiliam Mkapa, kwa maumivu aliyoyapata. Wananchi wetu wapo pamoja na ye ye na wamenituma nizifikishe salamu hizi kama Amiri Jeshi Mkuu wetu kwa kupitia kwako. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika eneo letu la Jimbo la Mpanda Magharibi kule mpakani mwa Ziwa Tanganyika kati yetu na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia na Burundi. Eneo langu la Ikola, Karema, Kasangatongwe, Kaselamiaga na Lwega ni maeneo yanayoshambuliwa mara kwa mara na wezi wa majini.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri iliyofanywa na Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania haitasahaulika. Napenda nizifikishe salamu za Wananchi wangu na pia kwa kutaja orodha ya kazi nzuri iliyofanywa na wanajeshi hawa katika eneo langu tangu walipoanza kufanya kazi hiyo kando ya ziwa. Ujambazi ulioripotiwa mwambao mwa Ziwa Tanganyika kwa mwaka 2000 hadi Mei, 2004, matukio yaliyoripotiwa ni 14. Watu waliotekwa ni 46, waliorudi salama ni 32. Watu waliouawa kwa kupigwa risasi ni wanne. Watu 10 hawajulikani walipo hadi sasa. Mali zilizoporwa ni nyavu 11. Karabai

zaidi ya nne na bidhaa za dukani mbalimbali. Jumla ya thamani ya mali zote zilizoporwa inakaribia shilingi milioni mia moja. Ziliripotiwa ni shilingi 87,285,500. Tarehe 4 Juni, 2000 majambazi wanne wenyе silaha za *SMG* walipora nyavu moja bila kuua, yenye thamani ya shilingi 145,000/=. Tarehe 4 Juni, 2000 majambazi hao hao walipora nyavu moja na vitu mbalimbali nyumbani kwa watu bila kuua vyenye thamani ya shilingi 717,000/=. Tarehe 19 Juni, 2000 majambazi walipora mali za duka bila kuua wala kuteka na thamani ya vitu haikujulikana.

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Novemba, 2002 majambazi wenyе silaha aina ya *SMG* walipora fedha shilingi 66,000/= bila ya kuua. Tarehe 30 Novemba, 2002 majambazi hao walipora shilingi 15,000/= bila kuteka wala kuua. Tarehe 7 Machi, 2003 majambazi wasiojulikana idadi wakiwa na *SMG* walipora wavu mmoja, karabai nne, kamba za uvuvi nne, vyote vikiwa na thamani ya shilingi 705,000/=. Tarehe 7 Machi, 2003 huko Kasangatongwe, majambazi walipora mali za duka na vitu mbalimbali majumbani kwa watu zenye thamani ya shilingi 1,536,000/= na kuteka watu watano ambao hadi sasa hawajulikani walipo. Tarehe 27 Machi, 2003 majambazi watatu wakiwa na *SMG* walijaribu kuteka boti, waliposhindwa walimwua mwanamke mmoja kwa risasi na kumjeruhi mwanamme mmoja na kutoweka. Tarehe 3 Agosti, 2003 majambazi kadhaa walipora begi la nguo, redio moja, mtumbwi mmoja, bila kuteka wala kuua, vyote vikiwa na thamani ya shilingi 129,000/=.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Desemba, 2003 majambazi wanne wenyе *SMG* tatu walipora nyavu mbili, mtumbwi mmoja, kuteka watu sita na kuua mmoja. Mateka watano walirudi salama kwa msaada wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Thamani ya mali haikufahamika. Tarehe 20 Desemba, 2003 majambazi walipora nyavu moja na vifaa vya nyumbani na mali za dukani vyote vikiwa na thamani ya shilingi milioni moja na nusu. Watu sita walitekwa na baadaye walirudishwa kwa msaada wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Tarehe 13 Februari, 2004 huko Ruwega-Ikola majambazi wasiofahamika idadi yao walipora nyavu moja na vifaa mbalimbali majumbani mwa watu vifaa vyenye thamani ya shilingi 1,700,015/= na kuteka watu watano na hadi sasa hawafahamika walipo. Tarehe 1 Machi, 2004 majambazi wasiofahamika idadi, walipora nyavu mbili, mtumbwi mmoja, vyote vikiwa na thamani ya shilingi milioni moja na nusu na kuteka watu 11, kuua mmoja kati ya hao mateka na kuacha 10 salama. Tarehe 11 Mei, 2004 majambazi watano wenyе silaha za *SMG* mbili walipora nyavu mbili na bidhaa mbalimbali zenye thamani ya shilingi 600,000/= na kuteka watu 12 na kuua mmoja kati ya mateka hao na kuwaacha mateka 11 salama. Baada ya kuokolewa na askari wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, pamoja na Wananchi na kufanikiwa kuuawa kwa majambazi hao wanne na kukamata *SMG* mbili zikiwa na *magazine* nne bila ya risasi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, kwa haya yote, napenda kuwapa pongezi Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi nzuri waliyonayo katika mipaka yetu. Pamoja na hayo, bado tuna matatizo ya vitendea kazi kwa jeshi letu lililopo hapo Ikola, kikiwa kikosi kidogo tulichosaidiwa kutoka Mbeya. Jeshi hilo hawana vitendea kazi vya kutosha kwa maana gari wanilotumia mpaka sasa halina hali nzuri. Vilevile hawana fungu zuri la kutumia kwa ajili ya mafuta, vipuri, tulikuwa tunaomba misaada kutoka kwako

Mheshimiwa Waziri ili kulifanya jeshi hili liwe jeshi imara. Jeshi lenye kucha ni mwenye kucha na meno awezae kufanya kazi yake kwa kutumia viungo vyake kweli kweli bila kuomba msaada kutoka maeneo ya watu wengine. Orodha niliyonayo kutoka Kambi ya Jeshi huko Ikola ni kwamba mahitaji ya mafuta kwa kipindi cha nyuma walikuwa wanapata kila mwezi lita 290, kiasi kidogo sana. Petroli kwa mwezi hakuna. Tunashukuru kwa msaada wako Mheshimiwa Waziri, kutuletea injini kwa ajili ya matumizi ya ziwani, ingawa hatuna mtumbwi. Mimi mwenyewe binafsi nimetoa mbao 150 kwa ajili ya kuunda mtumbwi. *Oil No. 40* hakuna. Fedha za matengenezo ya gari hakuna. Mahitaji halisi kwa ajili ya ulinzi na utawala, tunahitaji dizeli lita 500 kwa mwezi. Petroli lita 300 kwa mwezi. *Oil No. 40* lita 50, fedha za matengenezo ya gari na *boat engine* shilingi laki mbili.

Tuna ubovu wa barabara kati ya vijiji vyetu Tarafa ya Karema. Karema ilio kando ya Ziwa Tanganyika, tunaomba msaada upande wa Mheshimiwa Waziri aweze kutusaidia kututengenezea walau kilomita nane katika mipango yake, kuimarisha nguvu za uwezo wa jeshi kando ya ziwa.

Mheshimiwa Spika, upande wa mapungufu mengine, tuna upungufu pia wa jenereta, walau ndogo ya *ku-charge* betri, inabidi wanajeshi wetu watoke umbali wa kilomita 130 kutoka Ikola hadi Mpanda Makao Makuu ya Wilaya, kwenda *ku-charge* betri kwa ajili ya *Radio Call*. Tendo hilo ni la hatari sana, naomba msaada wako Mheshimiwa Waziri, tuweze kupata vitendea kazi. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri, juu ya nyongeza ya *Radio Calls*, huko Ziwan kuna shida nyingi sana. Tungeweza kupata hata zile *Radio Calls* ndogo tukawapa wanamgambo wetu wakawalinda wavuvi, zile za mkononi ili waweze kuwasiliana na askari wetu huku upande wa pili nchi kavu. Maana ujambazi umekuwa mwangi majini na watu wanatekwa, lakini wanaweza wakasaidiwa iwapo patakuwapo mawasiliano mazuri kati ya ndani ya ziwa na ufukweni. Askari wetu ni mahiri, wana uwezo mkubwa na tunaomba waweze kutusaidia kwa kuwapa vitendea kazi ili kunusuru maisha ya watu na mali zao. Maeneo ya kando ya Ziwa Tanganyika, Karema na sehemu nyingine zote ni maeneo yaliyo wazi. Nguvu za utendaji kazi wa Wananchi wa kule ni uvuvi, uvuvi ni sehemu ya maisha yao, ni sehemu ya mapato. Ni ajira pekee kwa Wananchi wa kwetu kuweza kuondoa umaskini katika maeneo yale. Inapotokea hali kama hiyo, Wananchi wanashindwa kuingia ziwani kwa sababu ya ujambazi na uvamizi na mara nyingi wale waliokamatwa na wale waliotokea huko ni wale wanajeshi waasi wenye ujuzi wa kutumia silaha nzito kule upande wa pili wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Wizara hii mia kwa mia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautoshi kwa mchangiaji mwagine. Kwa hiyo, tunaishia hapo. Lakini kabla sijasitisha shughuli za Bunge, niwataje wale watakaochangia kipindi cha mchana. Mheshimiwa Shaibu Ahmad Ameir, alichapwa kimakosa kwenye orodha kwamba amechangia mara mbili, kumbe

alishachangia mara moja tu. Kwa hiyo, atakuwa yeze ndiyo msemaji wa kwanza kipindi cha mchana, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Bernard Membe na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, kuna nafasi ya watu wanne tu. Basi wajiandae hao niliowataja na baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo jioni hii kuongea katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, nami naungana na wenzangu kutoa mkono wa rambirambi kwa wazee na ndugu wa Marehemu waliofariki hivi karibuni katika Bunge letu hili, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza hotuba hii ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa jinsi ilivyotayarishwa na leo imetumalizia kasi yote kwani tulikuwa na kilio kikubwa sana katika mambo mengi lakini katika hotuba yake yote ameyataja. Kwa hiyo, tunaipongeza sana hotuba yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza mwenyewe Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kazi kubwa anayofanya pamoja na timu yake yote ya Wizara hii kwa juhudhi wanayofanya ili kuendeleza Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumpongeza *CDF*, Machifu wote wa Makao Makuu ya Jeshi, Wakurugenzi wote wa Makao Makuu ya Jeshi, Wanadhimu wote, Maafisa na Wapiganaji wote wa Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania pamoja na JKT kwa kazi yao kubwa wanayofanya na sisi tunaona kweli sasa hivi vijana wanachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza *Brigade Kamanda* wangu wa Nyuki, *Brigade* yaani *101KV* kwa kazi kubwa anayofanya. Yeye ni kijana mchapakazi, mwadilifu na mcha Mungu sana. Kwa hiyo, tunakwenda naye sambamba, begabega tukiwa nyumbani na tunampongeza sana kwa juhudhi zake anazofanya katika kazi hii. Vile vile sikuwasahau Boto pamoja na Bao wa *Brigade 101KV* kwa kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia salaam nawapelekeea Makamanda wa Vikosi wote wa Kanda ya Zanzibar kwa kazi kubwa wanayofanya pamoja na Maafisa na Wapiganaji kule Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri asubuhi aligusia masuala ya ujenzi. Ingawa ametupa moyo kabisa katika ujenzi wa hospitali ya Bububu yaani ni kuwa moja katika hospitali za Kanda zitakazopata msaada lakini bado tunamwomba lile jengo la *X-ray* alimalize pamoja na maabara kwa sababu maabara iliyopo siyo ya uhakika.

Kwa hiyo, haya tunaomba atumalizie kipindi hiki itakapofika wakati wa kujenga hospitali basi mambo haya yawe yameshamalizika vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2003/2004 nilimwomba Mheshimiwa Waziri ajenge barabara ya kwenda Bububu kwa sababu iko katika hali mbaya hasa wakati wa mvua inakuwa mbovu. Namwomba tena ile barabara aende kuijenga barabara ya Kambi ya Mtoni mle ndani barabara ni mbovu sana. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri ayazingatie hayo na ayatekeleze katika kipindi hiki cha mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Bububu imebahatika kupata fukwe nzuri sana ambayo iko Pwani. Namshauri Mheshimiwa Waziri nafasi ile aitumie kwa kuijengea *Rest House* ambapo itasaidia Maafisa wake wanapokuja Zanzibar au hoteli maana pale mahali watu wanapamezea mate, ni mahala pazuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuzungumzia kuhusu kiwanda au karakana iliyokuwepo Zanzibar kunako miaka ya 1990 iliyokuwa imejengwa makao makuu ya Jeshi karibu na Bwalo la Maafisa. Sehemu ile palikuwa na karakana kubwa ambayo inasaidia wananchi kuchonga vipuri vyta magari ya Jeshi na vipuri vyta aina nyingine. Kiwanda kile sasa hivi kimekufa kutokana na jengo kuwa bovu. Mashine zile zote zimepelekwa *Mtoni Camp* na hivi sasa havitumiki zimekaa tu kwa muda wa miaka 10 zipo pale. Mashine zile mimi naona huenda zikaharibika kukaa bila kazi.

Namwomba Waziri kama mashine zile sasa hivi Jeshi halizitaki kuzitumia ingezirudisha Serikalini kwa sababu zile mashine zilipatikana kwa msaada wa Wachina kwa Serikali ya Zanzibar. Kama hawataki kuzitumia wangerudisha Serikali wakawapa jamaa wa JKU ili zipate kufanyiwa kazi kuliko kuziweka pale.

Kambi ya Mtoni kama tunavyoijua ni mahali ambapo papo karibu na bahari hasa vyuma kama vile vikikaa siku nyingi vinaharibika. Tunaomba sana hizo mashine kama Jeshi sasa hivi halitaki kuzifanya kazi basi wazirudisha Serikalini ili wapewe jamaa wa JKU wafanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Tanzania kuwa ni nchi ambayo ni kitovu cha ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, vitendea kazi vilivyokuwepo wakati huo ni Wanajeshi. Sasa Wanajeshi hao wamestaafu na wengine wameshakuwa wadhoofuli hali.

Kitendo cha kuwaacha tu wakae bila kuwakumbuka itakuwa Taifa hili halikuwafanya jambo zuri. Wale sasa hivi hawana nguvu, wanastahili walelewe, kuwapa kiunuo mgongo pamoja na pension itakuwa bado hawajafikiriwa.

Mimi naomba Jeshi sasa hivi angalau lingeweza kuchukua nafasi ya kuanzia *Lt. Canal* na kuendelea mbele hawa watu ingewasaidia chochote ili wapate kuhuika maisha yao kama ngazi za juu wanavyozenziwa na Serikali. Hii imedhihirika wazi sasa hivi utakuta *Canal* mzima anatengeneza balskeli au anaiza madafu, *Lt. Canal* mzima sasa hivi utamkuta anakwenda kuchokoa pweza pwani, hali imezidi kuwa mbaya.

Vile vile nilimshuhudia mimi *Brigade General* mzima sasa hivi hali yake imekuwa mbaya sana toka amestaafu. Naomba Serikali hawa watu ingewatupia jicho la huruma angalau ikawalea kwa kumalizia umri wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukiangalia katika Maofisa wanaotoka Zanzibar wengi wanastaafu sana kwa umri na kiasi hiki sisi tunaona baadaye tutalaumiana kwa upande mmoja wa muungano kulaumu mwensiye kwa sababu Maofisa wengi wanatoka Zanzibar. Nashauri Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yako mngefanya *crash* ya kuwapa mafunzo Maofisa wapya kiasi cha *intake* mbili au tatu ili ku-cover pengo lile au kama sivyo basi itakuwa upande mmoja utamuelemea upande mwingine kwa sababu wataonekana upande mmoja Maafisa wote watupu upande mwingine hakuna Maafisa. Kwa hiyo, tunaomba mngefanya *crash*, mkachukua vijana wa Zanzibar kiasi cha kuweza kukidhi lile pengo liliopo pale ili tupate kuwa na uwiano mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, leo nitakuwa sina zaidi na naipongeza Wizara hii na naiunga mkono mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangulize shukrani kwako kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hoja aliowasilisha kwa utulivu na hoja zikieleweka waziwazi hali ambayo inatupatia nafasi ya kuchangia hotuba yake vizuri tukiwa na hakika ya kile tunachotaka kukisema.

Vile vile napenda nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa sababu naye aliwalisha na kutoa mapendekezo ambayo pia yamekuwa ni mazuri na yanaweka mwelekeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na hasa Jeshi lenyewe la Wananchi wa Tanzania kwa kazi kubwa ya Ulinzi na Usalama wa mipaka ya nchi yetu ambayo ni kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kwa uaminifu na uadilifu mkubwa. Kwa kweli nawapongeza kwa sababu wameweza kuweka hali ya amani na utulivu wa nchi yetu hali ambayo imepelekea nchi yetu kuwa na

mshikamano na kuwa na nafasi ya kutekeleza majukumu mengi ambayo kwa kipindi hiki yanatekelezwa kwa usahihi kabisa na Askari wa Miamvuli chini ya Serikali ya Awamu ya Tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali na Wizara husika kwa jinsi ambavyo wameweza kudumisha nidhamu ya hali ya juu katika Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa na wamekuwa ni watu ambao wakati wote wanapofanya kazi hujitahidi sana kuzingatia taratibu na hata wanapokuwa na matatizo yao hukaa chini na kuyatatua kwa kufuata taratibu kwa hiyo, hawana manung'uniko yanayokuwa ya hadharani wala yanayopelekea Taifa letu kukumbwa na aibu za viongozi au watenda kazi au walinzi wa nchi kulalamika. Ni suala ambalo napenda niwapongeze sana.

Lakini vile vile napenda nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa *General* Tumainieli Kiwelu, kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya katika kushirikiana kwa hali ya juu sana na Serikali kuhakikisha kwamba mipaka ya Mkoa ya Kagera ambayo ni ya nchi yetu inalindwa kwa wakati wote na anatoa ushirikiano wa kutosha kila inapotakiwa kufanya hivyo, nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru tena Serikali kwa uamuzi wake wa kuianzisha kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika Wilaya ya Muleba amba ni upanuzi na nyongeza ya kambi ambazo zimepata kuwepo na pia katika kambi chache ambazo Serikali imeamua kuanza nazo. Kwa kuanza kambi nyingine katika Wilaya ya Muleba ni suala ambalo nalipongeza sana na naishukuru Serikali kwa sababu kambi hii itaweza kutoa mafunzo, ujuzi na taaluma kwa vijana wengi zaidi nami naamini kwamba itakuwa ni ya manufaa zaidi hata kwa eneo lenyewe la Wilaya ya Muleba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Wizara na Serikali ni kwamba kwa sababu katika hotuba Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba wale vijana wanaopata mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, mwisho wa mafunzo yao huwa wote hawawezi kuchukuliwa na vyombo mbalimbali vya Jeshi likiwemo Jeshi la Wananchi na taasisi mbalimbali za *TANAPA*, Magereza na kadhalika.

Kwa msingi huo, ukizingatia kwamba mafunzo yale ya nidhamu, utifu, kujenga Taifa, umoja na mshikamano ambayo yanakuwa tayari yamekwishafundishwa na yamezama katika mioyo na tabia za vijana wale wa Jeshi la Kujenga Taifa mara wanapokuwa wametoka wale wachache wanaobaki bila kupata nafasi basi hurudi kwenda kukaa katika vijiwe ambapo vijiwe hivyo mara nyingi havina manufaa. Mimi nashauri basi katika kusaidia vijana wetu ambao wanaweza kubahatika kupata mafunzo haya, naomba Serikali ione uwezekano wa kutoa dhana kama vyerehani, mashine za useremala, fundi uashi na kadhalika ili wanapoondoka pale basi wakawe ndio vitovu vya kunzisha vikundi katika jamii vya kuweza kuinua maendeleo ya vijana na kujitegemea kuweza kuchangia uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba kama nilivyochangia katika Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana kwamba tunao vijana wa Taifa la leo na kesho na ni hazina kwa Taifa letu basi hawa ambao tunawapatia ujuzi ni vizuri tusiwapoteze badala

yake watumike kuwa kitovu cha uzalishaji mali na baadaye watakuwa ni vijana wazuri wa kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie la pili ambalo nimelichukua katika hotuba hii liko chini ya majukumu mbalimbali yanayohusu ulinzi wa nchi chini ya kichwa cha maneno Ulinzi na Usalama. Nawapongeza sana Wizara kwa mambo mengi walijokuwa wakiyafanya nami napenda chini ya kichwa hiki cha maneno nizungumzie lile linalohusu huduma ya tiba kama ambavyo limeelezwa katika Ibara ya 19 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambapo mionganoni mwa huduma ambazo wamekuwa wakizitoa ni pamoja na huduma ya tiba ambapo hospitali mbalimbali zimekuwa zinapata huduma na kwa ujumla dawa za kutosha zinapatikana katika hospitali, vituo vya afya na hata zahanati za Jeshi ambapo dawa zinapokuwa hazipatikani basi wale wagonjwa hununuliwa dawa kutoka nje ya hospitali hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri jambo hili kwa ambavyo mwaka 2003 pia nilipata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii, nami nilizungumzia moja kwa moja kuhusu kambi ya Jeshi la Wananchi Kaboya ambalo nilisema ni maarufu na inajulikana kwa kituo cha *2IKJ*.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu baada ya hotuba yangu Bungeni alichukua nafasi ya kutembelea katika kambi ile na akajionea mengi ambayo nilikuwa nimemweleza na hata mengine kuyachukulia hatua kwa mfano hatua ya kukarabati muundo mbinu wa maji machafu aliyoyaona. Lakini vile vile naomba kwa wakati huu nirudie kuyazungumza yale ambayo naona ni kipindi muafaka pia kuyarejea kwa kuwa bado hayajatekelezwa ipasavyo sio kwa lengo kwamba nataka kusahihisha napenda nikumbushe kwa sababu ya umuhimu wa jambo lenyewe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya Kaboya ni kambi ya muda mrefu na ni kambi maarufu katika Kambi za Jeshi la Wananchi Tanzania, naomba ifanyiwe ukarabati mkubwa mionganoni mwa ukarabati unaoendelea baada ya kwamba Serikali imepata msaada kwamba sasa tutakwenda kupatiwa msaada kutoka nchi za nje basi ule uwezo mwingine amba Serikali inao naomba ijaribu kuona uwezekano wa kuelekeza katika kambi ya Jeshi la Kaboya ili kuweza kuona zahanati niliyoomba ambayo ilikuwepo lakini ilipopigwa mabomu wakati wa vita vya Iddi Amini, basi tangu wakati ule haikuweza kujengwa nyininge.

Hali ya wananchi wa vijiji vinavyozunguka kambi na uhusiano na kambi ya Kaboya ni mzuri kiasi ambacho pamoja na huduma ndogo wanayoitaoa katika kambi ili walijonayo ambayo wanatumia tu nyumba za watumishi kutoa huduma za zahanati bado huduma hizo zinaweza kuenea kwa wananchi wanaozunguka vijiji vya kambi ile ambavyo viko katika kata tatu, kata ya Mayondwe, Izigo na Muhutwe. Takribani vijiji vyote 10 vikiwemo vile vya Mayondwe, Bugasha, Itoju, Izigo, Kabale, Katoke, Bushumba, Nyakashenyi na Busole wanategemea zahanati hii ndogo ambayo inayo Mganga mmoja na nesi mmoja.

Sasa ukiangalia wanaozunguka kambi ile na udogo wa zahanati lakini na umuhimu wa kambi na kazi kubwa ambayo Wizara yenye we imejikita katika kutoa

huduma za tiba kwa wananchi wake pia naomba sasa tujengewe zahanati nzuri ambayo itaweza kutosheleza mahitaji haya na vile vile itaweza kutoa huduma nzuri hata kwa kikosi chenyewe cha Kaboya.

Vile vile kulingana na umbali uliopo kutoka ilipo hospitali ya Mkoa na kambi ya Kaboya ni takribani kilometra 42, naomba wapatiwe usafiri wa *ambulance* ili kuweza kusafirisha wagonjwa kutoka Kaboya wale watakaokuwa wameshindikana kuwapeleka katika hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niliomba barabara ya mashujaa. Pale Kaboya ndipo mahali palipozikwa mashujaa. Wale wote waliopigana vita vya Kagera wakapoteza maisha yao kishujaa, bustani yao ya mashujaa iko pale pale Kaboya. Lakini barabara hii ambayo inatoka Ntungamo kwenda Kanyinya inapita katikati ya kambi na upande wa kushoto unapotokea Ntungamo ni mahali ambapo wale mashujaa walipopandikizwa katika bustani yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile barabara ni ya tope, napenda kuungana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ambapo imeomba Serikali ione uwezekano wa baadhi ya barabara kuwa ni za Jeshi badala ya kuziacha chini ya *TANROADS*. Nami naomba barabara hii ya Ntungamo - Kanyinya, iwe chini ya Jeshi kwa maana kwamba iwekewe lami. Lakini vile vite katika hotuba ya mwaka 2003/2004 niliomba kuwe na alama za kutoa ishara ya utii tunapopita pale mbele ya mashujaa kwa sababu ni barabarani kabisa kuondoa tu katika ile sehemu ya kutunza barabara kunakobaki basi ni mashujaa lakini unakuta upitaji wa pale haujengi heshima wala kuonyesha kwamba wenzetu waliokufa kishujaa wamepumzishwa mahali pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Kaboya ikarabatiwe, pia nyumba zake za kuishi ili kusudi mazingira ya pale yaweze kuwa bora na yaweze kuwavutia hata wale wapiganaji wanaoishi katika eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la tatu ambalo napenda kulizungumzia siku ya leo na inawezekana ikawa ndio la mwisho kulingana na wakati, kambi ya Kaboya kama zilivyo kambi nyingine zilizotajwa hapa ipo katikati ya mahali wanapoishi watu ina eneo lake kubwa ambalo linajulikana mipaka lakini na maeneo mengine hayajulikani. Kwa taratibu zake na kwa utamaduni wa wote wanaoishi Kaboya na Wakuu wa Kikosi pale wakati wote wamejitahidi kuwa na uhusiano mzuri wa wananchi wake wanaokaa pale.

Kwa hiyo, wamekuwa wakiwaruhusu kutumia maeneo ya Jeshi kulima mazao yao ya muda mfupi na kuondoka. Lakini katika hali kama hiyo, kulingana na hali halisi iliyopo sasa hivi ambapo ardhi imekuwa ni mali adimu na baada ya kupindi fulani watu wanaamua kuanza kuweka mazao ya kudumu na hata wengine kuamua kujenga na kuishi, nami naunga na ushauri wa Kamati kwamba ni vizuri maeneo ya Jeshi yakajulikana hata kama wanapenda kuendelea kuwa na mahusiano kwamba walime mazao ya muda mfupi lakini mimi nashauri maeneo hayo yajulikane wazi, yawekwe mipaka inayoeleweka ili kuhakikisha kwamba maeneo hayo wakati wowote yasije kuleta mgongano kati ya wananchi na Jeshi na hatimaye ikapelekeea kupunguza eneo la Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kupunguza eneo la Jeshi ni kama yale tuliyoyasikia katika kambi nyingine yanapelekea wananchi kupata madhara hasa wakati Jeshi linapokuwa katika mazoezi yake, risasi huweza kuruka kuingia katika miili ya wanachi, mifugo, majumba na kutishia maisha yao. Kwa sababu wananchi hawaji kwa siku moja na kujenga wanakuja taratibu sasa ule utaratibu wao wa namna ya kuja naomba uangaliwe ili wasiruhusiwe kujenga pale majengo ya kudumu na baada ya pale tena ikatokea mivutano kati ya Serikali au kati ya Jeshi na wananchi kitu ambacho kinaweza kuondoa amani na maelewano mazuri yaliyokuwepo.

Lakini kama vijiji vinavyozunguka vikaeleshwe hivyo, watendaji wa Serikali na wa Vyama vyta Siasa wakaeleweshwa hivyo na wananchi wakawa wanalijua hilo, ninaamini kabisa mahusiano yataendelea kuwa mazuri lakini na mipaka ya Jeshi itaheshimiwa na hakutawenza kutokea tatizo lolote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hilo kwa sababu najua tunakozidi kuelekea tunataka kusisitiza juu ya utawala wa sheria kama nchi yetu ilivyo. Kwa hiyo, katika sheria hii, ni vizuri ubinadamu unapoingia usisahau taratibu, taratibu zikisahaulika moja kwa moja watu wakishakuwa wamezoea kuwaondoa katika tabia ya mazoea sasa wanaanza kudai kwamba ile ni haki yao na ndio mwisho wa baadhi ya maeneo ya Jeshi kupewa wananchi. Napenda wananchi wapewe maeneo hayo lakini maadam yalitolewa kwa ajili ya Jeshi basi yabaki kwa ajili ya Jeshi na wananchi wapate maeneo mengine ambayo bado yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, kwa jinsi ambavyo ameitambua kazi ya uongozi wa Mkoa wa Kagera nami na Mheshimiwa mwenzangu wa Wilaya ya Muleba, Mheshimiwa Wilson Masilingi na mimi wa Muleba Kaskazini basi akatambua shughuli yetu. Naomba sasa tushirikiane katika kuona haya ambayo yako ndani ya uwezo wake yaweze kutekelezwa na Serikali ili zile pongezi nyingi alizozitoa kwetu zionekane katika matendo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na pia nawaombea utekelezaji mwema katika majukumu ya Wizara kwa kipindi kijacho tena nisisahau kuwaombea waongezewe bajeti kwa sababu wanayo majukumu mengi ya kutekeleza ambayo Wizara inatakiwa kuyasimamia yanahitaji pesa za kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, aliyoiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoniongoza leo katika mchango wangu ni maswali mawili ya msingi ya Kimataifa. Swali la kwanza ambalo litaniongoza katika mjadala huu, ni je, Jeshi letu linao uwezo wa kutulinda, kujilinda na kuchakaza maadui wa Taifa hili kwa wakati wowote, kutoka upande wowote, muda wowote nchi yetu itakapokuwa inavamiwa kama ilivyotokea mwaka 1978? Swali la pili je, azma ya Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ya kulitaka Jeshi letu liwe dogo, imara na bora kwa ajili ya kulinda mipaka na raia wa nchi hii, inatekelezwa kwa vitendo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kila ninapajaribu kujibu maswali haya, naikumbuka vita ya mwaka 1997 kati ya Ethiopia na Eritrea. Eritrea nchi ndogo kweli kalikokuwa Jimbo la Ethiopia na baada ya kumng'oa Mengstu Haire Mariamu, Rais au Waziri Mkuu Zenawi, akaahidi kuliondoa Jimbo lile iwe nchi kamili na ikawa. Lakini mwaka 1997, mwezi Februari, Eritrea iliivamia Ethiopia nchi kubwa ile na baada ya mwaka mmoja na nusu Waethiopia kuwa *humiliated* kijeshi na ilikuwa *humiliated* kweli, Eritrea ilishika sehemu ile ya Badea kwa muda wa mwaka mmoja na nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ndogo iliyokuwa Jimbo, ilisaidiwa na Ethiopia yenye we iliishinda nchi kubwa ya Ethiopia. Nilipokuwa najiuliza maswali haya, picha iliyokuwa inakuja ni ya Ethiopia na Eritrea kwamba kumbe nchi jirani bila kujali ukubwa au udogo wake inaweza kuivamia nchi kubwa kama Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu maswali haya, zipo njia tatu kubwa ya kwanza ningeweza kwenda kwenye Jeshi letu kueleza udhaifu wa Jeshi letu unaoweza kutufikisha pabaya lakini kufanya hivyo wakati mwingine sio vizuri. Njia ya pili ni ya kuangalia wenzetu katika nchi zilizotuzunguka wana nguvu za Kijeshi kiasi gani ili tujilinganishe na sisi wenye we ndio kazi nitakayoifanya sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tujue na kwa takwimu zilizotolewa na *CIA World Report* mwaka 2002 na Chuo cha *Stockholm International Peace Research Institute (Correspondence of Military Expenditure)* ya mwaka 2003 itatuongoza kuzijua nchi zinazotuzunguka na nguvu zao za Kijeshi na matumizi yao ili tujipime.

Kenya katika mwaka 2002 Pato lao la Taifa lilikuwa dola bilioni 32 za Marekani. Katika Pato hilo la Taifa walitumia 2.1% yaani dola za Marekani milioni 185 kwa ajili ya matumizi ya Jeshi, linganisha na Tanzania ambayo kwa mwaka huo wa 2002 kwa *GDP* ya dola bilioni 19.6 za Marekani tulitumia 0.2% kwa ajili ya matumizi ya Kijeshi.

Uganda ambapo *GDP* yao kwa mwaka 2002 ilikuwa dola bilioni 31 za Marekani walitumia 2.1% na wenye we sawa na dola za Marekani 124 milioni kwa ajili ya matumizi ya Kijeshi kununulia silaha mbali ya fedha nyingine za misaada zinazotoka sehemu nyingine duniani.

Rwanda nchi ndogo *GDP* yake mwaka 2002 ilikuwa dola bilioni 6.4 za Marekani na walitumia dola za Marekani 112 milioni sawa na asilimia saba ya Pato lake la Taifa kuwekeza katika matumizi ya kijeshi. Burundi Pato lake la Taifa mwaka 2002/2003, ni

bilioni 3.8 dola la Marekani, matumizi waliyoyatenga kwa ajili ya Jeshi ni asilimia 5.3 ya pato lake la Taifa sawa na *US Dollar 42 million*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Angola ambao ndio bingwa wa *National Air Defence* katika Afrika, inayopiga vizuri sana katika Afrika, yenyewe ilikuwa na dola bilioni 16.9 za Marekani. Pamoja na vita vyake vyote lakini walitenga dola za Marekani 227 milioni katika shughuli za Kijeshi. *DRC, GDP* yake ni bilioni 34, wakatenga asilimia 4.6 ili kufanya matumizi yawe milioni 250 dola za Marekani kuhudumia shughuli za Jeshi lao. *Mozambique* nayo katika *GDP* yake ya bilioni 19 na wenyewe kidogo walitumia asilimia moja, sawa na milioni 35 za Marekani kwa ajili ya Jeshi lao. Malawi wametupita pia katika kutenga asilimia ya matumizi ya kijeshi wao ni 0.7 sawa na milioni 13 za Marekani kwa *GDP* ya bilioni 7.2 kwa mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningweza kwenda kwenye nchi kubwa za Kiafrika kama *South Africa* ambayo *GDP* yake kwa mwaka 2002 ni bilioni 434 dola za Marekani na katika hizo wametumia nusu ya bajeti tulioipitisha hapa mwezi uliopita kwa ajili ya matumizi ya kijeshi. Wanaume wanatumia fedha kulinda majeshi yao na kuhudumia majeshi yao kwa kujilinda hata yale ambayo hayana vita ndani yake. Tulinganishe na Tanzania ambayo katika mwaka 2002, ukiachia mbali misaada mingine kwa pato la Taifa la bilioni 22, tunatumia milioni 19 tu, tumpitwa karibu na nchi zote za *SADC* katika kutenga fedha za matumizi ya kuhudumia Jeshi letu, tumpitwa na nchi za wenzetu wa Afrika Mashariki katika kutenga fedha zile za Pato la Taifa kuhudumia majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo njia moja niliyosema ukitaka kujipima kama una nguvu mwangalie Musa kama ana nguvu zaidi ya wewe, wasiwasi wangu upo hapo. Tukiendelea kufuata masharti ya nje yanayotaka *severe military budget cutting* kwamba tupunguze matumizi ya Jeshi letu eti tu kwa sababu hatuna vita na kwamba Tanzania ni nchi ya amani na utulivu tunaweza kuja kujuta siku moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoona nchi za jirani zinakuchokoza chokoza mara wateke nyare binadamu, mara waingie, mara wakutukane, wamesoma takwimu hizi zinaweza kuwa za kweli sana na zinaweza zisiwe za kweli sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unapozisoma takwimu hizi ukajua nguvu ya Jeshi ya nchi jirani yako unaweza kuifanyia vituko hivi lakini haya wanayotufanyia nchi za jirani ya kuteka watu au za kuingia ovyo na kututukana tukana visingeweza kutokea kabla ya mwaka 1978 wakati Jeshi lile lilivyokuwa katika hali nzuri sana katika nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubali kwamba mwenendo wa Jeshi letu tunaudumaza wenyewe. Bajeti ya Angola katika Jeshi peke yake ni zaidi ya trilioni tatu tulizozipitisha sisi katika mwaka huu wa bajeti kwa nchi nzima. Tuna haki gani ya kufuata kila tunachoambiwa na kutekeleza kila tunachoambiwa bila kujali uchungu na usalama wa nchi yetu? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tena kwamba tukiangalia takwimu nilizozitoa za nchi zinazotuzunguka na chokochoko ndogo ndogo zinazojitokeza kwa nchi hizi zinazotuzunguka, hatuwezi kukaa kimya na kudhani kwamba Jeshi letu lipo *combat ready*. Jeshi letu lazima tuliiamarishe liwe na uwezo wa kulinda nchi yetu, kujilinda wao wenyewe na kuchakaza maadui kwa dakika yoyote, kwa upande wowote na muda wowote watakapoingia katika nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za wenzetu zinatumia ujanja mmoja mkubwa wa kujaribu kulea majeshi yake na kuyaweka katika hali nzuri. Njia moja wanayoitumia ni ya ku-*engage* au kuyashirikisha Majeshi haya katika *peacekeeping missions* kwamba unapolishirikisha jeshi lako katika Majeshi ya kulinda amani unapata faida kubwa tatu. Faida ya kwanza, askari wako wanapata posho wanapokuwa katika vituo vile vya nje.

Pili, askari wako wanapata mafunzo ya kijeshi na matumizi ya kisasa ya sayansi na teknolojia katika vyombo vya kijeshi vinavyoendelea kule duniani. Tatu, ni kwamba nchi yenyewe pamoja na Wizara inapata faida ya kupata silaha mpya ya ku-*replenish* yaani kila silaha aidha zinapotumika kwa miaka minne wanapewa silaha mpya, kwa ajili ya vijana wake wanaopigana au wanaolinda amani katika nchi hizo za nje. Hilo linapotokea ndipo nchi pia inavyoweza kujisaidia katika masuala ya matumizi ya Kijeshi. Tukililegeza hilo tunajiua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa wito huo kwamba njia moja ya kujaribu kulipa uzito suala hili ni kuwashirikisha vijana wetu katika *peacekeeping missions* na kwa vile Tanzania ni nchi ya amani ya utulivu jukumu hili ni letu na la kihistoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kutokana na sababu hizi zote nilizozosema na takwimu hizo zote nilizozitoa ndizo zinazonifanya niunge mkono mia kwa mia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu bila kupoteza muda na bila kutia ubishi kuitisha bajeti ambayo ni ndogo sana ukilinganisha na nchi zote zinazotuzunguka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuipitishe kwa *speed* za mwanga wa juu na tumwombe Waziri kama fedha hizi zinakwisha alete *Supplementary Budget*, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi yupo hapa, tupitishe tena ili Jeshi hili tuliuine na tujenge hadhi ya Jeshi letu kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tunajenga hadhi ya Taifa letu. Heshima ya nchi yoyote ile ni ukakamavu na uhodari wa Jeshi lake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi hii ili kuwa mmojawapo wa wachangiaji kwenye hotuba hii ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Lakini vile vile nimpongeze Waziri wa Ulinzi kwa hotuba yake safi na nzuri inayotia moyo, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Ulinzi na wataalam wote walioiandaa hotuba hii. Lakini vile vile niwapongeze dada zetu hawa ambao mara mara tunakuwa

pamoja kwenye Kamati yetu kwa kazi zao nzuri, Ndugu Vevo Mchango pamoja na Imakulata. Nawapa pongezi za dhati kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kila kiongozi ana mipaka yake ya kazi. Haiwezekani kwamba kiongozi huyu amwingilie kiongozi huyu ikiwa Waziri, Makatibu na wengineo. Kwa hiyo, namweleza ndugu yetu hapa mchangiaji wa upande wa Upinzani ambaye alisema kuwa Mkuu wa Majeshi apewe sheria za uchaguzi aende nazo Pemba na kitabu kile akamate mkononi, ile si kazi yake. Ile ni kazi ya Tume ya Uchaguzi na sisi viongozi wa kisasa. Halafu vile vile kama kutatokea uvunjaji wa sheria, Mkuu wa Jeshi si kazi yake, Wizara ya Mambo ya Ndani ndio wanaohusika, Jeshi la Polisi kudhibiti na kupeleka Mahakamani. Kama hilo halijui basi alijue. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa awe mstahimilivu, asubiri kama alivyosubiri Sereweji aelimike, halafu aanze kuchangia. Asianze kimbele, *front*, wakati hawezি. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Chama chetu cha Mapinduzi kina sera ya amani na utulivu. Hakitothubutu hata siku moja kuchukua vijana na kuwaandaa kufanya vurugu kwanza hakina sababu hiyo. Kwa hiyo, wananchi wake waliomwambia kwamba kuna vijana wameandaliwa kufanya vurugu, mimi namwambia akawaambie hilo halipo kwa sababu sera ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake ni amani na utulivu na ndio maana nchi za nje wanapenda sana kuwekeza, kutalii na mengi mengineyo. Hilo alijue na hatuna sababu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwambia kuwa vurugu Chama cha Mapinduzi hasa Zanzibar hawatuwezi, kwa sababu tulipindua na tunayajua yote na natumai kuna msemo unasema kwamba: "Samaki hafundishwi kuogelea baharini." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nachangia kuhusu kambi yangu ya Welezo ambayo mwaka 2003/2004, nilichangia na nikamweleza Waziri atembelee pale ili aione kambi hiyo ilivyo, ina uchakavu wa ofisi na uchakavu wa hospitali, kwa hiyo namwomba aiangalie kwa jicho la huruma. Katika hizo fedha za maendeleo alizotenga na hospitali hiyo ishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilichangia mwaka huo huo kuhusu kambi yetu ya Kisakasaka na Chukwani, haina umeme na hili alitazame ili aweze kupeleka umeme Chukwani na Kisakasaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza sana Waziri kwa hospitali yetu ya Bububu lakini bado hatujaridhika. Mwaka 2004/2005 isiwe *story*, tuwe tumeshamaliza jengo lile kwa sababu hospitali ile ni hospitali ya wanajeshi na viongozi wengi tunapenda kwenda pale pamoja na wananchi wengi tu naipenda hospitali ya Bububu. Kwa hiyo, nampongeza lakini namwomba imalizike haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kutoka Zanzibar ni sawasawa na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano kutoka Tanzania Bara, kwa hiyo, lolote lenye kasoro ni wajibu wetu kulisema hapa Bungeni na hasa Wabunge wa Chama Tawala. Itakuwa vibaya sisi Wabunge Chama Tawala kukosoa kwenye majukwaa vya kisasa na uwezo tunao wa kusema hapa. Kwa hiyo, ndugu zetu na Waheshimiwa wetu hawa Mawaziri wanaohusika na Wizara hizi za Muungano, wasituone kwamba tunawasakama, ni haki yetu kufanya hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nipo kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa hiyo, sina wasiwasi na hotuba hii, isipokuwa kama alivyosema Mheshimiwa Bernard Membe, kwamba nchi zote zinajiandaa kwa mapambano yakinoteka wakati wowote na kuna usemi wa kiulinzi unasema hivi: “Vita haiishi, isipokuwa inaahirishwa.” Vita havishi nchini isipokuwa vinaaharishwa, vinaahirishwa kukiwa na hali ya amani na utulivu. Mimi leo lilivyoahirishwa Bunge hapa nikaambiwa nitachangia saa hizi, nilijiandaa kuja kusema. Kwa hiyo, wakati vita sasa hivi havijakwisha ila vimeahirishwa, vijana wetu lazima tuwape uwezo wa kuwa na zana za kisasa na za kutosha ili hivyo vita vikiwa tayari waweze kupambana kileo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini juu ya hayo yote, tunakubali kwamba Wanajeshi wetu wana uzalendo na hasa kutokana na makazi yao wanayokaa, jinsi nyumba zao zilivyo chakavu, nazo vile vile tunaomba ziboreshwwe tusiwe tunawasifu kwa uzalendo wao huku wanapokaa hapastahiki. Mheshimiwa Waziri tumetembea nyumba kadhaa tumeziona safi sana, nzuri lakini zizidi kuboreshwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu wanajeshi wastaafu. Sisi Kamati ya Ulinzi na Usalama tunasikitishwa sana, tunasikitishwa kwa jinsi wanajeshi wetu wanavyostaafu bado wangali vijana wabichi kabisa kabisa, wana uwezo na hasa maofisa. Hivi sasa Jeshi letu tumeliweka kama Jeshi la mpito kwa sababu akishastaafu hapa anaondoka anatakiwa Uganda, Burundi, Kongo na kwingineko, lakini hapa tumeshamwondoa. Falsafa inasema hivi: “Furahia mabadiliko lakini usiyaombee kwa sababu huyo anayekuja hujui atakuendesha vipi.” Haya mabadiliko kila wakati mara huyu kakaa siku mbili hayupo, siku mbili kakaa hayupo, siyo mazuri, mwisho watakuja kuona wanaburuzwa.

Kwa hiyo, naomba sera ya Jeshi ibadilishwe, tusaidiane na tukishasaidiana miaka iongezwe ili maofisa wetu waweze kufanya kazi vizuri. Tunawakosa maofisa wataalam ambao wana ujuzi. (*Makofî*)

Nimekwenda hapa kwenye gari za Nyumbu nimeona vijana wetu wa Jeshi lakini keshokutwa watakuwa hawapo pale, sijui tena wataandaa nini kingine ambacho tunajivunia sasa hivi kwamba Nyumbu ni nzuri lakini kesho kutwa watakuwa hawapo na wakiwa hawapo itabidi tuwaandae wengine. Kwa hiyo, hili vile vile ningeomba lifikiriwe kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nasema kwamba Jeshi lolote nchini huwa lina nidhamu na taratibu, kwa hiyo, hata tukiwa na timu au michezo Jeshini huwa

zinafanya vizuri sana na vile vile wana wakati wa kucheza. Kwa hiyo, vile vile ningeomba Mheshimiwa Waziri ziundwe timu ambazo zinaweza kutukomboa na zikawa timu nzuri za kuweza kuleta mabadiliko ya kimichezo hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo nazidi kuwapongeza wapiganaji wote kwa kazi zao nzuri wanazofanya za uzalendo na nasema kwamba naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ingawa kwa dakika kidogo. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Wawi wakiwemo Makamanda na Wanajeshi wa vikosi vya *14KJ* na *151KJ*, napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi zake nzuri na ushirikiano mzuri na kutuletea hotuba hapa iliyso safi kabisa yenye mwelekeo wa kimaendeleo, bila kupoteza muda napenda kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli leo nimefarijika sana kuipata hii nafasi, nilifikiri sitoipata, lakini nimeipata na sina maneno mengi isipokuwa nasimama hapa kwa kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri inayofanya kwa kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2000, kwa kutekeleza mambo ya maendeleo katika nchi yetu. Naishukuru sana Serikali. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri leo imenifurahisha sana kuingiza mambo fulani fulani ya kimaendeleo katika Jimbo langu la Wawi. (*Makofi*)

Kwanza ni ukarabati wa majengo ya askari, nawashukuru sana na naipongeza Serikali. Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, nampongeza sana leo na askari huko waliko leo wamefurahi na wanansikia Mbunge wao ambavyo nafurahia, kwa hiyo, nashukuru sana kwa sababu wanajeshi wale wanaishi katika mazingira magumu na toka mwaka wa kwanza nilipoingia hapa Bungeni natetea, natetea, *Alhamdulillah* leo tumefikia angalau nusu. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali ziingizwe fedha hizo, Wabunge wenzangu tukubali tuingize fedha tufanyiwe mambo ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili vile vile ukarabati wa hospitali yetu ya Jeshi ya *14 KJ*. Napenda sana kuishukuru Serikali kutenga fedha ambazo zitatutengenezea hospitali yetu ile kwa sababu hospitali ile ni ndogo sana na vile vile haina sehemu hata ya kujifungulia akinamama pale wakiwa wajawazito mpaka waende Chake Chake hospitali kuu ndio waende kujifungua. Vile vile haina *generator* wala majokofu. Kama tunavyojuua askari wengi wanaofanya kazi sehemu ile ni wale ambao wengi wanatoka katika maeneo mbalimbali ya sehemu za bara na nyingine. Kwa hiyo, ikitokea ajali ama kifo basi maiti mpaka ipolekwe katika hospitali ya Chake Chake. Vile vile matatizo ya umeme katika Kisiwa cha Pemba ni makubwa, kwa hiyo, ikipatikana jenereta pale na jokofu basi litatusaidia na vile vile kama nilivyozungumza ni vizuri sana sehemu ya kujifungulia akinamama, katika fedha hizo za ukarabati na hiyo iingizwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda sana kuishukuru Serikali kwa kukubali kutoa eneo lake la *14KJ* na kujengwa *Supermarket* ambayo itawahudumia askari, ni kwa ajili ya askari. Toka mwaka wa kwanza nilipoingia hapa Bungeni natetea

*Supermarket* kwa sababu nilikuwa nawaona na sio siri ni kwamba askari walikuwa na matatizo, wanakwenda Mjini Chake Chake kule kukopa, kununua vitu katika maduka ya watu binafsi. Ile ni kudhalilisha, sio nzuri kwenda kukopa kopa tu Mjini kule, siyo vizuri kwa askari, kwa hiyo, ni vizuri kuwa na duka lao wenyewe na hivi sasa napenda kusema kwamba leo hii hii nimezungumza na huko kikosini, nimeambiwa tayari limeshaezekwa kila kitu isipokuwa labda vifaa ndio vinataka kuingizwa katika awamu hii. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kuwaonea huruma maaskari hao na kuwapatia *Supermarket*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda sana kuipongeza Serikali kwa kikosi chake cha Jeshi kushiriki katika kujenga nyumba mia tatu za hapo Kisasa. Ile inaonyesha kwamba maaskari wetu wana umuhimu mkubwa sana si katika suala la ulinzi tu, bali hata masuala mengine ya ujenzi wa Taifa. Kwa hiyo, tunawapongeza sana askari hao na tunawaomba wasichoke, wailinde nchi hii pamoja na kuiletea maendeleo. (*Makofi*)

Mwisho, sipendi nipoteze muda, napenda sana kuishukuru Serikali kwa kuwaunganisha wanajeshi na kuwapatia mafunzo mbalimbali hasa hasa yale ya *computer*. Hata kule katika Jimbo langu la Wawi baadhi ya maafisa wamekuja Dar es Salaam kupata mafunzo ya *computer*. Hiyo ndiyo kazi inayotakiwa Mawaziri wafanye na Serikali yetu ifanye, sio inawaacha tu askari wanalinda tu bila kupatiwa ujuzi wowote. Hivi sasa ni dunia ya sayansi na teknolojia, kwa hiyo, nashukuru sana Serikali kuamua uamuzi huo wa kuwafundisha wanajeshi wetu, masomo ya *computer*.

Kwa hiyo, wenzangu nakuombeni sana leo hii tuipitishe hotuba hii na vile vile kwa mara nyingine iongezewe bajeti, iwe ni kubwa zaidi ili maaskari wetu wawe katika hali ya furaha kwa sababu na wao wanatufurahisha kwa kutulinda usiku na mchana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshismiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wake, Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Makamanda wote wa vitengo na maeneo mbalimbali, Wapiganaji na Watendaji wote, raia wanaofanya kazi kwenye Majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naheshimu sana kazi zinazofanywa na Jeshi letu kulinda mipaka ya nchi yetu. Pia naheshimu na kupongeza sana huduma zinazotolewa na Jeshi letu kwa raia kama huduma za matibabu katika maeneo mbalimbali, huduma za maji, maduka na kadhalika. Pia napongeza sana kazi zinazofanywa na Jeshi kama Kandarasi za ujenzi wa nyumba zinazotolewa na Serikali, pia ujenzi wa barabara, madaraja na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana mafunzo yanayotolewa na Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu. Napongeza sana kazi za uzalishaji wa mazao mbalimbali zinazotolewa na vijana wetu kwa mazao kama zabibu, mahindi na pia mboga za aina mbalimbali zinazoongeza vipato kwa kambi zetu. Nimpongeze sana Mkuu wa Kambi ya Makutupora, maana nasikia kupitia kilimo ameweza kununua magari mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mkuu wa Chuo cha Monduli kwa kazi nzuri anayofanya kwa kutoa Maofisa wa Jeshi walioiva kama wale amba mimi mwenyewe nilishuhudia wakipata kamisheni tarehe 31 Julai, 2004. Hata hivyo, naomba Serikali iongeze fedha zinazotolewa kwa Jeshi letu la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa, mafunzo, ujenzi wa nyumba za Maofisa wa Jeshi na wapiganaji, sare, magari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba yake nzuri sana, aliyosoma kwa ufanisi mkubwa na kuifanya ieleweke vizuri sana. Hongera sana na naunga mkono hoja hii kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, napenda kuwapongeza Katibu Mkuu, Bwana B. S. Mchomvu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George Waitara, Mnadhimu Mkuu wa wa JWTZ M-Luteni Jenerali Iddi Gahu, Mkuu wa JKT, Meja Jenerali David Mwamunyange na wasaidizi wao wote kwa kumsaidia Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa na kuijengea Wizara hiyo heshima kubwa humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa niaba ya Wabunge wenzangu amba tulishiriki katika zoezi la kulenga shabaha huko JKT Makutupora tarehe 25 Julai, 2004, kwa heshima kubwa tunatoa shukrani zetu nyingi kwa kuruhusiwa na kuandaliwa zoezi hilo. Tunaomba tupelekewe shukrani zetu kwa Meja Mosha na Maafisa wasaidizi na askari walioendesha zoezi hilo kwa heshima, nidhamu ya hali ya juu, uvumilivu na uelewa mkubwa.

Vilevile shukrani kwa huduma nzuri sana kwa siku hiyo nzima, kuanzia asubuhi hadi alasiri. Hongera sana na wote tunaunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za wanajeshi katika Kambi ya Mtoni, naomba Serikali ichukue hatua za kujenga nyumba za kutosha katika Kambi ya Jeshi ya Mtoni Zanzibar ili Wanajeshi wa kambi hiyo waishi kambini badala ya sasa kupanga au kuishi nje ya kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo ya wanajeshi, naomba Serikali iwapatie mikopo muafaka wanajeshi wote, mikopo ya vifaa vya nyumbani ili familia zao ziondokane na wasiwasi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa Kambi ya Mtoni Zanzibar, naomba sana ukarabati wa hali ya juu sana kwa Kambi ya Mtoni Zanzibar, kwani hivi sasa baadhi ya majengo katika kambi hiyo ni ya zamani sana na yamechakaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashirikiano ya vyombo vya ulinzi, naomba Serikali wakati wote iwe na ushirikiano mkubwa na vyombo vya ulinzi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hasa katika mambo ya kiutalam, ikizingatiwa zaidi mambo ya ulinzi wa bahari, anga na nchi kavu.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina sababu yoyote ile ya kutoikubali hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nimpongeze kwa jinsi alivyoandaa hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo ya kusisitiza. Jeshi letu ni jeshi lenye nidhamu ya hali ya juu na ni jeshi kweli la wananchi. Nidhamu hiyo tunaitegemea ionekane hata katika mazingira ya kawaida pale wanapoishi na majirani zao (*private life*). Utunzaji wa fedha walizopangia na Serikali, ni kweli inatia aibu jeshi letu linapolinganishwa kwa ufujaji wa fedha hizo na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, *financial discipline in the army* ni jambo muhimu sana. Ukitiwa *Audit Reports* karibu zote, Jeshi linaonekana kuwa na tatizo la nidhamu ya matumizi ya fedha wanazopewa na Serikali. Soma *Audit Reports* za 2001/2002, makosa karibu yanafanana. *Repeatedly*, makosa ni hayo hayo ya matumizi mabaya bila kufuata utaratibu. Tenda kutolewa bila kufuata taratibu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mtazamio wangu kuwa inawezekana kabisa Jeshi halina wataalam wa kutosha wenye fani ya uhasibu. Pia inawezekana kuna ulegevu wa kufuatilia kanuni na taratibu za kifedha ndani ya majeshi. Lakini pia inawezekana kuna watu ndani ya majeshi, wanafanya makusudi. Hivyo basi, sasa umefika wakati kwa majeshi yetu kujiangalia upya kukomesha kabisa *financial indiscipline in the army*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mgambo, jeshi la Mgambo ni jeshi la akiba pale nchi inapoingia matatani. Jeshi hili, hakuna mtu anayekataa lisiwepo, wala wananchi wasifundishwe shughuli za kijeshi. Matatizo yaliyopo ni kwamba askari hao baada ya kufuzu, hubaki tu vijijini. Hakuna mratibu wa shughuli zao hapo kijijini. Hakuna anayefahamu mgambo huyu hapo kijijini taaluma yake hiyo anaitumiae.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi hili bila ya usimamizi wa kutosha, ni mazalio ya ujambazi, unyanyasaji na kila aina ya uovu unaweza ukajitokeza kwa kutumia askari hao ambao wamefundishwa shughuli za kijeshi, ambao hawana mratibu na hana kazi. Maoni yangu ni kwamba sasa umefika wakati wa kujua askari hao wakoje, nani anaratibu shughuli zao za kila siku hapo kijijini walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya mgambo. Mafunzo ya mgambo ni muhimu kama nilivyosema hapo awali. Wakufunzi wa mgambo huko vijijini wanatakiwa pia kuwa na nidhamu kwa wale wanaowafundisha. Huko Bariadi Kata ya Kasoli, wakufunzi wa mgambo wanafanya vituko. Mwananchi akichelewa au asipoenda eneo la mafunzo, wakufunzi kwa kutumia sungusungu na mgambo Kata, wanatoza faini, wanakusanya kuku, mayai na kadhalika. Hili linafanya wananchi waone mgambo ni wa lazima na ni adha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kuwa, lingekuwa ni jambo la manufaa kwamba wakufunzi wakae na wanafunzi wao wajadili na waelimishane taratibu za kufuatwa kwenye mafunzo. Mimi nitaungana na wanakijiji chochote kuwaelimisha wananchi kwamba mafunzo ya mgambo ni ya Kikatiba. Lakini kupora mayai, kuku na kutozwa faini, siyo sehemu ya mafunzo ya mgambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili nilishalisema tena mwaka 1998, jinsi wakufunzi walivyokuwa wakitoza faini, wanachukua kuku, mayai na kadhalika kwa mtu asiyehudhuria mafunzo. Pia nilishasema ndani ya Bunge lako Tukufu jinsi ya wakufunzi walivyokuwa wananyanya wazee ambao watoto wao hawapo katika meneo hayo, wengine wamesafiri na wengine wamehama. Wazazi hasa baba, anakamatwa achukue nafasi ya mwanae katika mafunzo. Haya yalikwisha baada ya kulisema hili Bungeni. Namshukuru Mheshimiwa Edgar Maokola-Majogo, alilikomesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu na leo Mheshimiwa Waziri atalitolea kauli suala hili linalowafanya wananchi wachukie mgambo bila sababu. Ahsante.

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wataalam wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara yao. Kwa kuendelea, naomba niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba nizungumzie Shirika la Nyumbu. Shirika hili lilianzishwa kama kituo cha uhawilishaji teknolojia (*transfer of technology*) na uendeshaji teknolojia ya kutengeneza magari. Tangu kituo cha Shirika kuanzishwa, kumekuwa na tatizo la Shirika kutopata fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba ielewewe kuwa Shirika hili pamoja na majukumu ililo nayo, pia ni kituo au chombo cha utafiti na maendeleo (*Research & Development Institution*). Kutokana na hali hiyo, Shirika linahitaji sana msaada wa fedha za kuendeleza *Research & Development* katika Shirika hili, ili liweze kuwa na maendeleo ya uundaji magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika lina wasomi wazuri sana wenye uzalendo, ari na shauku kubwa ya kufanya kazi. Shirika limefanya kazi nzuri sana na nydingi sana kwa

mfano magari yaliyoletwa hapa Dodoma na mengineyo kama la Zimamoto, vipuri kwa DAWASA, magari moshi na vinu vya kuchambulia pamba, korosho na mengi mengineyo. Haya wameweza kuyafanya kwa sababu ya ari, moyo, uzalendo, stadi na elimu waliyo nayo. Kwa kazi hizi nzuri, mimi nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali mwaka 2004/2005 imewatengea shilingi milioni 600, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwapa zaidi. Hii au Shirika hili ni la kiutafiti zaidi kuliko uzalishaji kibashara. Kutowapa fedha ya kutosha, kutawafanya wafanyakazi wengi kutotumika ipasavyo na kama watacaa muda mrefu hawafanyi kazi, kwa maana nyingine kukaa bila kutumia elimu na stadi walizo nazo, kunaweza kuwafanya wahame kwenda sehemu nyingine ambako watatumika kikamilifu. Hii itafanya shughuli za Shirika kuzorota. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza bajeti ya Shirika hili ili liweze kufanya kazi nzuri iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho niiombe Wizara kuwa vitambulisho vya wanamgambo vinachelewa kuletwa kwa vijana wanaomiliza mafunzo yao. Baadhi ya Washauri wa mgambo wa Wilaya, hawana vyombo vyausafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuwapatia vyombo vya usafiri hata kama kwa kuwakopesha. Kwa wale amba wana magari, lakini yameharibika, basi iangaliwe kama wanaweza kuwapa mikopo ya kutengenezea magari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu ili niwe mchangiaji kwa maandishi hii leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na wataalam wake wote, kwa kuleta hotuba yao nzuri sana. Hivi sasa naanza kuchangia hotuba hii

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003/2004 kwa mchango wangu, nilizungumzia Kambi za Wachukwani na Kisakasaka. Kambi hizi hazina umeme na leo katika hotuba ya Waziri, hakugusia kambi hizo. Kwa hiyo, nataka maeleo Mheshimiwa Waziri atafanikisha lini kuziwekea umeme kambi hizi!

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilizungumzia Kambi ya Welezo kwa Hospitali yao chakavu sana. Kwa hiyo, ifanyiwe ukarabati. Lakini hadi leo, kambi hiyo haina ukarabati wa barabara wala ukarabati wa hospitali ya kambi hiyo, pia wakiweza na ofisi chakavu kabisa. Kwa hiyo, naomba Waziri anieleze kambi hii itatekeleza lini haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hospitali ya Bububu, huu ni mwaka wa nne hospitali hii iko kwenye *story* tu. Kwa hiyo, namwomba Waziri atuelezee kwa kina kabisa mradi huu utamalizika lini.

Mheshimiwa Naibu spika, kuhusu Mradi wa Mgodi wa Meremeta. Mimi niko kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama, lakini tunasikiti hadithi tu za mradi huu. Ni wajibu wetu kujua mradi huu ili tuweze kuueleza pakitokea hoja. Kwa hiyo, namwomba Waziri aelezee ni lini Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, watapelekwa kwenye mradi huo ili kuona kazi inayoendelea! Siyo kupata sifa za juu juu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Jeshi la Nyumbu na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri, pamoja na wanajeshi wote.

**MHE. KHADIJA SALEH NGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa rambirambi zangu kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yetet Mwalyego na familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri na ya kupigiwa mfano popote pale, si hapa Tanzania tu, bali na nje ya nchi. Jeshi hili kweli ni Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kutimiza ahadi yake aliyoitoa katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2002/2003 katika Kituo cha Jeshi cha Potoa, kilichopo Zanzibar, nashukuru sana. Hivi sasa juhudhi za kukamilisha uwekaji wa umeme, zinifikia ukingoni na naamini mambo madogo madogo yaliyobaki yamatilizika mwaka huu wa 2004, kama maji na siku za uhakika, huku ukizingatia umuhimu wa kituo hicho kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia, kwa Wizara hii kukitupia jicho la huruma kituo hiki cha Potoa, kilicho na askari wavumilivu kwa muda wa zaidi ya miaka 40 bila kituo hicho kuwa na mambo muhimu ya kibinadamu kama maji safi, umeme na simu. Natumai vijana hao wanastahili kupongezwa kwa utulivu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa mara nyininge.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Maofisa wa Jeshi, wapiganaji na watendaji wote katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwa uadilifu na juhudhi ya hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, tunaishukuru Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa juhudi zake katika kuanzisha Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa huko Burigi, Muleba Kusini. Nachukua nafasi hii kwa mara nyingine kuwahakikishia ushirikiano wa wananchi wa Wilaya ya Muleba na Mkoa kwa ujumla, katika kufanikisha uanzishaji wa Kambi mpya ya Jeshi la Kujenga Taifa kule Burigi, Muleba Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AISHA P. MAGINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa pole kwa wale wote waliopata matatizo katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti. Pia natoa rambirambi kwa familia za Waheshimiwa Wabunge waliopoteza maisha hivi karibuni. Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la nyumba kumi za Jeshi, zilizoko Wilayani Kibaha, Mkoani Pwani ambazo zimeharibika vibaya. Hazijawahi kufanyiwa matengenezo yoyote tangu zijengwe. Sasa je, Serikali inasema nini juu ya kuzitengeneza na kuziua nyumba hizo kwa wanajeshi wanaokaa katika nyumba hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nyumba tatu ambazo zimebomoka kabisa yaani zimeezuliwa mabati na paa zake na hakuna anayeishi humo. Je, isingekuwa ni vema kuzijenga upya na kuwauzia wanajeshi kuliko kuziacha kama zilivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna taarifa ya kuwa kati ya nyumba hizo, moja haikaliki, kuna maajabu yaani anayeishi huko, hupigwa usiku na vituko vingi bila kumwona anayefanya hivyo na hivi sasa hakuna anayeishi humo. Naomba suala hili la nyumba za Kibaha liangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwunga mkono Mheshimiwa Waziri, hotuba yake ipite. Ahsante sana.

**MHE. DANHI B. MAKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, lakini nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kambi za Jeshi, makambi ya majeshi kukaa mijini, siyo vizuri na yanatakiwa yahamishwe ili yawe mbali na makazi ya raia hasa wa mijini.

Aidha, ujenzi wa makambi mapya nje ya miji, unaweza kugharamiwa na mapato yatakayopatikana baada ya kuuza maeneo nyeti ya katikati ya miji, ambayo yanahitajika sana na yatanunuliwa kwa bei ya ghali au wanaweza kutafuta wabia wa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kiuchumi na pato yatakayopatikana yajenye kambi mpya. Pia askari kukaa nje ya raia wengi, yatadumisha nidhamu kwa askari wetu ambapo sasa wamekuwa na tabia za kiraia mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujambazi, kwa sababu nchi yetu sasa haiko vitani na kwa sababu tatizo la ujambazi linazidi kukua siku hadi siku na kusababisha upotevu wa maisha ya raia na mali zao na kwa kuwa hata magari na watu wanaogopa kutembea usiku na hivyo kuathiri uzalishaji/uchumi wa Taifa letu, ni muhimu sasa Jeshi letu likatumika kufanya operesheni maalum na hata kama italazimu iwe ya kudumu hadi hapo jambazi la mwisho litakapokamatwa na kushikishwa adabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, polisi wetu wameshindwa kazi hii na kwa hiyo wasaidiwe. Jeshi letu lina sifa kubwa Afrika na hata duniani, kwa ukakamavu na maarifa na ujasiri na ndiyo maana nchi jirani zinaogopa kutuingilia. Sasa kama tumetisha majeshi ya nje, vipi majambazi wachache sana kama hawa waendelee kutubabaisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makazi, nyumba za kukaa askari ni shida, lakini Jeshi hili sasa linatumika kujenga nyumba za Serikali, kitu ambacho tunakipongeza sana na wameonyesha uwezo mkubwa wa kitaalam na uzalendo. Sasa kwa nini tusitumie Jeshi hili kufanya ujenzi wa nyumba zao makambini, nyumba za Polisi, majengo ya Shule za Msingi Vijijini, Shule za Sekondari, Zahanati na kadhalika. Serikali itumie Kandarasi hawa ili kuepuka ubabaishaji, wizi na uhuni unaofanywa na makandarasi wengine na kutoa kazi hafifu sana na hivyo kuleta hasara Kitaifa. Hata ujenzi mkubwa miradi, mikubwa kama barabara, madaraja na kadhalika ni vema wakapewa uwezesho wa kivifaa na utaalam ili hatimaye wapewe kazi hizo zote.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na ya kina. Pia nawapongeza wapiganaji kwa kazi yao nzuri ya kudumisha amani nchini

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa heshima niliyopewa ya kuratibu ujenzi wa mnara wa kumbukumbu ya mashujaa wetu. Nitajitahidi kutimiza wajibu wangu. Naipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa suala hili. Naomba kusisitiza kuwa Watanzania tulishiriki katika Vita vya Ukombozi wa Bara la Afrika kwa sababu ya kutambua wajibu wetu kama watu huru kwa wenzetu waliokuwa wakitawaliwa na kunyanyaswa na wakoloni, tulichangia fedha, nguo chakula, damu na mwisho uhai wetu, vijana wetu chini ya uongozi wa Jemadari wao Mkuu Hayati Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, walijitoa mhanga na kushiriki katika mapmabano ya ukombozi, wale waliokufa vitani, maiti zao zilirudishwa na kuzikwa Tanzania, lakini maiti nyingine zilizikwa katika maeneo ya mapambano kwa sababu ya ugumu wa kuzirudisha Tanzania na pia wengine walijeruhiwa na kupata ulemavu wa maisha na tunao mionganoni mwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Watanzania tumeamua masalia ya miili ya mashujaa hao, izikwe rasmi na kwa heshima zote za kijeshi, ili kutunza kumbukumbu ya mchangano wao katika ukombozi wa Bara la Afrika, miili ya mashujaa hawa imegeuka udongo, lakini mchangano wao utakumbukwa milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, majina ya askari wetu wa Jeshi la Ulinzi, yameandikwa kwa wino mwekundu yaani katika ardhi ya nchi kadhaa za Bara la Afrika,

ilibidi vijana wetu wengine wafe na kulemazwa ili wengine wakombolewe na tunawashukuru wote walioshiriki kufanikisha kazi hii ya kihistoria. *Inshallah.*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenta Taifa Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha vizuri sana. Napenda nimpongeze *CDF*, Makamanda na Wapiganaji wa Jeshi letu kwa kazi nzuri wanayoifanya kulinda nchi yetu. Katika kutekeleza majukumu haya makubwa, tunawapa heko viongozi wa Wizara chini ya Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Mchomvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 nilimwomba Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa awalete Wataalam wa Jeshi (*Field Engineers*), waje Mwanga watusaidie kulipua mawe na kutengeneza barabara za (i) Vuchama - Managugu - Ngofi, Tarafa ya Ugweno, (ii) Mwero - Butu, Tarafa ya Usangi, (iii) Mangio Kivisini, Tarafa ya Ugweno na (iv) Ndorwe - Kilomeni - Sofe - Chanjala, Tarafa ya Dembeni. Zikikamilika barabara hizi, zitakuwa kichocheo kikubwa cha uchumi wa Wilaya yetu. Mwezi Septemba, 2002 wataalam wanenye wa Jeshi wakiongozwa na Kamanda wa Kikosi cha *Field Engineers*, walikuja akakagua barabara zetu, wakafanya makadirio ya kazi yenyewe na vifaa vinavyohitajika na askari watakaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya *sorovea* ya wataalam wa Jeshi, tulipewa mapendekezo ya kazi ya awali ambayo wananchi walitakiwa kuifanya ili kazi ya Wanajeshi ya kuzitengeneza barabara hizi, ichukue muda mfupi. Wananchi wa Mwanga wakaifanya kazi hiyo mara moja na wakajitayarisha kushirikiana na wanajeshi waliotegemewa kufika Novemba, 2002. Hadi leo, askari hawajafika kufanya kazi ambayo Mheshimiwa Waziri alituahidi. Hii ni pamoja na Maafisa wa Jeshi waliokuwa kwenye hoja ya bajeti ya Wizara hii mwezi Julai, 2003, kuahidi kuwa kikosi hicho kitafika Mwanga kabla ya mwisho wa mwaka 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ya Jeshi kutotekeliza ahadi yake, imewafadhaisha sana wananchi. Wananchi hawaelewii, inakuwaje Jeshi litoe ahadi halafu ahadi hiyo isiwe? Kwa niaba ya wananchi wa Mwanga, naomba sana sana kuwa huu ni wakati muafaka wa kutekeleza ahadi hiyo ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunamshukuru Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa kushiriki kikamilifu katika ufunguzi wa Maabara ya Harambee ya ujenzi wa Hosteli ya Shule ya Sekondari ya Cleopa Msuya. Vijana wa Mwanga wanamshukuru sana Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi. Ahsante sana.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza mno Wizara hii kwa kazi nzuri na madhubuti ya wapiganaji wetu pamoja na Makamanda wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii kwamba wakati wa amani, ishirikiane na Jeshi la Polisi na wananchi (*Sungusungu*) kupambana na wimbi la wahalifu (majambazi) sugu. Naliagini Jeshi litaweza kuondoa kero hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Majeshi yaingilie kunusuru hadhi ya michezo nchini kama riadha na mpira, ili ziwakilishe Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ile *Garage* ya Nyumba ifufuliwe na kuimarishwa upya. Hata hivyo, nawatakia kazi njema na kila la kheri Wapiganaji na Makamanda wote.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani na pongezi nyngi sana kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu, Makamanda Marwa na wa Jeshi la Kujenga Taifa, Mwamunyange na Makamanda wengine ndani ya Majeshi yetu. Kazi nzuri za vikosi zinaonekana. Waziri wa Wizara hii, yupo karibu sana na Wanajeshi wetu, mpenda watu, hana makuu na ni mchapakazi. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu Jeshini. Elimu ni ufunguo wa maisha, wanajeshi wetu katika fani zao waendelezwe kimasomo hadi shahada na ujuzi mbalimbali wa teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu michezo Jeshini. Katika nchi hii, michezo ni afya. Hivyo, ni muhimu kuwa na timu za michezo tofauti. Timu zetu ziimarishwe kupewa vifaa muhimu kama vile mipira, jezi na uwezo, walimu na makocha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Daraja la Ubena na *culvert* la Mdaula, vikosi vya Jimboni - *KJ92, KJ121, CEK* na *KJ621*, wanapata matatizo ya usafiri kwa barabara zao. Tumejitahidi nao, lakini tunahitaji msaada wenu Makao Makuu. Gharama ndogo sana, naomba twende tukaone ili utusaidie daraja hilo dogo.

**MHE.AZIZA SLEYUM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wizara hii inafanya kazi kama nyuki na matunda yake ni asali. Hii inamaanisha ushirikiano wa pamoja kati ya Waziri na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika suala la ujenzi wa nyumba. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hii inamaanisha askari wa mwanzuli wanavyoshirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa barabara, nina imani na haki ya kutamka kuwa hata kama tutawaongeza bajeti Wizara hii na kupata vitendea kazi askari wetu, nina imani kuwa Makandarasi hawatatusumbua na kujipatia pesa nyngi zaidi za ndani ya nchi hii na kujinufaisha wao na nchi yao. Kwa hiyo, barabara hizi, vijana wetu wanajeshi wangejenga vizuri zaidi na kujipatia mapato mengi zaidi ili kupunguza matatizo ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la barabara, ningependa Mawaziri watatu wa Ujenzi, Ulinzi na Fedha, wakakaa na kukubaliana kuwa fedha uwape/kuwakopesha Jeshi kiwango cha fedha ambacho watajipatia vifaa vyta kutendea kazi, vifaa vyta ujenzi wa barabara na hatimaye kazi hizo za barabara zifanywe na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu UKIMWI, naomba sana Jeshi kuweza kutoa semina nyingi kwa askari hao ambao wengi ni vijana na vijana ndio waathirika. Tunaomba sana suala hilo liwe ni agenda kubwa ndani ya Jeshi hilo, kwani wengi wanaopotea ni vijana, nasi ndiyo tegemeo letu kubwa sana. Vijana ndio nguvukazi, kama vijana wataondoka kwa wingi, itakuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maeneo ya Jeshi, naomba Wizara iandalie zaidi makambi ya vijana. Makambi hayo mengi sasa yanakua mijini kutokana na kukua kwa miji. Lakini itakapopata maeneo mengine ambapo watafanya mambo yao kwa usiri na bila kuwa na wasiwasi na ugomvi wa askari na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Tatalinda na kujenga nchi yetu.

**MHE. DR. ABDULKADER A. M. SHAREEF:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuungana na Wabunge wenzangu kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuwapongeza wanajeshi wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuilinda nchi yetu. Tuna fahari na kujivuna kwa utendaji kazi wao. Pongezi zangu maalum kwa Jenerali George Waitara, kwa uongozi wake wa kupigiwa mfano Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupendekeza mambo mawili, la kwanza ni kwamba Jeshi letu limetoa mchango mkubwa katika ukombozi wa Bara la Afrika. Katika mchango huo, wapo walikuufa ndani ya nchi na nje, ambapo ndugu zao wengine pia walikuufa kutoka nchi mbalimbali ndani ya Afrika. Lakini hapana kumbukumbu maalum ya wakombozi nchini. Tunayo kumbukumbu ya mashujaa ambao wakombozi ni mashujaa vile vile. Lakini bado wakombozi wanahitajia kuwekewa kumbukumbu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo napendekeza tuanzishe *Ukombozi Square* Jijini Dar es Salaam ambapo kila mwaka tutawakumbuka kwa kushirikiana na wawakilishi wa wapiganaji wakombozi kutoka Mataifa ya Kusini mwa Afrika. Tuchague *round about* moja Dar es Salaam na kuiita *Ukombozi Square*, yenyе kumbukumbu ifaayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yetu kwenye vikosi vyta amani kuitia *UN* au *AU*, umekuwa duni sana. Ni mara chache sana kushiriki. Wakati umewadnia kujaribu kushiriki kwenye shughuli za utunzaji amani kuitia *UN* na *AU*. Vijana wetu watapata uzoefu, vifaa na heshima zaidi. Nashauri tuliangalie kwa makini suala hili katika siku zizazo, hasa pale ambapo mchango wetu utakuwa wa manufaa makubwa kwetu na kwa wale tutakaowasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho narudia kusema tena kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa pole kwa familia na ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Mkoani Morogoro. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia juu ya ulinzi wa baharini. Kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge na nimetembelea na kuona mimi mwenyewe hali ya *Navy*, naomba kupatikane vyombo vingine vipya ili kukamata nafasi bora ya Ulinzi wa Bahari na Maziwa ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, chelezo (*slipway*) ni muhimu sana kwa uhai wa vyombo vya Baharini. Hivyo, chelezo cha Kigamboni ni kibovu na kinahitaji matengenezo na kitanuliwe ili kiwe na uwezo wa kupandishwa vyombo vyetu na vyombo vingine ambavyo ni vikubwa, ili kuleta mapato ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majengo (nyumba). Majengo ya makambi yetu mengine ni ya zamani. Kwa maana hiyo, mabovu na yanahitaji hatua ya haraka kufanyiwa ukarabati, aidha, kuongezwa nyumba zaidi kwa ajili ya Maofisa na Wapiganaji wetu. Wapiganaji wetu, baadhi yao bado wanaishi iraiani, jambo ambalo ni hatati kiulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zana za ulinzi, kulingana na hali ya ulimwengu wa kileo na hali ya matokeo ya vita vya kileo yaani teknolojia ya kisasa, napendekeza kupatikana zana za kivita za kisasa yaani Ndege za kisasa, silaha za mapambano (kivita) za kisasa, manuari zenye uwezo mkubwa zaidi na mafunzo ya kitaalam kwa Makamanda na wapiganaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nilipata nafasi nzuri ya kuchangia nilipokuwa ndani ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge lako Tukufu, nategemea kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na watendaji wake wote, watafuatilia na kuyachukulia hatua kulingana na hali ya uwezo wa bajeti yetu ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa mara nyingine tena kumwomba Waziri kupitia kwako, kuyatatua au kuliondoa tatizo la Kambi ya Bumbwini Kongwe huko Zanzibar kwa usafiri wa uhakika (gari), maji safi (kupatiwa mabomba ya maji), mawasiliano (redio za mawasiliano) na kujenga uzio wa kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu, nina matumaini kwamba Mheshimiwa Waziri atayashughulia ipasavyo yote niliyochangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. ANNE KILANGO MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia hotuba hii katika vipengele viwili muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kustaafu askari, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukisikia kilio chetu cha Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kuhusu askari wastaafu. Askari wa Jeshi letu kulingana na sera yetu, wanastaafu wakiwa na umri mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili iliyopita, tulimwomba Amiri Jeshi Mkuu awatumie viongozi wa Jeshi hasa Majenerali wetu wanaostaafu, kwani umri wao unawaruhusu kuendelea kulitumikia Taifa. Mheshimiwa Rais ametuitikia kilio chetu kwa kumteua Jenerali Mstaafu Rashid Makame kuwa Balozi wa Tanzania, nchini Malawi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali inapokamilisha uandikaji wa sera mpya ya ulinzi, iboreshe kipengele cha umri wa kustaafu askari. Mfano hai ni Jenerali Robert Mboma, ambaye bado ni kijana na sasa hivi ni Jenerali Mstaafu. Jenerali George Waitara, nina uhakika miaka sita ijayo kama si pungufu, atakuwa Jenerali Mstaafu. Atakapostaafu atakuwa ni kijana mdogo bado. Serikali iliangular hili. Niendelee kumwomba Mheshimiwa Rais aendelee kuwatumia Majenerali wastaafu kwenye nafasi Serikali, ambazo zinalingana na vyeo vyao. Kwani wana uwezo mkubwa wa kuendelea kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kwamba Serikali iendelee kuboresha Jeshi la Kujenga Taifa. Vijana wanapopitia Jeshi la Kujenga Taifa, wanajenga uzalendo na ukakamavu. Serikali ihakikishe inarejesha makambi yote yaliyokuwepo mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake nzuri na ya kusisimua ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Jitihada za Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi katika kuendeleza Wizara yake, ni za kutia moyo na za kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kukumbushia ombi la vijana wa Jimbo langu la Siha, la kupatiwa nafasi za kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Nitapenda pia kueleweshwa zaidi kuhusu utaratibu ambao unatumika katika kuwapokea vijana ambao wapo tayari kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa unyenyekevu na heshima kubwa, nachukua fursa hii kuunga mkono hoja hii. Hongera Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi kwa kazi nzuri.

**MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Makamanda wote kwa kazi

nzuri sana ya kuandaa hotuba hii ya bajeti ambayo ni ya kina na yenye mwelekeo na matumaini ya kuendeleza vyombo hivi vya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda pia kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu katika jitihada zake za kuimarisha vyombo hivi na hasa kulirudisha Jeshi la Kujenga Taifa katika hali yake ya zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo kuhusu barabara za ulinzi. Suala hili siku hizi halitiliwi mkazo. Napenda barabara hizi zisimamiwe na JWTZ. Majeshi yetu kama JWTZ, Polisi, Usalama wa Taifa, Uhamiaji, waajiri vijana katika JKT. Tunalipongeza sana Shirika la JWTZ, Nyumbu kwa kazi nzuri ambayo hivi sasa zinafanyika. Shirika hili lipate fedha zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikosi cha Ujenzi cha JKT sasa kipewe uwezo zaidi kutokana na kazi nzuri sana inayofanyika. Tumeona kazi zao wa ujenzi wa nyumba 153 kwa miezi mitatu kule Dar es Salaam na sasa nyumba 250 hapa Dodoma. Liongezwe fungu la fedha kwa ajili mafunzo. Mafunzo kwa majeshi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, ila naomba kuchangia kitu kimoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya mgambo. Walimu wa mgambo walioko huko Wilayani wanafanya kazi yao kwa shida sana kwa sababu ya kutokuwa na usafiri wa kuaminika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Nzega muda wote imekuwa ikipelekewa mikweche ambayo hufika pale na kupakiwa kama *scrap* katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri tutapatiwa gari jipy?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bwana Mchomvu, Katibu Mkuu, Jeneral George Waitara, Mkuu wa Majeshi, Luteni Jeneral Iddi Gehhu, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi, Meja Jeneral David Mwamnyange, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kazi nzuri ya ulinzi wa Taifa hili, nikijumuisha Watendaji Wakuu wote wa Wizara, kwa maandalizi ya hoja hii kwa unadhifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa namna ya pekee nimshukuru tena sana Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa usikivu wa kero kadha za Jimbo letu la Uchaguzi la Kilombero, hususan hasa kwa kuelekeza matumizi ya *Bail Bridges* za Kiberege na Sagamaganga, ili kuwezesha kuunganisha mawasiliano ya majimbo mawili ya Uchaguzi ya Kilombero na lile la Ulanga Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina haja ya kusifu sana utendaji wa Wizara hii, hususan kwenvye mawasiliano na raia. Naamini Jeshi letu ni lenye mawasiliano bora sana na raia wake kuliko majeshi mengine mengi duniani. Pamoja na migogoro mingi, naamini ufumbuzi wake ni kuelimishana tu kwa vikao, mikutano kati ya Jeshi lenyewe, viongozi wa Serikali na kisiasa na raia.

Baada ya kusema hayo, naomba sana Wizara hii iweze kurejesha uanzishaji wa Kambi la JKT, Chila lililoko jimboni kwangu. Pamoja na mipango mingine iliyandoaa Jeshi letu, ningeomba Wizara irejeshe Chuo hicho na kuzingatia jukumu la kukuza sekta ya kilimo ili kuinua hali ya uchumi wa raia wanaowazunguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Jeshi letu ni Jeshi la Wananchi. Ushahidi ni pamoja na utengenezaji wa gari la Nyumbu, *Suma Ltd.* na ujenzi wa nyumba pamoja na *TANZASINO* kwenvye huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na kuitakia Wizara hii kupewa mafungu yaliyoombwa bila kipingamizi. Ahsante.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza sana Waziri wetu, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara hii. Amekuwa mtu mwenye mahusiano mazuri na mapenzi kwa wananchi wa Taifa hili. Pia amekuwa mstari wa mbele kutembelea kambi zetu za Jeshi na kuwafariji wapiganaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara aliyofanya Mheshimiwa Waziri katika Mkoa wa Mbeya, ametupa faraja sana na matumaini makubwa kwake binafsi, Rais wetu na Chama cha Mapinduzi kwa ujumla. Amekuwa mfano wa kuigwa kwa unyenyekevu na uchapakazi wake. Mungu amzidishie na aendelee na msimamo wake huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa niaba ya wananchi wa Mbeya, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri na kuikarabati Hospitali ya Jeshi, Kambi ya 44KJ Mbalizi - Mbeya, chini ya ufadhili wa Wajerumani. Hospitali hii imekuwa kimbilio la wananchi wa Wilaya nzima ya Mbeya Mjini na Vijijini. Imesaidia kuondoa kero ya muda mrefu ya huduma nzuri na bora za afya, kwa wapiganaji wetu na raia wote wa Wilaya ya Mbeya, hususan maeneo ya Mbalizi, Songwe, Iwindi na Umalila kwa ujuma. Tunashukuru kwa wema huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni Kambi ya Itende nayo imefanya kazi nzuri kwa upande wa mahusiano na raia wote wanaoizunguka kambi hii. Wamekuwa mstari wa mbele kwa michango mbalimbali ya maendeleo. Wamenisaidia sana katika Ujenzi wa Shule ya Sekondari Kalobe, jirani na kambi hii. Moyo huu naomba uendelezwe na wapiganaji wetu wapewe nyenzo za kuhimili maisha ya leo, ili waweze kulitumikia vizuri Jeshi letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Jeshi limefanya kazi nzuri sana katika maeneo kadhaa, zikiwemo za kuokoa maisha ya wananchi, kusaidia wananchi wakati wa maafa na kuonyesha umahiri mkubwa wanapopewa *tender* za ujenzi, kama nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali itoe *tender* nyingi na fedha nyingi kwenye Jeshi. Utengenezaji wa magari kwa kutumia ujuzi wao wenyewe, ni hatua kubwa mno. Eneo hili lipewe motisha wa vifaa na fedha ya kutosha. Wapelekwe kujifunza zaidi ili waweze kupata teknolojia mpya zaidi (Kikosi cha Nyumbu ni hazina kubwa).

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera kwa Waziri na Watendaji wake wote. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, Katibu Mkuu wa Wizara, Mkuu wa Majeshi, Jenerali George Waitara, pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuanda mpango mzuri wa bajeti hii yenye mwelekeo wa kuimarishe Ulinzi na Usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi za awali, nazidi kutoa pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, pamoja na watendaji wake wote, kwa kazi nzuri wanayofanya siku hadi siku katika suala zima la ulinzi wa nchi hii. Naishauri Serikali sasa ifikie wakati wa kuona umuhimu wa Wizara hii kuwa na Naibu Waziri, kwani Wizara hii ni kubwa, ni nyeti na yenye majukumu mazito katika Taifa hili. Haistahili kuwa na Waziri bila msaidizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwa jinsi ninavyomfahamu Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, kwa jinsi alivyo mchapakazi na makini katika utendaji wake. Wizara ikipata Naibu Waziri, mafanikio yatakuwa maradufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huu wa awali, napenda pia nitoe ushauri juu ya Jeshi la Mgambro. Naipongeza Serikali kwa juhudzi za kuendesha Jeshi la Mgambro katika maeneo mengi nchini kwa lengo la kuimarishe ulinzi na usalama wa raia na mali zao kwa kuongeza wapiganaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudzi hizi, napenda niishauri Serikali kuwafikiria Walimu wa Jeshi la Mgambro kuwapatia usafiri, kwani Jeshi hili la Mgambro kuanzia ngazi ya Wilaya mpaka Mkoa, hawana usafiri jambo ambalo linawapa ugumu wa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tatizo hilo la usafiri, Jeshi hili linakabiliwa na tatizo la vitendea kazi. Mfano silaha, sare na vifaa vingine vyta kijeshi yaani ngazi ya

Wilaya na Mkoa. Nina hakika Wizara ikikubaliana na mimi katika ushauri na kuutekeleza, tutakuwa tumeleta ufanisi katika zoezi zima la Mgambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuboresha sekta ya malipo ya pensheni kwa wastaaifu, tofauti na ilivyokuwa zamani. Vile vile naendelea kuipongeza Serikali kwa kuwathamini askari wanapokuwa kazini. Naishauri Serikali kuwathamini askari hata wanapostaafu, kwa kuwalipa mafao yao kwa wakati kwani wapo askari waliostaaifu zamani hadi leo hawajalipwa mafao yao, hata kumbukumbu zao hazionekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kufufua Mafunzo ya JKT (Operesheni Mkapa), kitendo ambacho kimepunguza vijana wengi waliokosa ajira na kukata tamaa. Kwa kuwa zoezi hili limekuwa ni ukombozi kwa vijana wengine, naishauri Serikali ipunguze masharti ambayo yanawanyima haki vijana wengi wenye nia na uwezo. Mfano michoro mwilini, elimu. Mfano, aliyemaliza Darasa la Saba, kukataliwa au maumbile ya mwili kama miguu kutokuwa na ufa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi lina utaratibu wa askari kukaa/kutumikia Jeshi miaka sita bila kuoa au kuolewa. Naishauri Serikali kwamba sheria hii ibadilishwe mapema iwezekanavyo kutokana na gonjwa hili la UKIMWI pamoja na maambukizo mengine kwani askari wengi wanapokaa bila ndoa, huenda ovyo bila kujali maambukizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali, kwani imekuwa ikitoa mikopo mbalimbali kwa maafisa wa ngazi za juu. Naiomba Serikali sasa iwatazame askari wote wenye nia ya maendeleo yao kwa kuona uwezekano wa kuwakopesha vifaa vya ujenzi na samani kwani kambi nyingi za Jeshi la Wananchi ziko mbali na miji inayotoa huduma za kukopesha kama *TUNAKOPESHA Ltd*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika takwimu za suala zima la UKIMWI, kati ya Taasisi ambazo zimekumbwa kwa kiasi kikubwa na janga la UKIMWI, ni pamoja na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hivyo, basi naishauri Serikali iweke mikakati ya kutosha ya kupambana na janga hili la UKIMWI ili kuwanusuru wapiganaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuishauri Serikali kwa maeneo kadhaa ambayo naamini Serikali itayafanyia kazi, sasa namalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia moja.

Pia napenda kuwapongeza Makamanda na Wapiganaji/Wanajeshi wote kwa kazi nzuri wanayofanya ya kulinda nchi yetu. Naishauri Serikali kuwapatia vitendea kazi vya kutosha, hasa Kambi ya Ihumwa na JKT Makutupora, yakiwemo magari ili kuboresha usafiri katika makambi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze idadi ya vijana wanaojiunga na JKT na makambi ya kuchukua vijana yaongezwe.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo mzuri kwa Taifa letu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Mchomvu, Jenerali George Waitara, Mkuu wa Majeshi, Luteni Jenerali Iddi Gahhu, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi na Meja Jenerali David Mwamunyange, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, kwa uongozi wao mzuri na kuliongoza Jeshi letu kwa nidhamu ya hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa hivi sasa linafanya kazi nzuri sana ya kulea vijana wetu kwa nidhamu kubwa na kuwapa mafunzo ya kila aina na hatimaye vijana hao wanapomaliza kozi zao huwa wanajipatia ajira mbalimbali kama kujiunga na Jeshi (JWTZ), Polisi, Idara ya Wanyamapori na kadhalika na wanaobaki basi hujifunza jinsi ya kujitegemea kwa shughuli mbalimbali kama ufundi, kilimo, uvuvi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mafia, naliomba sana Jeshi letu upande wa JKT waje Mafia na kuona uwezekano wa kuanzisha kambi ambayo itakuwa inashughulikia masuala ya ulinzi na hata kuanzisha Mradi wa Ujenzi wa Maboti na kujishughulisha na masuala ya uvuvi. Hivyo, vijana wetu watapata elimu nzuri inayohusu uvuvi wa kisasa na uundaji wa maboti kibashara au hata kwa kutumia wenyewe Jeshi kwa kuvulia na kuwatumia samaki hao makambini au hata kuuza nje ya wilaya na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mkuu wa Jeshi la Ulinzi na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, waje Mafia na kuona uwezekano huo wa maoni niliyoyatoa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa uongozi wake mzuri katika Jeshi la Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri asimamie vizuri Jeshi lake ili lisije likatumwi vibaya katika Uchaguzi Mkuu wa nchi wa mwaka 2005 na kuhakikisha kuwa Jeshi halijiingizi katika ushabiki wa kisiasa hasa kule Zanzibar kama ilivyotokea kule Pemba mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri ashughulikie suala la mpiganaji ambaye alishindwa kuendelea na kazi ya Jeshi kutokana na kupata ugonjwa wa akili. Mpiganaji huyu amewahi kuwasilisha barua yake ya malalamiko Wizarani ambayo iliandikwa tarehe 11 Januari, 2004 ambayo ilipelekwa Makao Makuu ya Jeshi. Mpiganaji huyo ni Bwana Abdalla Suleiman Khamis mwenye Namba *TR0921*. Pamoja na maelezo haya naambatanisha nakala ya barua hiyo kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ya Ulinzi, kuongeza dawa katika hospitali za Jeshi kwani hata wananchi wa kawaida huwa wanapata matibabu katika hospitali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uajiri katika Jeshi, naishauri Wizara kuajiri vijana katika Jeshi letu bila kuangalia itikadi ya Chama hasa kule Zanzibar namwomba Waziri awe mwangalifu na afuatilie kwa karibu sana taratibu za uajiri katika sekta hii.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nampongeza Mheshimiwa Waziri na wapiganaji wote kwa kazi nzuri ya ulinzi na uzalishaji wanazoendelea kutekeleza, naomba nizungumze machache yafuatayo:-

Kwanza, nawapongeza JWTZ kwa juhudi zao za kuboresha mazingira ya makabi yao, ikiwa ni pamoja na majengo yao ndani na nje kama vile Makao Makuu ya JKT. Hata hivyo, bado kuna haja ya kuendeleza zoezi hilo kwa ufanisi zaidi hadi katika unadhifu wa wapiganaji wenyewe. Haya yote wanaweza kuyafanya bila nyongeza ya Bajeti bali kwa kutumia vizuri zaidi nguvu kazi walijonayo na ya kutosha kabisa. Ubora na *functionality* ya nyenzo zao pia kama vile magari ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aghalabu utakuta magari yao hayana taa (*tail lights* na *head lights*) na pengine wanayatumia hivyo hivyo nyakati za usiku na mchana. Hii inaongeza uwezekano wa kusababisha ajali na kuhatarisha maisha ya raia na wapiganaji wenyewe, mbali ya uharibifu wa vifaa na mali unaoweza kutokea.

Pili, juhudi za Jeshi katika kuendeleza teknolojia zimeendelea kuonekana ingawa bado kuna nafasi kubwa sana ya kuimarisha juhudi hizo ili kuboresha wayafanyayo. Mimi binafsi naendelea kuamini kuwa Jeshi, lilipewa nafasi na kuwezesewa, linaweza kutoa mchango mkubwa katika nyanja mbalimbali za mafunzo na utafiti. Naamini tunaweza kuwa na *centres of excellency* hususan kwa upande wa tiba na teknolojia. Tunachotakiwa ni kupanga kupatia uchaguzi tunaotakiwa kuufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuelezwa na *Military Scientist* mmoja kwamba mpiganaji wetu ana *chance* ya 5% tu ya kupigana vita katika maisha yake kama askari. Hii maana yake ni kwamba, mbali ya kuandaliwa kama wapiganaji wazuri, pia wanaweza kutumiwa kwa shughuli zingine za uzalishaji mali na vile vile huduma mbali mbali kwa viwango vya utaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja ya kulifanya jeshi letu kuwa chanzo cha umahiri katika taaluma mbali mbali, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo (*training*) na utafiti (*research*). Tunachohitaji ni kuwekeza kwao hawa wapiganaji wetu na Taasisi zao, kitu kimoja tayari wanacho, nidhamu ambayo pia huwezi kuimarisha kwa urahisi sana mionganoni mwa wapiganaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza *TATC* (Nyumbu) kwa kazi wanazoendelea kufanya, ikiwa ni pamoja na *proto types* mbili za magari ambayo yameletwa kwa maonyesho leo hii katika viwanja vya Bunge. Tatizo lao kubwa ni *financing*. Kwa mfano, bei ya *proto type trucks* walizoleta ni shilingi 50,000,000/= kwa kila moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika hakuna anayeweza kununuua magari haya kwa bei hiyo isipokuwa Serikali yenye. Serikali iyanunue magari hayo na kuyakabidhi kwa watumiaji walio karibu na *TATC*, kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, ili kutoa nafasi kwa watafiti kuendelea kufuatilia kwa karibu ubora na uboreshaji wa hizo *proto types*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Serikali kuyanunuua magari hayo watakuwa wamechangia katika utafiti wa uendelezaji wa kazi nzuri walizofanya na wanazoendelea kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache hayo, naomba nikamilishe mchango wangu kwa kuunga hoja mkono. Asante.

**MHE. KHAMIS SALUM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya mchango wangu ni kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuliongoza vizuri Bunge letu na pili nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, pamoja na watendaji wake wote ambao wamemsaidia kutekeleza kazi zake nzuri kwa mwaka 2003/2004, pamoja na kutayarisha kitabu hiki cha bajeti kizuri na kinachoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni moja tu, kwa kweli sina budi nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa bidii zako kwa ukarabati wa majengo na Zana za Makambi ya JWTZ, Zanzibar hasa kwa leo nazungumzia kambi ya Hospitali Kuu ya JWTZ, Bububu Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati mzuri unatupatia vizuri, kwa ujumla hali inaridhisha sana kinyume na hapo nyuma ila maombi kwa Mheshimiwa Waziri uone uwezekano wa aina yoyote tupatie kwa wagonjwa na la pili tupatie usafiri wa uhakika kwa Mkuu wa Hospitali hiyo ya Bububu ambaye ndiye Daktari Mkuu Dr. Dalu. Hivi sasa hana usafiri, *Suzuki* aliyonayo ni mbovu sana na hivi sasa imelala na haistahili kupanda Mkuu kama huyo kutokana na juhudzi zako nategemea suala hili utalipa kipaumbele sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri tu ndiyo kilio changu cha leo kwa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Makamanda wote wa Jeshi kwa kazi nzuri ya kusimamia ulinzi nchini. Kwa niaba ya wananchi wa Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe binafsi naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naungana na Kamati ya Ulinzi na Usalama kuwa barabara zote za ulinzi nchi hii ziwe chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, badala ya kuwa chini ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Ruvuma tuna barabara mbili za ulinzi, ya kwanza kutoka Lituhi - Liuli hadi Chiwindi. Barabara hii inapitika sehemu kwa sehemu na kwa tabu na sehemu nyingine hazipitiki kabisa. Barabara ya pili ni Songaa hadi Mitomani nayo ipo katika hali si nzuri, ingefaa barabara zote hapa nchini zingetunzwa mara kwa mara ili ziweze kupitika kwa muda wote wa mwaka, masika na kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jeshi lina wahandisi wengi na wanye uwezo, nashauri Wizara iunde Kampuni ya kutengeneza barabara, kampuni ipewe vifaa vyote muhimu ili waweze kufanya kazi ya kutengeneza barabara hapa nchini pamoja na barabara za ulinzi. Kwa kuwa kampuni ya Meremeta sasa ina uzoefu mkubwa wa mambo ya madini mgodi wa Buhemba ni kielelezo. Kwa mwaka wa kwanza kabisa kampuni imefanya vizuri sana na naamini itaendelea kufanya vizuri zaidi kwa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbinga, Tarafa ya Mpepo ina dhahabu nyingi na hakuna Kampuni yoyote kubwa imeonyesha nia ya kuwekeza katika Tarafa hii ya Mpepo. Kwa muda mrefu wachimbaji wadogo wadogo wanaparuza juu juu tu na hawana uwezo wa kuchimba chini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Kampuni ya Meremeta ielekeze macho na nguvu zake Wilaya ya Mbinga, Tarafa ya Mpepo ili iwekeze huko kuchimba dhahabu kama Buhemba. Tarafa ya Mpepo, Wilayani Mbinga ina dhahabu nyingi sana ni vyema ikachimbwa kwa faida ya maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana naunga mkono tena mia kwa mia.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii ila kuna sehemu moja, moja tu, ningependa kutoa ushauri. Nyumbu, wameonyesha dalili ya kutengeneza gari, *pump* na mashine mbalimbali, hivi hamuoni mkiboresha Nyumbu na kuwaunganishia mafundi wengine ili waweze kutengeneza magari na kuyaboresha nasi tuwe na vyombo vyetu kama ilivyo Japan, China, Korea na kadhalika.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Ulinzi na jeshi la Kujenga Taifa, kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemon M. Sarungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia naomba nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa hotuba yake nzuri ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambayo imeeleweka na pia inatoa nafasi nzuri kwa raia wote kuyaona Majeshi yetu yana kiwango kizuri cha maelewano na wananchi wake. Kwenye hotuba hii nampongeza sana Mkuu wa Majeshi Jenerali George Waitara, Katibu Mkuu wa Wizara Bwana Bernard Mchomvu, Makamanda wote na watumishi wote Wizarani kwa kazi nzuri ambayo imetoa hotuba hii nzuri kwenye Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kutoa pole kwa familia na Ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Yetete Mwalyego na pia Marehemu Mheshimiwa Theodos Kasapira. Pole pia ziwaendee wapiga kura kwenye Majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeridhika kabisa kama maelezo yalivyotolewa na Waziri kwenye hotuba yake juu ya mapungufu ya vifaa na vitendea kazi kwa ajili ya ulinzi wa Taifa. Jeshi lipokee kiasi ambacho kimepatikana sasa. Matumaini yao yawe mazuri kwamba Serikali inafanya juhudhi zote ili tuweze kukamilisha mahitaji yote kwani mpaka sasa Bajeti ya Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa linaboreka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu mpaka sasa ni kwamba Jeshi la Ulinzi na Usalama na Jeshi la Kujenga Taifa ni kwa ajili ya Ulinzi wao. Kwa hiyo, kama Waziri alivyosema, Jeshi letu hili lina ushirikiano na mahusiano ya karibu na wananchi wake. Kwa hiyo, wananchi wa Tanzania wanaishi kwa ukaribu na Majeshi yao. Wapo askari wengi wanaoishi kwenye nyumba za ku-share na wananchi wakati Jeshi lina upungufu wa nyumba kwenye kambi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tukio moja Mwanza ambalo Jeshi letu lilivunja nyumba za wananchi katika Kata ya Isamilo eneo la Nyashana. Kikosi kilicho kwenye eneo hilo kilifanya uvunjaji wa nyumba hizo za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasiliana na Wizara pia na Waziri mwenyewe Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, juu ya tatizo hili ili wananchi hawa watendewe haki ikiwa ni pamoja na kulipwa fidia ya mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu suala la mpaka kwenye eneo hilo kati ya wananchi na Jeshi ulikuwa ndiyo unaandalishi. Na hasa hasa ukizingatia kwamba eneo liko ndani ya mipaka ya Jiji la Mwanza, basi Halmashauri ya Jiji la Mwanza inahusika sana kwenye kuainisha eneo hilo na pia kuweza kulitangaza kwamba ni Jeshi na kuihusisha Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii nitamwalika Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wakati nikimpatica taarifa ya tatizo hili aweze kuja Mwanza, atembelee

eneo hili ikiwa ni pamoja na kuwapa pole wananchi hao waliopatwa na mkasa huo. Jambo hili muda mrefu sasa na nazidi kuomba Wizara ishughulikie tatizo hili. Ninayo imani wakati Waziri akitoa majibu ya hoja hii, pia aniarifu ni lini atakuja Mwanza ili aweze kujiona yaliyotokea na hata pia kuwapa pole wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nitoe shukrani zangu kwa yote jinsi Jeshi letu linavyolinda nchi yetu na hasa hali ya utulivu na amani. Naunga mkono hoja ya Waziri wa Ulinzi na Usalama na Jeshi la Kujenga Taifa kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza na kumtakia afya njema Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nampongeza sana na naomba niwapongeze wafuataao, Katibu Mkoo, Bwana Bernard Mchomvu, Mkoo wa Majeshi ya Ulinzi Jeneral George Waitara, Mkoo wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi, Luteni Jeneral Iddi Gahru na Mkoo wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jeneral David Mwamnyange.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wapiganaji wote Tanzania bila kuwasahau wapiganaji wangu wa Kituo cha mafunzo cha Mikumi. Wapiganaji wangu wa Kituo cha Mafunzo cha Mikumi na Mkoo wao Kituo hiki cha Mikumi ni ukombozi kwa Wanamikumi na Mikoa ya Kusini na nchi jirani kwa misaada ya usalama, hasa kwa majambazi wanaojitokeza Mikumi kutoka pembe zote Dar es Salaam na wengine kutoka Zambia. Hivyo Mikumi ni kituo cha kukutania majambazi, naomba ieleweke kuwa bila kituo cha Jeshi Mikumi hali ingekuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya watu wote wa Mikumi tunaomba sana kituo chetu Wizara isikisahau mara kwa mara katika huduma kwa vijana wetu Mikumi Jeshini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi maalum, kama nilivyojieleza kuhusu kituo cha Mikumi na mara nyingi nimekuwa naeleza kupitia njia ya Maswali yangu kutoka Jimbo la Mikumi. Nimekuwa nikiomba sana ukarabati wa nyumba za kuishi wapiganaji hao zikarabatiwe hatua kwa hatua yaani kidogo kidogo mwanzoni mwa mwezi Julai, 2004 nilipelea barua ya maombi inayohusu ukarabati wa nyumba hizo hatua kwa hatua kwa Mheshimiwa Waziri, sijajibowi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikieleza kwamba hata Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mwenzangu wa CCM amewahi kutembelea na kuziona nyumba hizo na kushuhudia kwamba zilijengwa kwa kutumia miti sasa zimechakaa, zinahitaji kujengwa mpya hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kufika kwake, sasa leo nimeshangaa sikuingizwa kwenye orodha ya ukarabati wa kituo hicho cha Mikumi nategemea wakati wa kujibu hoja atakitaja kituo changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo eneo kubwa ambalo tunalima pamoja na Wapiganaji wetu. Sasa tunaomba tulime zao la miwa kwa kufanya biashara na Kilombero muwa ni zao la muda wa miaka mitano tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea jibu jema. Asante, naunga hoja mkono.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, pamoja na viongozi na wapiganaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nawatakia kila la kheri na nasema naiunga mkono hoja hii. Pamoja na hivyo napenda kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kutokana na uzoefu na uhodari ulioonyeshwa na Wanajeshi wetu katika shughuli za ujenzi wa nyumba za Serikali kwa bei nafuu na wakati mfupi kabisa, bado nina imani kuwa wakati huu wa amani hapa nchini na kwa vile bado kazi za kujenga miundombinu hapa nchini ni hafifu, napendekeza kila inapowezekana basi jeshi lishirikishwe kuendelea kujenga barabara, maji, nyumba na kadhalika. Hii itasaidia sana kusukuma maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kiwanda cha kutengeneza madawa cha *TANZANSINO* kiimarishe ili kiweze kutengeneza dawa za kupunguza makali ya Ukimwi. Suala la Ukimwi ni nyeti sana hasa katika kupunguza nguvu kati ya nchi hii hivyo kila mbinu zitumike kudhibiti hali hii na tatu, napenda kumwarifu Mheshimiwa Waziri kuwa bado kuna tatizo kubwa la Mipaka katika kambi ya Chukwani na wananchi wa eneo hilo. Hivyo naomba Mheshimiwa Waziri tusaidiane, tumalize tatizo hilo kwa usalama kabla hajatokea suala la kuvunjika kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, bado kambi za Chukwani na Kisakasaka zina giza, hivyo naomba sana hili ombi langu la kupeleka umeme huku litiliwe maanani kwa sababu ya unyeti wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, narudia kusema naiunga mkono hoja hii. Asante.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawatakia utekelezaji mwema kwa malengo mloliojivekea kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri kuwa Serikali yenye iwe mnunuzi wa magari yanayotengenezwa. Nyumbu inunuliwe na Serikali, Halmashauri na Manispaa ili wawe na uwezo wa kutengeneza gari nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vyombo vya habari nimesikia kuwa jeshi limetelekeza mabomu! Napenda kutahadharisha kuwa ulimwengu haujawa na amani tangu kuumbwa Adamu na Hawa. Vita vya kulenga ni vya *Habil na Kaini*. Ukisoma *Quran*, Biblia, *ancient* na *modern history* hakuna mahala palipoandikwa Amani, ni vita

tu. Unaweza kuwa mzuri lakini ukashambuliwa na wapenda vita, utajihami vipi? Naona mabomu kama yapo ni kuyatunza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendea kazi nya ulinzi sharti vitunzwe vizuri maana huwezi kujua ni lini balaa la vita litatokea. Vifaa nya Jeshi huko *Old Shinyanga* sharti vitunzwe vizuri kwa kukamilisha maghala yaliyoachwa bila kujengwa. Pia nyumba za wapiganaji kule kambi ya *Old Shinyanga* na Kizumbi sharti zijengewe ama zile mbaya zikarabatiwe maana zina hali mbaya sana. Pia vitendea kazi nya ulinzi na mikopo kwa wapiganaji viende.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakiwa kila la kheri katika kutekeleza malengo mliyojiwekea kwa kuboresha ulinzi wa nchi yetu.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hoja hii ya Makadirio na Matumizi ya Jeshi la Ulinzi na la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze Wizara hii kwa kuipatia hospitali ya Bububu ambayo ipo katika jimbo langu la Mfenesini, lakini pamoja na hilo naiomba Wizara iendeleze kwa kasi ukarabati wa maeneo mbalimbali katika hospitali hiyo ya Bububu kwani ni hospitali ambayo inategemewa sana na wananchi wote wa Zanzibar wakiwemo viongozi wa Kitaifa.

Lakini kubwa zaidi ni kuboresha chumba cha upasuaji ambacho nahisi kinahitaji marekebisho ya haraka, hii ni pamoja na njia iendayo katika hospitali hii muhimu ambayo labda itakuwa na urefu wa kilometra moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sina fadhila bila kuwasifu Madaktari wote wa Kituo hiki cha Bububu kwa uandilifu wao katika kutoa huduma kwa wagonjwa hasa Dr. wao kiongozi *Dr. Lt. Col. Dalu*, pamoja na manesi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishauri Wizara hii kukiboresha kikosi cha *Navy Kigamboni* hasa ile *workshop* ambayo ni tegemeo kubwa sana katika kutoa huduma mbalimbali za uzalishaji wa *spare* pamoja na utengenezaji wa kutoa huduma kwa meli ndogo ndogo kwa kuboresha chelezo chao cha huko Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningeishauri Wizara hii itilie mkazo sana suala la michezo kwani bado jeshi lina nafasi kubwa ya kuchukua sifa zote za ushindi kuanzia *Marathon*, Mipira ya aina zote na kadhalika hii ipewe nafasi kipekee kwani nidhamu iliyojaa jeshini hakuna sababu kwa nini Klabu bingwa ya mpira wa miguu isiwe *Jeshi Sports Club* na kumaliza utata wa Timu nyingine za uraiani na bado Jeshi likarudisha hadhi ya akina Philbert Bayi. Naomba Jeshi hivi sasa litangaze *operation michezo*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza Jeshi kwa jumla yote kwa ushupavu ulioonyesha katika ujenzi wa nyumba za Serikali, naomba sana Serikali isisite kutoa

nyenzo zote wanazozihitaji ikiwemo fedha ili tusije tukaliingizia dosari jeshi hili katika utekelezaji wa shughuli zake za ujenzi wa nyumba hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshauri Waziri aanzishe uwakala wa kuratibu wa kutoa huduma kwa Waheshimiwa Wabunge katika kununua silaha katika Ofisi yetu ya Bunge pamoja na kutupatia wataalam wa kutoa darasa la namna gani silaha inahitaji kuhifadhiwa kwa usalama wetu na familia, hii inaendana na kulishukuru jeshi kwa fursa iliyotupa kwa upigaji shabaha kitu ambacho tumefuzu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kulipongeza Jeshi kwa unadhifu wa mavazi kuanzia Makamanda Wakuu hadi askari wa kawaida, hii inaonyesha kuwa kioo chetu kinang'ara katika kiwango kinachotakiwa Kimataifa na nawapongeza sana askari wa kikosi cha *MP* kwa huduma zao wanazosaidiana na *Traffic Police* wakati wa ajali za barabarani hasa *Morogoro road* kwa kutoa ulinzi wa uhakika. Jeshi lihakikishe usafiri unaboreshw, askari wake hatupendi wapande daladala. Ahsante.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Makamanda wote kwa kazi nzuri za Ulinzi na Usalama wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja na maombi yao yote wapewe. Nisisitize kuwa jeshi linapaswa liaminiwe na hivyo bajeti yao iongezewe pesa ili liboreshe huduma zake za ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maoni yangu katika Wizara hii kwa jeshi la baadaye liweje ili kujenga jeshi imara ni vyema shule zetu za msingi zinazomilikiwa na jeshi ziimarishe kwani vijana wanaosema katika shule hizo huwa na maadili ya kijeshi. Vile vile shule za sekondari zilizopo zipatiwe vifaa ili kuboresha elimu ya watoto wa wanajeshi wakiwemo watoto wa wananchi kwa ujumla shule hizi zinahitaji kuboreshw zaidi ziwe za mfano kama zilivyo shule za *mission*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi ni watumishi wa saa 24 hivyo iwapo watoto wao watapata elimu nzuri katika mazingira mazuri itakuwa ni motisha kwao lakini pia watoto hao ndiyo walinzi wa Taifa la kesho hivyo shule za sekondari za Jeshi ziimarishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema pia tukaimarisha pia huduma za afya kama ilivyo kwa baadhi ya Kambi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuwapongeza wapiganaji wetu Mungu awalinde. Naunga mkono hoja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katibu Mkuu wa Wizara na Makamanda wote wa Majeshi yetu kwa kazi nzuri ya ulinzi na pia kwa hotuba hii nzuri ya bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuridhika kwangu kuhusu utendaji mzuri wa kazi zao, nasikitika kusema kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu ya makazi na vitendea kazi hasa usafiri. Nashukuru kwamba wenzetu wa Nyumbu wanajitahidi kuonyesha ustadi wao katika ujenzi wa magari ili hatimaye teknolojia hiyo ipunguze matatizo ya usafiri jeshini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi na nyinginezo katika sekta ya afya, Bunge kama nguzo ya tatu, haina budi kutamka kwamba hivi sasa Jeshi letu halina zana za kisasa za kupigana na maadui. Itakuwa ni hatari sana kama nchi hii itashambuliwa kwa anga na majini, tunaweza tukaangamia upesi kwani ingawa tuna Wanajeshi wazuri, lakini hawana zana. Hebu fikiria leo katika Bajeti tunanunua helikopta mbili ambapo wenzetu Malawi wana helikopta za kijeshi zaidi ya 30. Burundi na Rwanda wana ndege za kivita zaidi ya tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii isiendoolee kwani mbele ya safari kunawenza kuwa na hali mbaya kwetu kiusalama. Ifike mahali tuwe na jeshi linaloweza kuangamiza adui kabla hajafika nchini kwetu (*pre-emptive strike*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba moyo huu wa kujitolea uendelee lakini tuwe na *vision* ya namna gani tuataweza kujilinda siku zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Katibu Mkuu, Bwana Bernard Mchomvu, Makamanda, wapiganaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii, Majeshi na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii kwa hotuba nzuri na kazi nzuri za ulinzi na usalama pamoja na huduma nyingi nyinginezo kwa jamii kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri mengi, ningependa kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Ulinzi Mipakani, nafarijika kwa jitihada zinazofanywa kuimarisha ulinzi mipakani. Hata hivyo, ipo haja ya kuwa makini na kutopuuzia maeneo ambayo yanaonekana tulivu na yenye amani na usalama kwa hivi sasa. Mfano hai ni Mpaka wa Kaskazini Mashariki. Pamoja na hali ya utulivu iliyopo sasa, hii si dhamana (*guarantee*) ya hali ya utulivu iliyopo sasa daima na hivyo hatuna budi kuwa macho na imara kwa upande huo kama ilivyo kwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, doria ya Baharini na Maziwani, inafurahisha na kuleta matumaini mapya, tatizo hili sugu linatazamiwa kupatiwa ufumbuzi mwaka huu. Uvamizi, uharamia, uvuvi haramu na maovu yanayoweza kuiletea athari kubwa iwapo tutaendelea kuacha mipaka yetu ya baharini na maziwani bila ulinzi wa kutosha. Hivyo uimarishaji wa doria baharini na maziwani ni hatua inayostahili kupewa kipaumbele maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, barabara za mipakani, hali nzuri ya barabara za mipakani ni muhimu, kwa hili nashauri barabara za mpakani za Horohoro hadi Mwakijembe na kwa upande mwingine barabara itokayo Horohoro hadi Jasini ziwe chini ya uangalizi wa Jeshi. Vivyo hivyo napendekeza kwamba barabara itokayo Dahuni hadi Mwakijembe nayo ipewe kipaumbele maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne hali maalum ya Maramba na vijiji vya jirani. Kwa kuwa Kijiji cha Maramba na vijiji vya jirani kimezungukwa na misitu ya Akiba (*forest reserve*) na mashamba ya Mkonge ya mbegu na ya JKT vijiji vingi vya Tarafa ya Maramba havina ardhi ya kutosha kwa ajili ya kilimo na ufugaji. Hivyo, pamoja na azma ya kuzuia wananchi wasilime katika maeneod ya Jeshi, nashauri wananchi wanaoishi karibu na Jeshi la Kujenga Taifa Maramba waruhusiwe kulima mazao yasiyo ya kudumu katika mashamba ya JKT kwa utaratibu na udhibitit maalum. Vinginevyo, wananchi wa maeneo hayo watakwama katika jitihada za kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano napongeza jitihada zinazofanywa kuyapatia Majeshi yetu vifaa, nyumba na mahitaji mengine muhimu. Haya, pamoja na kuboresha namna ya kuwapandisha vyeo na mishahara na pia motisha nyingine ni muhimu sana kwa kukuza morali, nidhamu na utendaji bora. Haya ni muhimu sana vile vile taratibu nzuri za malipo ya pensheni na kuwatunza askari wastaifu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kabla ya yote nimpongeze Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na Wapiganaji wote wa vikosi vyote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutulindia nchi hii. Naunga mkono hoja hii asilimia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Wizara ya Ujenzi ili kutekeleza ombi letu la zamani katika Mkoa wa Rukwa na nchi yote, kuwe na uhakika wa uimarishaji wa barabara za mipakani. Jeshi la Wananchi kwa kutumia kitengo chao cha Uhandisi wangeweza kupewa jukumu hilo la kuzitambua na kuzisimamia katika kuzijenga. *Field Engineering Units* zingeweza kuzifanya kazi hizi kama watapewa fedha na vifaa. Usalama wa nchi unategemea sana jinsi barabara hizi zinavyotunzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu la pili ni kuiomba Wizara iimarishe mafunzo ya mgambo kwenye Wilaya zetu za mipakani. Mafunzo yaambatane na upatikanaji wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya *patrols* na pia kwa ajili ya mambo ya dharura. Mpaka

wetu na *DRC* unahitaji pia zana za kusafiria na kufanya doria kwenye Ziwa Tanganyika, ili wananchi wetu wasibughudhiwe na askari wanaokimbia mapigano kwenye nchi zao.

Nashukuru jeshi letu kwa kuimarisha mafunzo kwa wapiganaji wetu wa ngazi zote. Nashauri hiyo iende sambamba na kuendeleza teknolojia ya kisasa jeshini katika nyanja zote zikiwemo za kuimarisha kikosi cha kutengeneza magari na mitambo mingine. Nawapongeza Nyumbu kwa hatua hii ya kwanza nzuri ya kutoa magari ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya vijana wanaojiunga na JKT yaendelezwe kwa kasi ili tuwajenge kimaadili, kifikra, kiuchumi na kiukakamavu. Tuwafundishe zaidi njia za kuendesha biashara ndogo ndogo. Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, wasaidiwe mikopo midogo ya kuendeshea maisha yao na hili lingeweza kwa kuanzia tukawa na vijana wale tu watakaoonekana wanafanya kazi zao vizuri wakiwa kambini ili wanapohitimu, wapewe vifaa vyatupu kujidesha wenyewe. Mfano kwa wale wa useremala, uashi na kadhalika wangepeewa vifaa kwa kushirikiana na *VETA* Makao Makuu, watoe zawadi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja yote ya Wizara hii *and keep it up.*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia Majeshi yetu kwa amani na utulivu ndani ya nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nachukua nafasi hii kumpogeza sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Philimon Sarungi, hana Naibu Waziri lakini Wizara nzito iko shwari kabisa Mheshimiwa Waziri anafanyakazi nzuri ni kweli askari wa mwavuli, sisi Watanzania na hasa wanawake wote, tunaungana nae kwa kuhakikisha amani inakuwepo daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Tanzania la Ulinzi linafanya kazi nzuri sana, Makamanda wote hasa walioko vikosi vyatupu majini, lakini bado majambazi wanatuzidi ujanja, nashukuru Bajeti ya mwaka 2004/2005 itanunua boti za kupamba na hawa majambazi sehemu za Chifufu, Sengerema, Ukara, Ukerewe na maeneo mengi yanayozungukwa na Maziwa na bahari, tutashukuru sana kama askari wakisaidiana na raia wema hali hii ya wasiwasi itakwisha. Tunaahidi wanainchi watashirikiana na askari wetu katika kulinda usalama wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mbali ya kuwepo na kuratibu maeneo ya Ziwanu, pia tuisahau maeneo ya misitu iliyopo Wilaya ya Geita ili majambazi wasiendelee kupora raia wema na kuteka nyara magari na mabasi ya raia wema, jeshi lisaidie kuratibu katika misitu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri kuona umuhimu wa kuwa na jeshi dogo la ulinzi, lenye wakala waliofuzu vizuri na lenye zana na vifaa vyatupu kisasa, napenda niombe sana imefika wakati kwa kuwachukua wanafunzi toka shulenii moja kwa

moja hasa *Form IV* na *Form VI* wenye sifa za kijeshi, si kuchukua tu, hii itasaidia sana vijana wetu wasiendelee kukaa bila shughuli baada ya kumaliza elimu za sekondari, nafasi ya kuwapeleka Chuo Kikuu na Ualimu hazitoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumwombe sana Waziri asaidie hili. Tunashukuru kuwa tuna viwanda viwili tu vya kushona sare za jeshi navyo ni Ruvu JKT na Mgulani JKT. Viwanda hivi havitoshi ukizingatia mahitaji ni mengi, mbaya zaidi katika ukurasa wa 11 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema inabidi waagize nje ya nchi ili kuziba pengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari, kuagiza sare nje, inawapa mwanga wale majambazi kutumia viwanda vya nje kwa kushona sare hizo, zikiigizwa na wajanja zije zitumike visivyo, nitamwomba sana Waziri aweke udhibiti mkali, lakini bora zaidi ni ufanyike ujenzi au upanuzi wa viwanda vyetu humu humu nchini huu ndiyo usalama wetu wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, majambazi siku hizi wanavaa sare za askari wetu na wanasimamisha magari na uporaji unashamiri.

Tunashukuru kwa kufanya zoezi la kupima maeneo ya Jeshi, imekuwa kero baina ya raia na Wanajeshi na silaha zinatumika, inapunguza sifa tuliyonayo, Watanzania damu inamwagika, si vyema sana wananchi waelewe mipaka yao na Wanajeshi wawe na mipaka yao kisheria, naomba wamalize zoezi hili mapema na matangazo yatolewe kwenye Magazeti na raia wajulishwe. Tabia hii tukiendelea kuwa nayo tutafanya uadui kati ya Wanajeshi na Watanzania waishio karibu na makambi yote ya jeshi.

Sisi wazazi wa vijana waliopelekwa katika kambi za Makutupora, Oljoro na Ruvu, tunashukuru sana vijana wetu wana afya nzuri na waendelee vizuri na Serikali yao imewawezesha kuwapa mafunzo ya kilimo na mafunzo ya ufundi. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri katika hili ni jambo jema kwa vijana wetu tunaomba autaratibu huu uendelee miaka yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Waziri kuona umuhimu wa kujenga Mnara wa Makumbusho ya mashujaa hapa Dodoma, Makao Makuu ya Chama na Serikali, kwa kuona umuhimu wa kumteua Mheshimiwa Jackson Makwetta, kuratibu mpango huu. Hii ameonyesha jinsi ya kuwatumia Watanzania hasa Wabunge wenzetu kuwa waratibu wa maamuzi ya Serikali, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jackson Makwetta, tunamwomba aratibu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lipitishe makisio haya na naunga mkono hoja, Waziri apewe na aongezwe zingine hazitoshi. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuanza kumpongeza Waziri huyu kwa hotuba nzuri na kwa kweli kwa kusimamia vizuri Wizara

hii. Naomba niwapongeze wapiganaji wetu wote wakiongozwa na Jenerali George Waitara kwa kazi nzuri ya ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali kwa kuendelea kuwawezesha wapiganaji wetu kwa hali na mali. Rai yangu ni kwamba juhudhi hizi ziongezwe ili Jeshi letu liwe la kisasa. Bila kuwapa vitendea kazi vya kisasa tutakuwa hatuwatendei haki ndugu zetu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iifufue Kambi ya JKT ya Masange ili iweze kutusaidia wananchi wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kuona katika ukurasa wa 13 wa hotuba ya Waziri kuwa hospitali ya Mirambo, Tabora inategemewa kunufaika katika msaada wa ukarabati wa *GAFTAG* kutoka Ujerumani. Naipongeza sana Serikali kwa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iwakumbuke wapiganaji kwa kuwapa posho zao zote kwa muda muafaka na kuwakumbuka katika kuwapandisha vyeo. Naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, Katibu Mkuu, wafanyakazi na wapiganaji wote wa JWTZ na JKT kwa kazi nzuri na ufanisi waliyoifanya mwaka 2003/2004. Hongera sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja bila tatizo lolote. Aidha, napenda na naomba Waziri azingatie yafuatayo katika mwaka 2004/2005 nayo ni haya:-

Kwanza, uimarishaji wa vikosi vya mpakani, ni vyema vikosi vilivyoko mpakani vikaimarishwa zaidi kiteknolojia, kimawasiliano na kimaslahi na kuviungezea idadi ya wapiganaji. Maeneo ya mpakani Mkoani Kigoma muda wote yako hatarini kuvamiwa tokea Kongo na Burundi hasa kutokana na waasi toka nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ya simu na barabara za kupitika mwaka mzima ni muhimu sana endapo vikosi hivi vitalazimika kuingia kazini *in action*. Aidha, boti za kisasa kidoria Ziwanu Tanganyika ziongezwe ili kupambana na ujambazi na kuungeza doria kwa manufaa kiulinzi, kiusalama na kiuchumi kwa wakazi wanaotegemea Ziwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu nyumba kwa wanajeshi wastaafu. Naishukuru Serikali kwa kuwaandalia wafanyakazi wa Serikali nyumba za kuishi ambazo wanaruhusiwa kuzinunua ili wanapostaafu wawe na mahali pazuri pa kumalizia maisha yao. Mimi ningeshauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwajengea na kuwauzia nyumba Wanajeshi ili wanapostaafu wawe na makazi bora kuliko hali ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona ni kheri kabisa Wanajeshi wakakopeshwa nyumba kuliko vyombo vya usafiri kama pikipiki na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi zaidi za JKT zifunguliwe. Naomba kambi nyingi zaidi ambazo bado zimefungwa zifunguliwe ili vijana wengi zaidi wapate mafunzo ya JKT kwa lengo la kukuza uzalendo, nidhamu na umoja miongoni mwao. JKT ni chombo muhimu sana kwa taifa letu kiusalamu, kiulinzi na kiuchumi. Sisi tuliobahatika kupita JKT miaka ya nyuma tulifaidika sana na mimi ninaamini kabisa kwamba ni vyema kila kijana wa Tanzania kupata mafunzo haya. Pale bajeti yetu inaporuhusu kambi zaidi zifunguliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu kwa kurejesha tena utaratibu wa vijana kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Jeshi hili ni muhimu sana katika kujenga umoja wa Kitaifa na katika kuwaandaa vijana kwa maisha katika Taifa la Kitanzania. Hatua ambayo haijachukuliwa ni ile ya kurejesha utaratibu wa vijana wasomi kupitia Jeshi la Kujenga Taifa. Vijana hawa wanahitaji kujengwa ili wawe na uzalendo wa kweli na kama wenzao, ili waandalie kwa maisha katika Taifa la Kitanzania. Upungufu huu ni sharti uondolewe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu kilimo. Yapo mambo mawili yanayohusu kilimo, kwanza, ni umuhimu wa kuwafundisha vijana wanaopita Jeshi la Kujenga Taifa kilimo cha kisasa ili wakirudi makwao waweze kujajiri katika kilimo na wakati huo huo wawe kiini cha kilimo cha kisasa katika vijiji vyao. Wizara ya Kilimo na Chakula, ipo tayari kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa kutekeleza programu ya mafunzo ya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni umuhimu wa Jeshi la Kujenga Taifa kuzalisha mazao kwa wingi ili kujilisha na kujiongezea kipato. Hadi miaka ya 1980 baadhi ya makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mfano Mlale, Mkoani Ruvuma, Oljoro, Mkoani Arusha na kadhalika yalikuwa na sifa ya kuzalisha mazao ya kilimo kwa wingi na ubora wa juu sana. Aidha, baadhi ya makambi yalikuwa na ufugaji kwa mfano, Mafinga, Mkoani Iringa. Sifa hizi zimepotea na ni wakati muafaka kuchukua hatua za kurejesha sifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kikubwa na cha kisasa kitahitaji nyenzo bora kama matrekta na vifaa vyake na zana nyingine za kilimo. Nashauri kwamba Jeshi la Kujenga Taifa washirikiane na Wizara ya Kilimo na Chakula, kuandaa programu kubwa ya kilimo ambayo itatafutiwa mahitaji ya kuitekeleza. Hili ni jambo la haraka na muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo hicho kikubwa kitatumwa kuwafundisha vijana kilimo cha kiuchumi na kwa kufanya hivyo, kuua ndege wawili kwa jiwe moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuunga mkono hoja, sasa twende kazini.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuchangia kwanza kwa kuwapongeza, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemont Sarungi, kwa jitihada zake za kuinua utendaji wa Wizara hii muhimu, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizara hii muhimu , Katibu Mkuu na watendaji wote Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mkuu wa Majeshi na Wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, amani inayoonekana ndani ya nchi hii ni kwa mchango wao mkubwa wa kizalendo wanaoutoa, tunaomba waendelee kutekeleza majukumu kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba kusimamia mbali ya majukumu walijonayo wajitahidi haya yafuatayo yatekelezwe:-

Kwanza wakati huu tunajielekeza na Uchaguzi wa mwaka 2005 kuimarishwa ulinzi wa makusudi, Pemba Wilaya ya Kaskazini, Micheweni, Msuka na Mazwa ng'ombe. Hizi ni sehemu ambazo zina mawasiliiano ya karibu na Lamu, Somalia na Mombasa. Kuna dhana ya kuwa baadhi ya mabomu yanapitishwa maeneo hayo na baadaye kulekwa Unguja kupitia bandari ya Nungwi, Tumbatu, Fukuchani na kadhalika.

Pili, ujenzi wa hospitali ya Bububu, kituo hiki baadaye kiasiwi ili kwanza kutoa matibabu kwa Waheshimiwa hasa wanasiwa. Hali ya hospitali ya Mnazimmoja siyo ya kuaminika kwa wanasiwa wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na kujishughulisha na mafunzo mbalimbali, ningeshauri wakajielekeza zaidi katika kilimo, wakapata fedha na vifaa vyta kilimo ili kuijendeleza na kilimo cha kibiashara na siyo cha chakula tu na baadaye kiwe ni kitovu cha ajira kwa kusaidiana na Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyumbu inaweza kutengeneza si magari tu, bali matrekta madogo madogo ya mkono ya kulimia na yenye bei rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasaidiwe kwa kujenga nyumba za kuishi ili baada ya kustaafu wawe wanapo pa kuishi badala ya kuyumba yumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nashauri wanajeshi wastaafu hasa wale wenye vyeo vyta juu watengenezewa majengo baada ya kustaafu kurahisishiwa maisha yao. Kazini wao ni hazina kubwa ya nchi hii na kwa nyakati huwa wanakuwa na vyama vyta siasa (wanaodhaniwa vibaya) kuharibu majengo ya usalama nchini. Ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nichangie hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na watendaji wote kwa kuanda hotuba hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Lakini kwa lengo la kuboresha, napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Hali ya Jeshi letu kifedha bado hairidhishi hasa ikizingatiwa kuwa baada ya ushindi wa kumwondo Dikteta Idd Amin, tuliridhika na ushindi huo na kutelekeza baadhi ya vikosi hususan kikosi cha majini (*Navy*) nashauri Serikali iangalie vipaumbele vyake ili kuweza kuimarisha vikosi ya majini ili kulinda maeneo ya mipaka yetu ya bahari, Maziwa hasa Tanganyika na Nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huu wa amani, Jeshi letu lingejihuisha zaidi katika kuendeleza teknolojia kwa mfano, Shirika la Nyumbu litengeneze magari ya kutosha na kwa kuanzia mtumiaji wa kwanza liwe Jeshi lenyewe. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge nao waanzishe uzalendo wa kununua magari hayo. Ili kuvutia soko la magari ya nyumbu kodi zote ziondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kasi ya kukarabati makambi ya JKT iongezwe ili kuongeza idadi ya vijana wanaojiunga na JKT. Napongeza sana kwa kazi nzuri inayofanywa na kikosi cha ujenzi cha JKT kwa uwezo wao wa kkujenga nyumba za watumishi wa Serikali. Lakini haifurahishi unapoona wapiganaji wanavyoishi kambi ya Lugalo kambi hiyo ni historia ya Jeshi na pia ni kioo cha Jeshi la wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kambi hiyo iko mjini kwa nini Serikali isichukue hatua ya kujenga upya kambi hiyo ili kuwapa askari wetu maisha mazuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni kuipunguzia hadhi Kamati ya Ulinzi na Usalama kama itakapotembelea tena itakuta hali kama ilivyo kuwepo. Ni matumaini yangu kwamba Kamati itakapotembelea itakuta kambi ya Lugalo imejengwa upya kwa lengo la kulinda historia ya kambi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Spika, mwisho naipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kuirejesha miili ya mashujaa waliokufa huko Msumbiji. Ni matumaini yangu kuwa zoezi hili litakamilika kabla ya awamu ya tatu kumaliza muda wake.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na inayoleta matumaini, pongezi kwa watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya. Nampongeza Mkuu wa Majeshi yote mawili JWTZ na JKT. Vivyo hivyo ninampongeza mkuu kwa kuboresha mazingira ya makambi yetu hasa kwa kutenganisha makazi ya watu na mifugo. Nampongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu liko katika hatua ya mpito na linajionesha dhahiri kwa shughuli zinazofanyika. Jeshi katika kipindi hiki cha amani kushughulikia masuala ya huduma za jamii na kiuchumi ni kuliwekea thamani ya wazi Jeshi letu mbele ya macho ya wananchi na kuiondoa pitcha pekee ya jeshi kuwa wao ni wapiganaji tu na kuwa shughuli zao ni wakati wa vita na wakati wa maafa mbali mbali ya kitaifa wanapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilipongeze jeshi kwa shughuli mbalimbali za kijamii huduma linazozifanya. Shughuli hizi ni pamoja na huduma za afya katika hospitali zake ambazo zinahudumia si wajenzi tu bali na kwa raia pia. Kwa vile hospitali zimekuwa na mvuto mkubwa kwa wananchi ni vyema kwanzza Madaktari na wataalam wengine wakaongezwa na pili, vifaa viongezwe katika hospitali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile hospitali hizi zinapokea watu wengi wanaoathirika viungo mbalimbali kutokana na mazoezi na aina ya kazi zao. Wataalam wa viungo (*Physiotherapist*) ni vizuri wakaongezwa na wakawa mara kwa mara wanapatiwa mafunzo ya kuinua viwango vya taaluma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mashambulizi ya mara kwa mara katika Ziwa Victoria na hisia ya wananchi wanaokaa katika maeneo hayo wanahisi matatizo haya yanasaababishwa na watu kutoka nje ya nchi, nashauri Jeshi letu mara moja kuwa linafanya *operation* za kustukiza ili kulisaidia jeshi la polisi linaloonekana kuzidiwa katika kudhibiti katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa niaba ya wananchi na wapiga kura wa Jimbo la Kwimba na kwa niaba yangu binafsi, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBET J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, uongozi na wapiganaji wote kwa kazi nzuri ya ulinzi wanayofanya Kitaifa na jinsi wanavyosaidia Jeshi la Polisi nchini kupambana na ujambazi wa kutumia silaha katika maeneo ya mipaka na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba kuelekeza mchango wangu katika maeneo yafuatayo kuhusu Kambi nyingi za Kijeshi kuwa ndani ya miji na karibu na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukua kwa miji mingi, kambi za kijeshi zilizojengwa miaka ya 1961 hadi 1980 katika maeneo kwa wakati huo, yalioneckana kuwa mbali na miji na makao ya wananchi. Sasa zimegeuka kuwa ndani ya miji na kuzungukwa na wananchi na hivyo kufanya kazi za mazoezi kwa wanajeshi kuhatarisha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inaona hali hii kuwa ya kawaida au ina mpango gani kuhusu kambi hizi na mpango wa ujenzi wa kambi mpya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maonyesho ya mazoezi ya kijeshi kwa raia. Miaka michache iliyopita hasa wakati wa sherehe za Kitaifa, mara chache Jeshi la Anga lilikuwa likionyesha maonyesho ya ndege za kijeshi kwa raia katika gwaride maalum. Mazoezi hayo hivi sasa hayaonekani au kuwepo kwa nadra sana. Tunalipongeza Jeshi letu kwa jinsi lilivyofanya vizuri katika mazoezi na maonyesho huko Zambia kama tulivyoelezwa katika hotuba hii.

Je, ni lini Watanzania nao watapata nafasi ya kuyaona Majeshi yao katika mazoezi? Wananchi wa Wilaya ya Tanga na jirani zao walifurahishwa sana na mazoezi kama hayo yaliyojumuisha Jeshi letu na Majeshi ya nje, ikiwemo Ufaransa mwaka 2002/2003. Hivyo wananchi wengine pia wana hamu ya kuona mazoezi kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Naibu, kuhusu mgogoro wa mpaka kati ya Jeshi na wananchi katika eneo la Shule ya Sekondari ya Wananchi Songa, Kata ya Songa. Ninaomba kujua hatma ya mgogoro mdogo uliojitokeza katika Kata ya Songa, ambapo viongozi wa Kambi ya Jeshi Songa walidai kwamba Shule ya Sekondari ya Wananchi Songa imejengwa ndani ya eneo la jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na barua niliyoandika yente *Ref. No. MB/JMH/JWT/SSN/2110/VOL.01* ya tarehe 8 Machi, 2002 Jeshi halijatoa tamko rasmi juu ya eneo la mipaka yake na hatma ya shule hiyo ta Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shule hiyo iko katika eneo ambalo hata watoto wa wanajeshi wangeweza kunufaika na elimu itakayotolewa, niliomba Jeshi lisaidie katika kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa shule hiyo. Ukimya wa Jeshi katika kushiriki katika kazi hiyo, kunawatia mashaka wananchi juu ya hatma ya shule yao, licha ya wananchi hao kuendelea kujenga vyumba vipyta vinne vyta madarasa na vyoo kwa mradi wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, awaondolee wananchi wasiwasi na hivyo kuandaa kupima eneo hilo ili mipaka ya eneo la Jeshi ifahamike vizuri kwa lengo pia la kusaidia wananchi wema wasiingie kwa kutojua ndani ya eneo la Kambi ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima naomba uniruhusu na mimi nichangie kwa maandishi kwa Wizara hii muhimu sana kwa uhai na ulinzi wa nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii ni miongoni mwa Wizara ambazo zimepata bahati ya kiongozi ambaye tokea akiwa hospitali (akiwa Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa), alionyesha kukomaa kwake katika hali ya kuokoa maisha ya wananchi, kuwaondolea mateso na maumivu, aliithibitishia Tanzania kuwa

ye ye ni mpiganaji wa mstari wa mbele wakati wa janga la Iddi Amin Dada alipoivamia Tanzania na kuwaua watu wengi na wengine kuwaumiza na kuwaacha hospitali kwa kuwafuata wapiganaji wetu mstari wa mbele. Huyu ni Waziri na kiongozi jasiri wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hotuba hii kwa ukamilifu yaani kwa asilimia mia moja. Nimeamua kuunga mkono hotuba hii kwa kila sababu, kwani mionganoni mwa mambo ambayo yamekuwa yanawapa shida Wanajeshi wetu ni kuwa na viongozi wenye taaluma ndogo ya fani ya utawala kwa ujumla wake. Sasa nimeridhika sana kuona mfumo mzima wa utawala unaoendeshwa kwa mwelekeo wa Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika ni budi kukubali ukweli wakati wote mambo yanapofanya vizuri na hasa kwa kuwa hii Wizara inaendeshwa kwa mfumo wa nidhamu ya juu sana. Aidha, pale kidogo panapohitaji kuelekezana, basi ni budi tusichelewe kufanya hivyo. Mimi naomba maelekezo kutokana na utaratibu wa huduma za tiba kule *Bububu Hospital*, unaoangaliwa na Wizara hii.

Hospitali za Jeshi duniani kote na hapa Tanzania Bara, zinakuwa ndiyo bora zaidi na salama zaidi na pia huwa zina maumbile ya hospitali nzuri sana. Nimekuwa kwa muda mrefu naiangalia Hospitali ya Bububu kama kituo kidogo cha afya (*Health Centre*), kwani majengo yake bado hayajanitosheleza kuiona hospitali yenye hadhi ya Jeshi kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado Wizara ina wajibu wa kuikuza hospitali hiyo kuanzia ujenzi yake na pia taaluma ya Madaktari wake, hasa kwa kuwa sasa ni tegemeo la wananchi wengi wa Zanzibar yaani Unguja na Pemba. Pale ni lazima tuwe *Consultants, General Practitioners* na kiwango cha taaluma za juu kwa Wauguzi, *Laboratory Technologists* na fani zote *supportive*. Si busara kwa hospitali kama ile kuona *surgeries* zinafanywa na mwenye fani chini ya Digrii ya *Medicines* au kutegemea *Medical Assistants* wenye uzoefu wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Udaktari unakuja kwa kusoma vizuri, kufaulu mitihani na ndipo hata matibabu yake yanapoaminika na kutumainika. Namwomba Mheshimiwa Waziri atuonee huruma wananchi tunaoutumia na kuiamini hospitali hii, kwani nina hakika sana kuwa Serikali ya Zanzibar inapata msaada kwa kuwa ni kituo muhimu kwa kuisaidia hospitali yetu ya Mnazi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa tunazona juhudzi za kuinua hadhi ya hospitali hiyo, naomba tena kuwa bado tuendelee kwa kufanya jitihada za makusudi kuongeza Madaktari na Wasaidizi wao kwa kusomesha *Qualified Nurses* badala ya utaratibu wa kuwa watumishi wanaopata *crush programmes* pamoja na maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na hali ya viongozi wa *brigade* mbalimbali za Tanzania, nadhani Nyuki ina kazi nyininge ya ziada, kwani ile ina jukumu la kuiona Zanzibar kwa ukamilifu wa visiwa vyetu vyote viwili yaani Unguja na Pemba. Naishukuru sana Wizara kwa kutuletea viongozi wanaopenda Zanzibar na wao wamependwa. Ni kitendo kizuri kuona kila wakati wa Bunge la Bajeti, basi Brigedia

Jenerali wa Nyuki awepo Bungeni, kwani pale ni mahali pa kuonyesha uwakilishi wa Nyuki kama anapokuwa anahudhuria mambo mengine ya Taifa sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza hili kwa maana ya kuwa mambo yanayohusu Zanzibar, yanamgusa yeye na ni vyema inapotajwa mambo yake, basi aonekane na awaone wanaomsaidia. Nimekuwa sifurahishwi na hali ya Kituo cha Afya cha pale Migombani karibu na Makao Makuu ya *Nyuki Brigade*.

Kwanza kipo njiani na kabisa hakitoi sura ya Jeshi letu lilivyo, kwani JWTZ ni nadhifu. Nashauri sana kituo hicho kuwekwe Kituo cha Jeshi na kiwe na wataalam wanaolingana na hadhi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze wote wanaosaidia Jeshi letu la Kujenga Taifa kwa ushirikiano wao na JKU, Zanzibar kwa namna wanavyofanya kazi zao. Nawaomba sana waimarishe maingiliano na kutembeleana kwa kubadilishana wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii na naomba sana wapewe fedha zao zote kwa wakati.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Kujenga Taifa kwa hotuba yake nzuri na kazi nzuri ambayo amekuwa akifanya vizuri, pamoja na kazi nzuri za wapiganaji Wanajeshi na wataalamu wote walioko katika Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nawapongeza sana kwa mshikamano, moyo na ubunifu mzuri wanaoufanya naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi moja tu la kujua umri unaotakiwa kwa vijana wanaotakiwa kuijunga/kuajiriwa na Jeshi la Kujenga Taifa au Jeshi la Ulinzi. Wilaya ya Mbarali lina vijana wengi waliomaliza *Form IV* au *Form VI* wana umri kuanzia miaka 24 na kuendelea kitu ambacho kimekuwa kikwazo kikubwa kwao kutoajiriwa kwa madai ya kuwa na umri mkubwa mara ajira zinapotokea, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kujua ni vipi tutawasaidia vijana hawa wenye moyo wa kujiunga na Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, kwa kazi yake nzuri pamoja na ushirikiano wake na wafanyakazi wake pamoja na wananchi kwa jumla. Baada ya hapo napenda tena kuwapongeza viongozi wa Jeshi pamoja na wapiganaji wake hasa hasa wapiganaji wa kambi za *14KJ* na *15KJ* walioko katika kambi za Wawi, Pemba, kwa jinsi wanavyofanyakazi kwa bidii na ushirikiano na raia. Nawapongeza sana na napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kuingiza fedha za kufanya ukarabati wa nyumba za askari zilizoko katika kambi za Wawi. Napenda pia kuishukuru Serikali kwa kutenga fedha za kufanya ukarabati wa Hospitali yetu ya Jeshi iliyoko katika kambi ya *14KJ* iliyoko Wawi kitendo hicho ni cha kuigwa mfano, maana hospitali hii ni ya zamani na imechoka sana zaidi ya kufanyiwa ukarabati naomba pia dawa zipelekwe kwa wingi kulingana na wagonjwa. Napenda kuipongeza Serikali kukubali kuwa eneo la Jeshi hili kujengwe *Supermarket* itakayohudumia familia za askari katika kambi ya *14 KJ* Wawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuunga tena mkono hoja mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, timu nzima ya wataalam wa Wizara, Mkuu wa Majeshi na Makanda bila kuwasahau maafisa na wapiganaji wote wa jeshi letu shupavu la Ulinzi na Ujenzi wa Taifa, kwa juhudhi wanazozifanya kuhakikisha usalama na utulivu wa Taifa letu kwa kuzingatia vema mawazo ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, napenda kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa kuwa Waziri amekiri katika hotuba yake, ukurasa 44 kwamba rasimu ya Sera ya Ulinzi ya Taifa ndiyo kwanza imekamilika, baada ya kuchukuwa muda mrefu kuliko ilivyotarajiwu na kwa kuwa utekelezaji mzuri na wa ufanisi wa Sera unahitaji sheria mahsusini kuhusu sera husika, pamoja na kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo, ni ushauri wangu kwamba Wizara iandae kwa haraka muswada na kanuni muafaka kwa shabaha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria na kanuni hizo zitaelekeza ushirikishwaji wa raia na ujenzi wa miundombinu ya barabara, madaraja na vivuko katika barabara za ulinzi, hususan mipakani kwa mfano Jimbo la Kigoma Kusini na Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Kagera kwa ujumla, ambako kwa sasa nyenzo hizo muhimu kwa ulinzi hakuna, hali inayofanya Majeshi yetu na vyombo vyetu vya Ulinzi na usalama vifanye kazi ya ziada na katika mazingira magumu. Kwa hiyo, Waziri aandae kwa kazi ya utendaji wa kijeshi Muswada na Kanuni na kuviwasilisha Bungeni.

Pili, kwa kuwa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa, Ukurasa wa kwanza imebainisha Wakimbizi kuwa mionganini mwa majanga/maafa ya Kitaifa, ni maoni yangu na ushauri kwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwamba barabara, madaraja/vivuko na magati katika mwambao wa ziwa Tanganyika viwekwe chini ya mpango maalum wa kuimarisha na kujengwa. Vikosi vya Ujenzi vya Jeshi na Watalaam/Wahandisi wa jeshi wahusika kikamilifu katika usanifu wa miundombinu hiyo. Pia usimamizi na ushauri wakati wa ujenzi huo uwe chini ya Wahandisi na wataalam Wanajeshi kwa shabaha ya kutunza siri na kukidhi mahitaji ya kijeshi. Ili azima hiyo ifikiwe vizuri Wizara ya ulinzi na Jeshi la Kujenga taifa, iwe kiungo cha Wizara za Ujenzi; Mawasiliano na Uchukuzi (magati, bandari, viwanja vya ndege) na Tamisemi (wananchi) katika kufikia maamuzi ya haraka.

Mfano dhahiri unaothibitisha umuhimu wa hatua za haraka ni mwambao wa ziwa toka mto Malagarasi katika Kijiji cha Ilagala hadi Kalya eneo linalojumuisha Kata sita za Ilagala Sunuka - Sigunga - Igulula -Buhingu na Kalya, Kilometra zipatazo 20 toka mto Malagarasi hadi Kata ya Sunuka. Wananchi katika sehemu iliyobaki wana ari kubwa kuchangia nguvu zao zote katika ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vamizi za mara kwa mara katika sehemu hii unashabikiana na ulivyobainishwa katika mchango wa Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Magharibi, Jimbo linalopakana na Kigoma Kusini. Barabara ya Ilagala Kalya (kilometra 150) imebainishwa kuwa ni ya Mkoa kulingana na jio grafia yake, hakuna shaka ina sifa zote kuwa ya Ulinzi. Katika kijarida kidogo kilichotolewa sambamba na hotuba ya Waziri katika ukurasa 5, kifungu cha 5, imebainishwa kwamba zitapatikana mashua mbili mwishoni mwa mwaka 2004 zitakazotumika katika Maziwa. Namwomba Waziri atamke wazi ni ziwa gani kwa sababu yapo mengi. Kwa hoja nilizojenga katika mchango wangu zina muafaka ni Tanganyika na kwa zote mbili, kukabiliana na ujambazi na uvamizi katika mwambao wa Ziwa Tanganyika unaojumuisha Mikoa ya Kigoma na Rukwa katika masafa yapatayo kilometra 500.

Tatu na mwisho ni suala la kuendeleza utafiti wa teknolojia ya Kijeshi kwa lengo la kuongeza uwezo wa jeshi kimapigano. Tatizo limekuwa ufinyu wa bajeti. Naunga mkono ushauri wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba Serikali ichukue hatua za makusudi kuongeza fungu la fedha kwa shabaha ya kuendeleza utafiti na maendeleo (*R & D*), si kwa shabaha ya kuongeza uwezo wa kupigana tu, ila pia kwamba ni mahitaji ya karne tulionyayo na kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana, wahandisi wa gari ya Nyumbu wanastahili pongezi za Watanzania wote. Ni hazina ya Taifa na fahari yake. Tuwaenzi na kuwapa nyenzo ili waboreshe gari hilo. Uboreshaji wa sehemu muhimu za gari hilo mfano, *exel* na *hub* na pia *gear box* vinahitaji akili iliyotulia, uvumilivu na udadisi pamoja na ubunifu usiokata tamaa. Serikali ina wajibu wa kuwapa wataalamu hao mazingira hayo. Nashauri fungu la utafiti liongezwe maradufu kama si mara tatu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati na za makamanda kwa niaba yao akiwemo Mkuu wa Majeshi yetu na wenzake wote na wafanyakazi wa Wizara yetu ikiongozwa na Katibu Mkuu kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana kwamba Waheshimiwa Wabunge wamechangia hotuba hii kwa hali ya uwezo wao na ufanisi wa hali ya juu, nasema Waheshimiwa Wabunge ni askari wa akiba kwa kuwa jinsi walivyochambua hotuba hii nimefarijika na nimeona tuna askari wa akiba.

Matatizo yaitokea Mheshimiwa Bernard Membe, usiwe na wasiwasi, tunawafahamu wenzetu vizuri sana na wao wanatujua fika, wametuomba waje hapa wajifunze kutoka kwetu, tumekataa. Hili Jeshi sio Jeshi la kuchazea, Jeshi hili lina historia ndefu sana kama nilivyosema katika hotuba yangu, limetokana na busara na hekima na upeo wa kuona mbali wa waasisi wetu Baba wa Taifa, Marehemu Julius Kambarage Nyerere na mwanamapinduzi wa Bara la Afrika Hayati Abeid Aman Karume. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa Uganda nchi moja na nchi nyingine wakasema, mllichofanya Tanzania hakikuweza kufanya katika nchi yoyote. Tulivunja Jeshi, likasukwa upya, vijana wa JKT, vijana wa *Afro Shiraz* na Vijana wa TANU wakaungana, wakajenga Jeshi imara kweli ambalo linatokana na matakwa na matarajio ya wananchi. Kwa hiyo, hili ni Jeshi ambalo limejengwa kwa msingi wa wananchi.

Kwa hiyo, nataka niwatoe wasiwasi hata wenzeu wawe na vifaa hivyo vingi, vifaa haviwezi kushinda vita, vita vinapiganwa kwa mambo matano, siasa safi, saikolojia, pamoja na mambo mengine. Kama huna haya, hata uwe na silaha ya aina gani utashindwa tu. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba, Jeshi hili lipo imara, tunajua uwezo wa wenzetu na hatutaki kusema na hata bajeti yetu siyo mbaya na mambo haya mahali pengine hatuvezi kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wao pia ni wanajeshi wa akiba kwa michango yao ambayo kwangu ni kutambua kazi nzuri waliyofanya Wanajeshi wetu kwa kipindi cha miaka 40 tangu kuundwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, wamesisitiza na kuweka msimamo wa wananchi ambao wanawawakilisha kuwa jukumu la ulinzi ni jukumu la Taifa, ni jukumu la Watanzania wote bila kujali itikadi ya kisiasa, dini, jinsia, rangi, kabilia au sehemu anakotoka Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashakikishia Watanzania kwa kupitia Waheshimiwa Wabunge wao kuwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litaendelea kulinda nchi yetu kwa nguvu zote na kwa uwezo wote kama walivyofanya tangu tulipopata Uhuru wetu na tangu kuzaliwa kwa Muungano wetu chini ya uongozi shupavu wa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Rais wetu, wapiganaji wetu kamwe hawatatetereka wala kuyumbishwa katika suala la ulinzi la Taifa letu. Hakuna suluhu katika hili. Mlale salama, ambaye anataka kwenda kufunga ndoa, sherehe zifanywe, ulinzi ni imara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyokuwa kauli mbiu ya Majeshi ya Ulinzi inayosema: “*give us the tools we will finish the job.*” Kwa lugha nyingine tupeni nyenzo tutamaliza kazi tuliyopewa. Tunachotaka sasa tupitisheni bajeti, vijana watafanya kazi mliyowakabidhi hii ndiyo kauli mbiu. Haya mengine tusizungumzie maana ni mambo ya Jeshi. Vitu vinapita pita hapa tunaviona na tunajua wanapata mafunzo kutoka wapi, lakini hiyo isiwatishe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hotuba yangu kwa kauli na kwa maandishi na ningependa kuwahakikishia wao na wapiga kura wao kwamba tuna Waheshimiwa Wabunge mahiri sana, Bunge hili siyo Bunge la kuchezewa. Bunge hili katika ulinzi halina itikadi pamoja na kwamba rafiki yangu ameniambia mambo mengi ambayo nitakuja kumweleza na mengine tuwaachie Jeshi maana kamwe kama wewe siyo mwanajeshi usiyazungumzie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwatambua waliochangia kwa kauli. Kwanza napenda kumshukuru kwa moyo wa dhati Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. Unajua ukizaa mtoto amekua, bado ni mchanga unamwona anapevuka na anapochangia mambo yenyé hekima unafurahi sana.

Leo nimeona mtoto wetu, mjukuu wangu, ndugu Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, amekuwa tofauti kabisa. Hii imetokana na ushauri ambao ninampa mara kwa mara. Asipayuke afuate nyayo na naona anaifuata nyayo. Nakushukuru sana mjukuu wangu kwa mchango wake mkubwa. (*MakofiKicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kauli ni 13 ambao ni hawa wafuatao:-

Kwanza, namshukuru mzee wangu ambaye amenilea kisiasa nilipokuja hapa tangu amekuwa Waziri Mkuu wangu nimejifunza mengi kutoka kwake na tunamshukuru Mwenyezi Mungu bado anampa afya njema amemjalia, tunamhitaji sana, huyo siyo mwingine ni Mheshimiwa John Samwel Malecela, ambaye ni Mwenyekiti wetu. Mheshimiwa *Major Jesse Makundi*, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Jina Khatibu Haji, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mheshimiwa Shaibu Ahmad Ameir, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji na mwisho siyo mwingine mtetezi mkubwa wa Jeshi letu, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi orodha ni ndefu kweli wako 56 ambao ni Mheshimiwa Dr. Abdulkadir Shareef, Mheshimiwa Aggrery Mwanri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Dr.

Thadeus Luoga, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Esther Nyawazwa na Mheshimiwa Danhi Makanga, mtoto mpotevu, amerudi zizini. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Eliachim Simpassa.

Naomba radhi kama nimesahau mtu ye yeyote wanisamehe. Mheshimiwa Karim Said Othman. Nawashukuruni wote kwa michango yenu ambayo imetusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kabla sijaanza kujibu michango ya Waheshimiwa Wabunge, nataka ni wahakikishieni kwamba haya yote mliyoyatoa ni muhimu sana katika ulinzi wetu. Jeshi lina tabia moja utekelezaji tu. Timu ya Majeshi wako pale watatekeleza. Lakini nataka ni wahakikishieni kwamba tutayajibu kwa maandishi na kwa ufasaha kabisa na pale ambapo hatukutekeleza, tutaeleza sababu. Kwa hiyo, kabla Bunge halijamalizika tutayachapisha, tutawapatia mmoja, mmoja ili msiondoke na mawazo kwamba tumepuuza mawazo yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie mwenzangu ambaye ni Waziri Kivuli kwa kweli namheshimu sana kwa mawazo yake, ametusaidia kwa mengi sana ni Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi. Namheshimu sana kutokana na taaluma yake kama *Major* Mstaafu ambaye anajua taratibu na kanuni za Jeshi kama alivyofundishwa na kutii.

Namshukuru kwa kuwa ameunga mkono hoja kama alivyosema kutokana na fani yake kama Mwanajeshi. Lakini katika hotuba yake kuhusu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa kuna ubadhirifu mkubwa, mbaya wa fedha za walipa kodi zisizo na maelezo. Kama Mwanajeshi, angepaswa kufanya utafiti na kupata maelezo kwa wanaohusika na angepata jibu sahihi la kijeshi kama ilivyoainishwa katika kanuni za Majeshi ya Ulinzi juzu ya tatu kuhusu matumizi ya fedha. Fedha za walipa kodi ambazo wametengewa Wanajeshi zinasimamiwa kwa nidhamu ya hali ya juu sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hii ni sehemu ya nguzo mojawapo za Majeshi yetu ambazo ni utii, uhodari, uzalendo, nidhamu ya hali ya juu maelezo katika hotuba yake ukurasa wa tatu, ametia chungu chumvi kidogo kwa kuwa hakufanya utafiti wa kina. Sasa nataka nimtoe wasiwasi na wananchi wote hakuna fedha zilizopotea, hakuna fedha zilizoliwa na Jeshi lina tabia moja ukipoteza fedha ni *Court Martial* na yeye anajua wameshafungwa wengi na kufukuzwa kazi. Kazi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kutoa

maelezo kwa mambo ambayo hayajaelezwa na hayajapata maelezo ya kutosha na ya kina ndiyo ameona katika kitabu kile katika aya ya 173.2 na kuendelea ni mashaka siyo kwamba fedha hizo zimepotea. Kwa hiyo, ningeomba kama Mwanajeshi arekebishe kauli hiyo kwamba hakuna kitu ambacho kimeharibika. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za ukaguzi shilingi 5,351,595,809/=, mwaka wa fedha 2000/2001 ilihusu hoja za ukaguzi nne zilizohusiana na kutopatiwa nyaraka kwa wakati. Hivi sasa nyaraka zote zimeishapatikana, nyaraka hizo ni pamoja na zilizohusu ununuzi wa nyumba ya *DA Nairobi* nyaraka zimeishawasilishwa kwa Mkaguzi, hakuna fedha zilizopotea. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, masurufu ya shilingi 42,966,778/=, mwaka 1999/2000 aya 169 katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali masurufu yote yamerejeshwa na Wakaguzi wamefahamishwa. Matumizi ya shilingi 109,833,911/= yanahu hoja ya kwanza ya kuwasilisha nyaraka kwa Mkaguzi zilizotumika kununua nyumba za *DA Nairobi* na Kinshasha nyaraka hizo zimeishawasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya ununuzi wa *Sum Brown Belts* shilingi 125,538,000/= aya 177 ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali taratibu za kuidhinisha ongezeko la bei lilitokana na kushuka kwa thamani ya shilingi kati ya viwango wakati wa kuagiza na wakati wa kupokea na hiyo imeisharekebishiwa. Mishahara ya kutatanisha aya 178 mwaka wa fedha 2000/2001 shilingi 544,804,734/= malipo hayo yalihu malipo ya rambirambi na posho za Madaktari. Rambirambi ya mwanajeshi anapokufa lazima azikwe kwa heshima, huwezi kungojea tena kwamba lazima mkae mzungumze. Posho za Madaktari ambazo hulipwa baada ya tukio ambazo nyaraka zake hazikuwa zimepatikana kwa wakati kwa kuwa zililipwa Mikoani kuititia *BOT* na *NMB* hivi sasa nyaraka hizo zimekwishapelekwa kwa Wakaguzi kwa ajili ya uhakiki na hoja kufungwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya hoja za ukaguzi kweli ziliwu 48 kati ya mwaka 1998, 1999, 2000, 2001 sasa zimebaki hoja saba tu na zilizobaki kesi ziko Mahakamani sasa kama anataka tuingilie Mahakamani tunaweza Kijeshi, lakini tunavunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujira na maslahi kwa Wanajeshi, mishahara imeendelea kuboreshwa kwa kuzingatia mapendeleko ya *CDF* na uwezo wa Serikali kifedha. Mradi wa Meremeta kuna uwazi kweli kweli na tunamkaribisha aende akatembelee hata mjukuu wangu anaweza kwenda kutembelea kwa sababu akienda kule tutampatia usafiri wa kwenda kwao, hawana usafiri kule Kagera, iko wazi kabisa, nimekwishaeleza katika ukurasa wa 35 na 36 kwenye hotuba yangu. Mapitio ya posho mbalimbali *Ration Allowance* na *Hardship Allowance* Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina ili kuona viwango vinavyolipwa vinaenda na wakati na tumeishawakilisha. (*Makofit/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya kustaafu kufanyiwa mapitio, hili ni suala la sera litazingatiwa tutakapoandaa sera mpya. Pensheni kwa wastaafu wa miaka ya zamani hili ni suala la Kitaifa na lilizungumzwa na Waziri wa Fedha na Wanajeshi pia wanafikiriwa itakapotokea. Ni mambo ya Kitaifa hatuwezi kuyaingilia. Nayy kutumika kudhibiti uvuvi haramu wanafanya. Eneo la kujenga uwanja wa mashujaa Dodoma nimeeleza katika hotuba yangu. Halafu kukiukwa kwa taratibu za ununuzi wa zabuni hakuna taratibu ambazo zimekiukwa.

Sheria ya manunuzi ilipitishwa hapa Bungeni mwaka 2001 na inazingatiwa. Yapo maelekezo mahsusni ambayo *CDF* amempelekea kila Mkuu wa Kikosi na maelezo yanayatakiwa jinsi fedha zilizotumika. Lazima walete maelezo kwamba ni shilingi ngapi na Jeshi limesifiwa hata na Wakuu wa Nchi kwamba Taasisi zingine zifuate mfano wa Jeshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa *Major* Mstaafu Jesse Makundi, kama alivyosema nafikiri ni *communication breakdown*, laiti angejua, angekuta mambo yote haya yamekwisha. Baada ya maelezo hayo, nafikiri ameridhika na atakwenda kueleza kwamba aliyoyleza si sahihi, kama Mwanajeshi najua atafanya hivyo na asipofanya hivyo bado yeye ni Mwanajeshi wa akiba na unajua kwamba Mwanajeshi asipofanya mambo anayoagizwa na Waziri wake wa Ulinzi maana yake nini? Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, nakushukuru sana. Hayo yote Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, ameyasema kwa sababu ana uchungu na Jeshi na kwa kweli mimi amenisaidia mambo mengi na yeye ni mshauri wangu mkuu katika Bunge na yeye ni Mjumbe wa Kamati yetu na amechangia vizuri tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna mambo mengi ambayo wametuasa Waheshimiwa Wabunge, mengine ni ushauri, mengine ni maombi na mengine kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Bernard Membe, ni kutoa taarifa kwamba tuchukue tahadhari na tumesikia na mimi ninamshukuru sana. Ni mchangiaji mzuri sana, mimi sina wasiwasi kwa michango yake katika kuboresha Jeshi hili, tumefaidika sana. Wakati wa kupitia rasimu ya sera, alitoa michango mizuri sana naomba aendelee kutusaidia kwa sababu Jeshi hili ni letu sote.

Sasa nimegawa maeneo 18 muhimu kwa wote waliochangia kwa sababu muda hauniruhusu mambo ni mengi. Suala la matatizo ya usafiri na vitendea kazi hili limechangiwa na Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Jina Khatibu Haji, Mheshimiwa Ibrahim Marwa na Mheshimiwa Leonard Derefa. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kila jitihada inafanyika ili kutatua tatizo hili hatua kwa hatua. Lakini nataka niwahakikisheni pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wameomba na kuna matatizo sugu ya usafiri pamoja na *Ambulance* tutapeleka usafiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mipaka na maeneo ya Jeshi limechangiwa na Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Jina Khatibu Haji na Mheshimiwa Danhi Makanga, mambo ni mengi sana. Mwingine amesema makambi ya Jeshi yasiwe karibu na ndani ya Miji, yaende mbali.

Mwingine amesema watu wake wanataka fidia na wengine wamesema kwamba kwa nini Jeshi letu katika makambi yao wameteketeza mabomu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi nyingine sasa wanafurahia. Nasema kwamba msiwe na wasiwasi huo ni Mkataba wa *OTAWA* kwamba nchi zote ziteketeze mabomu ambayo yako kwenye maghala. Lakini kuhusu mafunzo bado tuna mabomu ya kuwafundishia vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni maeneo mengi hayakuwa na matatizo, hata hivyo, wananchi wamekuwa wanayaingilia na hivyo hatua za sasa za kuyapima maeneo hayo zimeishaanza. Waheshimiwa Wabunge, Jeshi halina ugomvi na wananchi, Jeshi linategemea wananchi na wananchi wanategemea Jeshi. Pale ambapo tumeona kweli wananchi wameweka miradi yao ya kudumu tunapima upya eneo na hivyo ndiyo tumefanya katika sehemu nyingi. Lakini Makao ya Jeshi hata ikiwa katikati ya Mji ni Makao Makuu ya Jeshi na Mwenyekiti ametusaidia sana Mheshimiwa John Malecela, kutokana na hekima na uzoefu wake, amefanya mambo mengi kuhusu Jeshi letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la kukubaliana tu, ni hatua ngapi wananchi wangejenga kule. Maeneo haya ya Jeshi ndiyo yalitangulia kabla ya wananchi hawajajenga. Sasa mvamizi ni nani? Jamani katika nchi nyingine hatuzungumzi kama tunavyozungumza, hutolewa kwa nguvu. Mheshimiwa *Major Jesse Makundi*, anajua na hakuna kauli. Sasa hili ni Jeshi la wananchi na ni vijana wenu. Wanajeshi wanasesma, sheria imesema hivi, kwa nini nyie wanasiaya mnatuvuruga? Nikasema hapana, nendeni polepole. Werezo tumelipa fidia kama Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, alivyosema tumewalipa, Oldonyo Sambu tumewalipa, lakini wao ndiyo wamevamia. Kwa hiyo, nataka niwatoe wasiwasi Mheshimiwa Stephen Kazi na wengine kwamba Jeshi hili nafikiri mngefurahi kama Jeshi liko karibu na Mjini maana mkipata matatizo mnakwenda kuwaleta, vinginevyo mambo yatakuwa vibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *strategic areas* pale Mjini ambayo Jeshi lazima lilinde. Nimekwenda China, majeshi yako kwenye kona *strategic area*. Hasa tukienda Ngorongoro huko mtatufuata tu. Mwanajeshi wakishakuwa pale, wananchi wanasesma usalama wao upo na wanawafuata tu. Kwa hiyo, hili nawahakikisheni kwamba ishini na amani na Wanajeshi wenu watalinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la hospitali ya Bububu, Mheshimiwa Jina Khatibu Haji, Mheshikiwa Haji Juma Sereweji na wengine waliochangia. Suala la Bububu na suala la Wawi, kwa kuwa kuna hisia potofu kwa nini Wawi, Wawi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka niwahakikisheni Pemba ni sehemu ya Tanzania na Pemba iko mbali sana na Unguja na nchi kavu. Sasa ndugu zetu hawa tusiwapelekee huduma ya kuaminika? Lazima tuimarishe Vikosi vyetu Pemba. Sasa maskini Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar ,akisema, ehee, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nampongeza sana, wote mngesema kama Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, nchi hii ingeendelea sana. (*Makofi*)

Kwa hiyo, suala la kuboresha Bububu halina mjadala, kuna marafiki zetu wamejitokeza wanataka kubomoa Bububu wajenge hospitali mpya ya kisasa na tumewambia njooni. Nilikuwa katika Umoja wa Falme za Kiarabu, wamekuja wamesema tutawajengeeni. Wajerumani wako tayari, sasa atakayetangulia ndiyo bora zaidi. Tunataka Bububu ile iwe ni Bububu kweli kweli. Hata viongozi kutoka Bara wanaweza kwenda kule kutibiwa, mandhari yake ni nzuri ni mahali ambapo unaweza kujenga *Five Plus Star Hotel*. Kwa hiyo, Bububu tutaifanyia kazi kweli kweli na itakuwa hospitali ya kujivunia. Tumepeleka *X-Ray*. Yale mambo ni ya *transitional* ni ya muda tu, lakini tuna mpango kamambe wa kuboresha Bububu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, faida tulizopata kutokana na ukombozi, mimi nawashukuru sana waliochangia suala hili na mtu aliyelichangia vizuri sana ni Mheshimiwa Jackson Makwetta.

Mheshimiwa Jackson Makwetta, namheshimu sana kwa uzalendo wake amesema hivi: "Watanzania hatukwenda kuwakomboa wenzetu kwa lengo la kutafuta faida yoyote ila ukombozi. Leo tunafurahi kuona wenzetu nao wako huru, Uhuru wetu ungekuwaje, usingekuwa kamili kama tungezungukwa na wakoloni. Nini thamani ya damu inayookoa maisha ya mtu ambaye angekufa." Mwisho wa kunukuu. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niwambieni mzee Nelson Mandela, baada ya Uhuru wa nchi yake alisema Watanzania wametufanya makubwa, sasa anaagiza wawekezaji wake wasaidie Tanzania. Popote tunapokwenda ile heshima tunayoipata ni kubwa mno. Katika vikao mbalimbali jina la Tanzania ni kubwa na vijana wetu wakienda Angola, Msumbiji, Mtanzania umaheshimika sana. Tuwashukuru waasisi wetu kutujengea heshima hii hata vizazi vijavyo hawatatusahau, tumefanya kazi hii kwa wajibu wetu kama Waafrika na kama binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa siwezi kueleza hayo ni mambo ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ndiyo wanajua ushirikiano tulionao. Lakini mimi nawahakikisheni popote ninapokwenda kwenye mikutano, Tanzania wanatuheshimu sana, nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmekwenda katika vikao mbalimbali mmeona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo katika Majeshi hili limechangiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Jackson Makwetta. Sasa leo nizungumzie kwa muhtasari huyu kijana, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, ambaye ni Mheshimiwa, kwanza nataka baada ya kumpongeza azingate mila na desturi, siyo kuropoka ropoka kwa wakubwa zake na babu zake ili kusema kwamba upara sijui una hekima, ni kukosa adabu. Lakini namsamehe kwa sababu leo amezungumza vizuri, angefanya fujo leo ningemmaliza kweli kweli. Lakini kukulaani, sitakulaani, lakini leo amezungumza mambo ya maana kweli, *reform* ya Jeshi.

Sasa sijui mambo hayo ameyapata kutoka wapi? Lakini kama ndiyo mwenendo wake atafika mbali na nafikiri ndiyo Kambi ya Upinzani wameona akili zako hizo ambazo zimetokana nasi na wakakuchagua kuwa Msemaji wao Mkuu. Lakini hii nataka niiweke kwenye *record* kwamba aendelee kushika uzi hivyo hivyo na sikiliza maoni ya wakuu, usipayuke. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo katika majeshi imechangiwa pia na ndugu Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Lucas Selelii. Michezo ndani ya Majeshi ni sehemu ya kazi na hupewa uzito unaostahili. Kuna wakati tulisema laiti Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lingepewa timu ya Taifa, lakini tuwezeshwe tu hiyo timu ingevuruga timu nyingi sana katika Bara la Afrika. Kuna nidhamu ya hali ya juu na kwa kweli mafunzo mazuri. (*Makofi*)

Ushirikiano kati ya Majeshi, umechangiwa na Mheshimiwa Ali Machano Mussa na Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga. Ushirikiano ni mzuri na ipo mikutano kati ya viongozi wa vyombo na pia michezo ya majeshi kila mwaka. Matatizo ya posho, mafao na malipo ya nauli za safari na kadhalika, limechangiwa na Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Anatory Choya na Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi. Limekuwepo tatizo la muda mrefu hata hivyo kwa sasa ipo Kamati Maalum inayosughulikia suala hili na hasa mafao.

Tumeandaa mikakati ya kuboresha Jeshi ya miaka 15 na ningepata muda ningewaeleza mambo yaliyofanyika. Ukilinganisha na huko nyuma ni makubwa sana. Wanajeshi wetu siku hizi wanakula kama Wanajeshi, wanavaa kama Wanajeshi, wanakuwa nadhifu sana wanakwenda likizo mpaka fedha za likizo zinabakia. Hata wale wanaokwenda Kagera wanakwenda. Mambo mengi yamefanyika, lakini haya yametokana siyo na sisi, bali yametokana na Amiri Jeshi Mkuu. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Omba hela.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni Waziri wa Ulinzi na mkubwa wangu Mheshimiwa John Malecela, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na usalama, ameniambia omba hela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kutoa hoja kwamba mtupatие hizo fedha tuzifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 38 - Ngome**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... 136,634,251,500/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge ni kweli upande huu sikuangalia. Kwa hiyo, kama alisimama tumpe nafasi. Lakini niwakumbushe kwamba Mheshimiwa Waziri hapa alikuwa na saa nzima ya kujibu, mmemkatisha katika nusu saa. Sasa sizuii mtu kutaka ufanuzi. Lakini naomba hilo nalo mlifikirie. Angefanua hapa ingekuwa mambo mazuri, lakini mkamwambia omnia hela, omnia hela. Kwa hiyo, ameomba hela. (*Makofi*)

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina sababu ya kushika hela ya Waziri. Ila tu nilitaka nipate maelezo kidogo. Hivi karibuni nilivyotembelea Jimbo langu la Kigamboni kuna kikosi cha *Navy*. Kikosi kile kina tatizo la maji la muda mrefu sana. Nilitaka tupate maelezo kama Waziri ameshashughulikia kiasi gani suala hilo ili vijana wapate maji. Kwa sababu kikosi kile ni muhimu na kutokana na umuhimu wa shughuli zao.

Lakini la pili, nilitaka pia nipate maelezo kwa sababu kikosi kile cha *Navy* vijana wanastaa fu wangali bado vijana sana na kuondoa wataalamu ambao wangetumikia angalau miaka kumi inayokuja zaidi, je, Waziri ana utaratibu gani au Serikali ina utaratibu gani kuwapa mkataba wale ambao wamestaafu ambao bado tunawahitaji katika Jeshi. Ni hiyo tu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, uwe unasiliza kwanza kwangu. (*Makofi/Kicheko*)

Nilikuwa nasema kifungu hiki ni cha Ngome. Kama ni mshahara ni wa Mkuu wa Majeshi. Sasa nadhani umesema mshahara wa Waziri hapa sio penyewe. Lakini hata hivyo nitampa nafasi aweze kujibu. Mheshimiwa Waziri jibu. (*Makofi/Kicheko*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumjibu ndugu yangu, mwanachama mwenzangu kama ifuatavyo, hapana. Suala hili limefafanuliwa vizuri sana na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Wametupa kazi ya kufanya walipotembelea *Navy* na tumezingatia kutokana na agizo la Kamati ambayo Mheshimiwa Dr. John Malecela, ameliweka vizuri sana na tutazingatia pamoa na mambo ambayo ameyagusia. (*Makofi*)

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ningesubiri niende mahali penyewe kwa sababu kama ulivyoeleza.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 - *The National Service Force* ..... 27,561,135,300/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

### **Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ..... 4,679,818,500/=

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 10 *Sub Vote 1001*, mshahara wa Waziri. Mimi sina haja ya kuchukua huu mshahara, kwa sababu nikiuchukua atanipa matatizo bure kumlisha mjukuu mtu mzima na mwenye kipara kama huyu ni kazi kubwa.

Lakini ningeomba Mheshimiwa Waziri anifafanlie kuhusiana na jambo tulilolizungumza kwenye hotuba yetu, kwamba mafao na haki za wastaifu katika Jeshi na mojawapo ni Wanajeshi wastaifu waliokuwa katika kikosi cha Mizinga ambao walidai madai yao ndani ya Mahakama Kuu na wakapewa haki yao kwa misingi ya kisheria na ikaagizwa kwamba walipwe mafao yao. Lakini wameendelea kuzungushwa, wameendelea kupata matatizo wakienda pale wanalipwa kwa mafungu mafungu mara shilingi laki mbili. Mtu anadai shilingi milioni nane analipwa shilingi laki mbili au tatu. Sasa mimi huyu Mheshimiwa Waziri ningeomba tu anisaidie, anitolee ufanuzi hawa watu anawalipa lini ili waache kumuamkia pale kila siku asubuhi wanadai madai yao mpaka sasa. Hilo tu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, amezungumza ningempatia matatizo kweli na kweli ningempatia matatizo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wastaifu linashughulikiwa chini ya taratibu za Serikali na Hazina. Tunalifahamu suala hilo. Lakini kama mtu amekwenda Mahakamani na Mahakama imeshaamua hatujapata habari. Lakini kuna wastaifu ambao kwa kweli wana matatizo tutayashughulikia. Ningemwomba Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, aje Ofisini kwa sababu hili ni suala pana zaidi siwezi kufafanua hapa. Lakini kwa ujumla nitafafanua, aje atakunywa kahawa kutoka Bukoba. Nitamwonyesha na nitamweleza zaidi kuliko muda huu kuja kueleza mambo ambayo kwa kweli ni mengi na yana milolongo mirefu sana. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, punguzeni utani m-zero *in kwenye hoja.* (*Kicheko*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba tu Mheshimiwa Waziri kwamba nimeeleza kwamba hili suala ni jambo ambalo linagusa maslahi ya watu. Mimi ameniita kwamba niende tu kwake tukazungumze. Kwa kuwa hawa watu nafikiri kwa faida yao ningeomba tu aeleze ni kwamba anategemea litaisha lini? Hilo tu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nilifanya kosa kumpongeza. Suala hili la madai huwezi kusema kwamba litakwisha lini. Kama wako Mahakamani na wameshaauriwa Mahakamani, ni suala ambalo kwa kweli ni utekelezaji wa Serikali. Sasa nikija kusema hapa na sijui ni wangapi. Ningewomba akubali tu Jeshi lina utaratibu wake na Jeshi lina sheria zake na kama wameagizwa watalipa. Maana ya kumwagiza pale aje kule ofisini nitamwambia itakwisha lini na haya mambo ya kule. Sasa anataka nimweleze hapa yatakwisha lini kumbe nilifanya kosa kusema kwamba anafuata nyayo. Lakini nimemsamehe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stephen Kazi, ulisema unangoja kifungu hiki.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimechangia kwa maandishi. Nimejaribu kuelezea tatizo la wakazi wa Mwanza eneo la Nyashana ambako kuna kituo cha Jeshi pale. Nilishaleta taarifa kwenye Wizara na Waziri nilishawasiliana naye kuhusiana na kuvunjwa kwa nyumba za wananchi pale. Kwa sababu kubwa ni kwamba eneo lile sasa ndilo linapimwa. Kuna wananchi walikuwa wanakaa kwenye maeneo yale hawajui kwamba wako katika maeneo ndani ya Jeshi. Sasa hili tumejaribu kulifanya kiutaratibu wa ndani kwa ndani.

Nilitaka tu Waziri anipe uhakika kwamba kwa sababu tulimwomba kama anaweza kupata nafasi afike kule pia aone na pia aonane na wananchi wale ambao bado wengine wanakaa kwenye mahema kwenye maeneo mbalimbali baada ya nyumba zao kuvunjwa. Sasa nilitaka tu kupata uhakika wa Waziri kwamba jambo hili analichukua namna gani na kama anaweza kuahidi kwamba atakuja Mwanza nitashukuru sana aje tulione lile jambo wananchi wale tuwaone na pia tuamue hili jambo la kuzungumza. Kwa sababu ni urafiki pande zote. Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Stephen Kazi, kwamba nimejitahidi kuja Mwanza kuonana naye lakini tunapishana kila wakati.

Suala hili tunalijua Mheshimiwa Stephen Kazi, kwanza nimpongeze na nataka niwahakikishie wananchi wa jimbo lake kwamba wana Mbunge kweli kweli. Kama wananchi wa Mwanza katika jimbo lake waliweka vitu vya mradi wa maendeleo ndiyo maana nilitaka nifike na Mkuu wa Mkoo na viongozi wa Wilaya tukae pamoja na wananchi. Jeshi haliwezi kuwaonea wananchi na Mheshimiwa Stephen Kazi, nakuhakikishia kwamba mwezi Septemba, 2004 wakati nakwenda jimboni nitapitia

kwako lakini safari hii uwepo jimboni ili tuweze kumaliza tatizo hili. Kwa sababu huko nyuma ulikuwa na kazi nyingi. Mara umekwenda kwenye mkutano pale Mwanza kukupata ilikuwa ni kazi kubwa na kwa kweli unafanya kazi kubwa sana na wananchi wa Mwanza Mjini mna Mbunge hodari sana katika jimbo lenu. (*Makofit*)

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo tu. Mwaka 2003 katika Bunge hili nilichangia kuhusu ukarabati wa kambi ya Mtoni. Nikaeleza kwamba moja ya kambi kongwe pale Zanzibar ni kambi ile ya Mtoni na ni kambi ya kihistoria. Sijaona juhudzi zake na sikuona jibu lolote.

Ningemwomba Mheshimiwa Waziri alithibitishie Bunge lako hivi leo ukarabati huo sasa utafanyika lini?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu wetu wa Chama chetu na Mbunge. Nataka nimhakikishie kwamba kambi ya Mtoni tumeipa kipaumbele. Historia ya Mtoni tunaifahamu katika Mapinduzi matukufu. Nataka nimhakikishie kwamba kama nilivyosema nilipokuwa nasoma hotuba yangu kwamba ukarabati mkubwa sana umefanywa na vikosi vyetu vya JWTZ na JKT.

Kama hakuona nafikiri itabidi niende Zanzibar ama aje ofisini tuagize viongozi wa vikosi watamweleza. Lakini kambi ya Mtoni ni moja ya makambi ambayo tumeyaweka katika orodha yetu kuikarabati jinsi tutakavyopata fedha. (*Makofisi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko voyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

## **Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 2001 - Industries, Construction and Agriculture..45,010,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko vovote)*

*(Bunge lilirudia)*

## TAARIFA

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kuketi kama Kamati ya Bunge ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005 kwa ajili ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote, naomba kutoa hoja kwamba makadirio hayo sasa yakubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa  
kwa Mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.48 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne  
tarehe 3 Agosti, 2004 saa tatu asubuhi)*